## MAMBO YALIYO KITABUNI


| *Sura* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| | Utangulizi | 5 |
| 1 | Kristo ni Mungu | 13 |
| 2 | Utu wa Kristo | 21 |
| 3,4 | Raha yetu | 29 |
| 5,6 | Kuhani wetu mukubwa | 37 |
| 7,8 | Melkisedeki na agano zuri kupita | 46 |
| 9 | Kuhani mbinguni | 53 |
| 10 | Zabihu inayotosha | 60 |
| 11 | Imani | 66 |
| 12,13 | Mwenendo katika imani | 73 |

# *Utangulizi*

Barua kwa Waebrania inatukumbusha maneno makubwa juu ya Bwana wetu Yesu Kristo - uungu wake, umutu wake, ufufuko wake toka wafu, kwenda kwake mbinguni, na ya kwamba atarudi tena. Lakini kuna maonyo mengi vilevile ndani ya barua hii.

Mbele ya kuanza kusoma na kueleza barua hii tuone kwanza kama iliandikwa kwa watu gani, kwa wakati gani, na kwa sababu gani. Kujua maneno haya kutatusaidia kufahamu nini Mungu anataka kutufundisha sisi kwa njia ya barua hii, na roho zetu zitafurahishwa na maneno ya ajabu tutakayosoma juu ya Bwana wetu Yesu Kristo. Kutatusaidia vilevile kupokea maonyo ya barua hii kwa sisi wenyewe na kuyanyenyekea. Haifai tujifurahishe na maneno matamu tu tunayoyasoma ndani ya Biblia bila kuwaza na kunyenyekea maonyo yanayoandikwa ndani yake kwa sisi. Tukumbuke ya kwamba barua kwa Waebrania ni sehemu ya Neno la Mungu lisiloweza kugeuka kamwe.

**Barua hii iliandikwa kwa watu gani?**

Iliandikwa kwa Waebrania, ndio Wayuda, waliokwisha kuamini Bwana Yesu kuwa Masiya na Mwokozi wao. Tukisoma barua hii polepole tutaona ndani yake maneno mengi kidogo Wayuda waliyojuana nayo kupita watu wa Mataifa, kama ukuhani, hema takatifu, kazi ya makuhani na zabihu walizozitoa. Tutasoma juu ya historia ya Waisraeli na habari za watu wa Mungu wa zamani. Hivi barua hii haikuandikwa kwa watu wa Mataifa waliogeuka Wakristo, lakini kwa Wayuda waliokuwa wamekwisha kupokea Yesu kuwa Masiya wao.

**Iliandikwa kwa wakati gani?**

Maneno mengine ndani ya barua hii yanatusaidia kufahamu kama barua hii iliandikwa kwa wakati gani. Ona maonyo ndani ya 13:7: *''Kumbukeni waongozi wenu waliowaambia ninyi Neno la Mungu; na kwa kuangalia mwisho wa miendo yao, fuateni imani yao.''* Shairi hili linatufahamisha ya kwamba wengine wa wazee waliochunga Wakristo hawa walikuwa wamekufa. Hivi tunafahamu ya kuwa kwa wakati huu

makanisa yalikuwa yamesimamishwa, na wale waliokuwa waongozi ndani ya makanisa haya kwa mwanzo wao walikuwa wamekufa. Hivi muda fulani ulikuwa umepita, labda miaka 20 ao zaidi, tangu Wayuda hawa waliposikia Habari Njema mara ya kwanza. Lakini shairi 13 la sura 8 linatuleta kufikili ya kwamba barua hii iliandikwa mbele ya 70 A.D. (miaka 70 nyuma ya kuzaliwa kwa Kristo).

Soma shairi hili tena polepole. Ona ya kuwa mwandishi hakusema ya kwamba agano la kwanza lilikuwa limetoweka. Alisema lilikuwa **karibu na** kutoweka. Anasema kuna agano jipya sasa na kwa pahali pengine ndani ya barua hii anatujulisha ya kwamba kwa agano hili jipya inapasa watu kuabudu namna nyingine. Agano la kwanza lilikuwa na hema na makuhani na sadaka. Lakini sasa kulikuwa na agano jipya na neno hili lilifanyiza agano la kwanza kuwa agano la zamani. Tunajua hekalu liliharibiwa kwa mwaka 70 A.D. lakini ndani ya sura 9 mwandishi aliandika juu yake sawasawa lilikuwa likisimama kwanza na makuhani walikuwa wakifanya kazi yao ndani yake.

Maneno haya yote yanatusaidia kufahamu ya kwamba barua hii iliandikwa muda mudogo mbele ya 70 A.D. Kwa mwaka 70 A.D. majeshi ya Waroma walikamata Yerusalema na kutimiza unabii wa Bwana Yesu ya kwamba *''halitabaki jiwe juu ya jiwe pasipo kubomolewa''* (Matayo 24:2). Hivi agano la kwanza lilikuwa karibu kutoweka na agano jipya lilikuwa limesimamishwa lakini lilikuwa kwanza zaifu.

### Wasomaji

Wasomaji wa barua hii walikuwa Wayuda, kama tulivyosema mbele. Kwa kutusaidia kufahamu mawazo yao tuangalie mashairi mengine ndani ya sura 10. Walikuwa Wayuda lakini walikuwa wakipata mateso ya kuogopesha kwa sababu walikuwa wamekiri ya kwamba Bwana Yesu Kristo ni Mwokozi wao. Walizarauliwa na kulaumiwa; wengine walipotewa nyumba na vitu vyao kwa sababu ya imani yao.

Waamini hawa walikuwa watu wa uhodari. Walisimama pamoja na wahubiri wa Habari Njema na waongozi wao kwa maneno ya Mungu hata wakati waongozi wale walipopigwa fimbo mbele ya watu wote na kufungwa gerezani. Walikubali na furaha kwa mali yao kunyanganywa na adui wao kwa sababu walijua walikuwa na mali mbinguni iliyo njema zaidi na inayodumu (Waebrania 10:34).

Lakini tukisoma barua hii polepole tutaona vilevile ya kwamba hata walisimama na uhodari katika imani wakati walipoamini kwanza, walikuwa wamepoa kidogo rohoni sasa. Wengine walikuwa wameacha kukutana na ndugu zao katika Kristo (Waebrania 10:25). Ni hatari wakati Mukristo, aliyewaka kwa maneno ya Mungu wakati alipoamini

kwanza anapoanza kukosa ndani ya makusanyiko ya kanisa. Ukiulizana naye juu ya neno hili, labda atakujibu, ''Ninaweza kuamini na kuabudu Kristo kwangu nyumbani vilevile.'' Lakini kwa macho ya mwandishi wa barua hii ilikuwa vibaya sana kwa Wakristo kuacha kukutana na Wakristo wenzao. Ilikuwa alama kwake ya kwamba walikuwa wakipoa rohoni na kwa sababu hii aliwaonya tena na tena ndani ya barua hii kusimama imara katika imani. Ni kama alifahamu ya kuwa wengine wa wale waliosimama na uhodari mbele walikuwa karibu kuacha imani yao, ndiyo imani ya kwamba Yesu ni Masiya.

Maneno haya yalikumbusha mwandishi habari za Waisraeli mia za miaka mbele wakati walipotoka katika Misri. Kwa wakati ule walilalamika na uhodari: ''*Bwana ameshinda kwa utukufu; farasi na mupandaji wake ametupa baharini*'' (Kutoka 15:1), lakini nyuma ya muda mudogo watu wale wale walikataa kuendelea mbele na kuingia inchi Mungu aliyoahidi kuwapa! Mwandishi alikumbuka habari hizi za huzuni wakati alipowaza juu ya Wakristo hawa wakianza kurudi nyuma. Ndani ya sura 6 aliwaonya kuendelea hata utimilifu, na alitaja wengine walioanguka na kutenda mambo ya kuogopesha, akisema ya kwamba haiwezekani kuwafanya upya tena hata watubu. Halafu ndani ya sura 10 aliwakumbusha ya kwamba ''*tukifanya zambi na kusudi nyuma ya kupokea kujua kwa kweli, haibaki tena zabihu kwa ajili ya zambi; lakini kutazamia hukumu kwa woga*'' (mash.26-27). Ndiyo, mwandishi wa barua kwa Waebrania alisumbuka sana rohoni juu ya maneno mengine aliyoyaona katikati ya waamini hawa.

**Historia ya wasomaji**

Tunataka sana kupata faida kwa sisi wenyewe ndani ya mafundisho mwandishi aliyoleta kwa watu hawa, hivi ni sharti kabisa kwa sisi kufahamu hali yao. Kumbuka ya kwamba walipata nguvu ndani ya dini ya Wayuda. Walijuana na mapambo ya hekalu katika Yerusalema, kuimba kwa Walawi na makuhani wenye mavazi mazuri. Walijuana na utaratibu wa kutoa zabihu mbalimbali na maneno yote iliyowapasa kufanya kwa kuabudu Mungu na utaratibu. Walijua habari za Wayuda wa zamani, wale waliojulikana, kama Musa, aliyeabudu ndani ya hema iliyofanana na hekalu lao, na Daudi na Solomono aliyejenga hekalu la kwanza, hekalu la mapambo mengi. Walijua ya kwamba alikuwa Mungu aliyesimamisha utaratibu huu wa kuabudu. Maandiko Matakatifu yaliwaagiza kuabudu hivi na walipenda maneno haya sana, wakakuwa tayari hata kupata mateso kwa dini yao.

*Halafu Yesu alitokea.* Labda wengine wa wasomaji wa barua hii walisikia mafundisho ya Bwana Yesu na masikio yao wenyewe na kusaidiwa kwa njia ya maajabu aliyoyafanya. Yesu alisema yeye ni Kristo, Masiya wa Israeli, na Mwana wa Mungu. Taifa la Wayuda

walikataa kuamini neno hili. Halafu mambo ya ajabu yalitokea siku ya tatu nyuma ya kufa kwake, na siku ya Pentekote muji muzima ulishituka kusikia ya kwamba Yesu huyu waliyemusulibisha alikuwa amefufuka na kurudi mbinguni. Maneno haya yalihakikisha ya kwamba alikuwa kweli Masiya wa Israeli. Mungu kwa uwezo wake aligeuza neno taifa la Israeli walilolifanya, akafufua Yesu toka wafu na kumuketisha kwa mukono wake wa kuume!

Kwa kuhakikisha maneno haya Roho Mutakatifu alikuwa amefika na maajabu ya kushangaza yalifanywa kwa jina la Yesu. Ilishinda hata watu wa Yerusalema kuyabisha. Basi watu wengi walitubu juu ya kuua Mwana wa Mungu. Walikuwa wamemwua kwa ujinga. Katika muji ule ule pahali Bwana wao aliposulibishwa watu walibatizwa kwa jina la Yesu na kupokea zawadi ya Roho Mutakatifu (Matendo 2:38).

**Taifa la Wayuda lilitengwa**

Hivi tunafikili wengine wa wasomaji wa barua hii, wale waliokuwa na miaka mingi kidogo, walikuwa kwa Yerusalema wakati maneno haya makubwa yalipofanyikana. Lakini zaidi ya watu walioishi kwa wakati ule walikuwa wamekufa na wengi wa wasomaji wa barua hii walikuwa vijana waliosikia Habari Njema kwa vinywa vya wazee waliosikia Bwana Yesu na masikio yao wenyewe (Waebrania 2:3). Mungu alikuwa amehakikisha kweli ya habari hizi kwa njia ya maajabu na alama nyingi. Kwa wakati ule kulikuwa na Wayuda wengi, hata makuhani, waliosema ya kwamba Yesu alikuwa Masiya wao, lakini hawakuachana na dini ya Wayuda mara moja (Matendo 6:7).

Hivi taifa la Wayuda lilitengwa. Wengi wa viongozi wao walikaa kuamini ya kwamba Yesu hakuwa Masiya na ya kuwa walifanya vizuri wakati walipoagiza asulibishwe. Watu hawa walijaribu kuhakikisha ya kwamba hakufufuka toka wafu. Lakini wengine waliamini ya kwamba Yesu alikuwa kweli Masiya, Mwana wa Mungu, na ya kuwa hakustahili kusulibishwa. Hesabu ya watu wale ilikaa kuongezeka nao waliamini ya kwamba alifufuka kweli toka wafu.

Wayuda hawa wote, wale waliokana ya kwamba Yesu alikuwa Masiya wao, na wale waliomwamini, walikaa kwenda kwa hekalu pamoja na kuomba pamoja. Walikutana ndani ya masunagogi mbalimbali kwa sababu Wayuda walikuwa na masunagogi mbalimbali yasiyopatana yote kwa maneno ya mafundisho yao. Lakini wao wote waliabudu Mungu mumoja ndani ya hekalu moja - ona Matendo 3. Hata mitume kama Petro na Yakobo na Paulo walipenda hekalu hili sana.

Hivi Wakristo wale wa kwanza walikaa kufikia hekalu na kushuhudia Kristo pale. Iliwapasa kuelezea watu ya kwamba Yesu alikuwa Masiya hata kama aliteswa hivi, na walitafuta ndani ya Agano la Kale

mashairi yaliyotabiri ya kuwa Masiya atateswa. Walionyesha ya kwamba mateso ya Yesu hayakuonyesha ya kwamba hakuwa Masiya. Walisema mateso haya yalihakikisha ya kwamba alikuwa Masiya kweli kwani yalitimiza unabii ndani ya Agano la Kale uliosema Masiya atateswa na kufa na kufufuka tena na kutukuzwa kwa mukono wa kuume wa Mungu (Matendo 3:17-20; 5:30-31).Basi watu wengi waliamini kwa sababu ya mahubiri yao. Na pamoja na habari hizi walitangaza ya kwamba Kristo atakuja tena. *"Kwa kuwa bado kidogo sana, yeye anayekuja atakuja, wala hatakawia"* (Waebrania 10:37).

Walipata mateso makali kwa sababu ya maneno haya. Walibeba mateso haya na furaha kwanza lakini sasa miaka ilikuwa imepita na Kristo *hakuja* tena. Hata mitume waliuliza Bwana mbele ya kurudi kwake mbinguni: *"Bwana, utarudishia Waisraeli ufalme wao tena wakati huu?"* (Matendo 1:6) Hawakufikili watu wa Mataifa kwa wakati ule. Bwana alikuwa amefufuka, alikuwa Masiya, na walifikili atarudi nyuma kidogo na kuwarudishia ufalme wa Israeli na kuwafungua toka utawala wa Waroma.

Hata Petro alihitaji ono toka Bwana kufungua mawazo yake. Kufika wakati ule hakufikili hata kidogo juu ya kuhubiri Habari Njema kwa Mataifa. Wayuda wa wakati ule hawakufahamu unabii wa Agano la Kale kama sisi kwa wakati wa sasa tunavyoweza kuufahamu. Wengi wao walingojea Bwana Yesu kurudia Israeli kwa wakati ule ule na kusimamisha ufalme wake pale katika inchi ya Palestina. Neno hili lingaliweza kuhakikisha kwa Wayuda wenzao ya kwamba alikuwa kweli Kristo, Masiya wao. Lakini miezi na miaka ilipita naye hakufika. Wakristo wazee walianza kufa na kwa kipimo hesabu ya Wakristo ilipoongezeka kwa kipimo hiki mateso yao yaliongezeka vilevile. Lakini Kristo hakufika. Na sasa Petro na wengine walikuwa wamehubiri Habari Njema kwa Mataifa! Sasa kulikuwa na waamini ndani ya miji mingi ya Wayunani. Bila shaka Wayuda walifazaika sana juu ya maneno haya! Habari Njema ile juu ya Yesu ilikuwa nini? Ona kwanza mutu huyu Paulo: aliokolewa kwa gafula na sasa alipelekea Mataifa maneno yale yaliyokuwa ya damani sana kwa Wayuda! Watu wengine walisema ya kwamba alileta Muyunani hata ndani ya hekalu!

Maneno haya yote yalifazaisha watu sana kwani ilikuwa desturi yao kujitenga na watu wa mataifa mengine, kama Mungu alivyowaagiza zamani. Mungu alitaka kufanya nini? Labda wengine katikati yao walikumbuka ya kwamba Bwana Yesu alisema: *"Kwendeni katika dunia pia, mukahubiri Habari Njema"* (Marko 16:15), lakini kwa siku nyingi hawakufahamu maana ya masemo haya.

Mafazaiko na taabu yao ziliongezeka kwa sababu viongozi wa Wayuda kwa maneno ya dini walizidi kushindana na Wakristo hawa wa sasa na kuwashitaki kwa watawala wa inchi.

Basi siku na miezi ilipita. Hata kama Wakristo wa kwanza walikuwa wenye uhodari, maneno haya yote yalitaka kushinda wengine katikati yao. Tumaini lao lilitaka kwisha na walianza kuwa na shaka juu ya kurudi kwa Bwana.

### Yesu ... ao hekalu?

Wakristo walikuwa na nguvu wakati maneno yao yalipotembea vizuri na watu wengine walipokuwa wakiokolewa. Lakini wakati miaka ilipoendelea na mateso yao yasipopunguka walianza kulegea na kuwa na shaka. Labda walikuwa wameamini maneno yasiyokuwa kweli? Walifikili Wayuda wenzao wataamini Yesu vilevile. Walikuwa wametazamia kurudi kwa Kristo wakizani Wayuda wote watamupokea na furaha ndani ya hekalu lao, na kukiri ya kwamba yeye ni Masiya wao. Lakini ilionekana wazi sasa ya kwamba taifa lao hawakutaka kuamini hata kidogo, na hata mitume walisema watakwenda kuhubiri Habari Njema kwa Mataifa kwa sababu watu wa taifa lao wenyewe walikataa kuamini. Wakristo walianza kufahamu polepole ya kwamba haiwezekani kuwa Mukristo na kufungana na dini ya Wayuda vilevile. Sharti Wakristo wajitenge nayo.

Watu waliopata nguvu katika dini ya Wayuda walipenda dini hii sana na kwa sababu hii ilikuwa nguvu kwao kuiacha. Wangalifurahi kusema ya kwamba Kristo ni Masiya wao kama wangaliweza kubaki na hekalu lao vilevile. Lakini walifahamu ya kwamba iliwapasa kuchagua — ao Kristo ao hekalu; ao zabihu ya Yesu ao zabihu za nyama; ao ukuhani wa Kristo ao ule wa Haruni; ao kukubaliwa na Wayuda wenzao katika inchi yao wenyewe ao "kwenda inje ya kambi" (Waebrania 13:13) kwa Yesu aliyekataliwa na taifa lao. Ndiyo, ilikuwa lazima kwao kuchagua...

Watu hawa walifazaika sana wakati walipowaza juu ya maneno haya. Wengine wao walikuwa wakisitasita na wengine walikuwa wameacha kukutana pamoja na waamini wengine. Si nguvu kwa sisi kufahamu mawazo yao. Na tunaweza kufahamu vilevile mawazo ya yule aliyewaandikia barua hii. Aliwapenda sana na alifahamu hatari watakayoipata rohoni kama wasipochagua njia nzuri.

### Warudi nyuma?

Nini itawapata kama wakirudi nyuma? Tuone kama Mungu alisema nini ndani ya 10:29, *"Haikupasa azabu kubwa zaidi kwa mutu yule aliyekanyaga Mwana wa Mungu, na kuhesabu damu ya agano aliyotakaswa nayo kuwa kitu kichafu, na kutukana Roho ya neema?"* Maneno haya ni maneno makubwa. Tafazali usiyaone bule. Watu

hawa wakichagua kurudi nyuma na kukwamana na dini ya Wayuda, wanafanya maneno matatu:

Kwanza, wanakanyaga Mwana wa Mungu. Maana yake si kukwaa tu, kwa bahati mbaya, lakini kukanyaga na kusudi. Wanakanyaga nani? Angalia tena ndani ya Biblia yako. Si Yesu lakini ni Mwana wa Mungu. Basi Yesu alikuwa Mwana wa Mungu ao sivyo? Taifa la Israeli walisema, "Sivyo, hakuwa Mwana wa Mungu." Lakini Waebrania hawa walikuwa wameshuhudia: "Ndiyo, yeye ni Mwana wa Mungu." Hata hivi sasa walijaribiwa kurudi tena kwa dini ya Wayuda. Lakini hawakuweza kufanya hivi bila kusema ya kwamba Yesu *si* Mwana wa Mungu. Walikuwa wamesema hivi mbele kwa ujinga pamoja na Wayuda wote wengine lakini sasa walikuwa wameona uwezo wa Roho Mutakatifu ukitumika ndani ya maisha na zamiri zao. Wakitaka kurudi nyuma sasa iliwapasa kukana ya kwamba Yesu ni Mungu.

Halafu nyuma ya kukana ya kwamba Yesu ni Mungu, neno la pili ni kuhesabu damu ya agano waliyotakaswa nayo kuwa kitu kichafu. Ndiyo, kama Yesu si Mungu, damu yake haina faida kupita damu ya mutu ye yote mwingine. Ona ya kwamba inaitwa hapa *damu ya agano.* Kama damu ya agano ni damu ya faida, agano hili lina maana na faida, lakini kama agano lilitiwa muhuri na damu ya bule, agano hili ni bule vilevile. Hivi kwa mutu kurudi kwa dini ya Wayuda ilimupasa kukana ya kwamba Yesu ni Mungu na kusema damu yake ilikuwa ya bule na hivi agano jipya halina faida.

Neno la tatu lilikuwa kutukana Roho ya neema. Ndiyo, ni Roho Mutakatifu, lakini ona kama anaitwa na jina gani hapa. Haitwi Roho ya kweli, ao Roho ya utakatifu lakini Roho ya *neema.* Wayuda walikuwa wamesulibisha Yesu kwa ujinga, lakini ona kwanza neema kubwa ya Mungu. Aliwapa njia kutubu wakati Bwana Yesu alipokwisha kufufuka na kurudi mbinguni. Kwa pahali pa kuwaharibu mara moja alisema nao, "Mumeua Mwana wangu lakini mulifanya hivi kwa ujinga. Mbele mulijaribu kujiokoa kwa njia ya kushika sheria yangu lakini sasa mimi ni tayari kuwaokoa ninyi kwa bule, kwa neema, bila matendo yenu mema." Ni habari za rehema na neema kweli. Walipewa njia kutubu na zaidi ya ile waliweza kupokea wokovu kama zawadi kwa sababu ya neema ya Mungu.

Mwamini ye yote akirudi kwa dini ya Wayuda sasa ni kama alisema na Mungu: "Mungu, sitaki neema yako. Tupokee rehema na usamehe kwa sababu ya kusulibishwa kwa Yesu? Hatutaki usamehe! Tungalifanya hivi tena; hatuamini ya kwamba yeye ni Mwana wako. Tupokee wokovu kwa neema? Wapi! Tunataka kufanya kazi njema na kushika sheria kusudi tuweze kufika mbinguni."

**Waamini wa kweli?**

Unasema: "Mwamini wa kweli anaweza kusema maneno mabaya namna hii?"

"Lakini nani alisema ya kwamba walikuwa waamini wa kweli?"

"Lakini," unajibu, "ulisema hivi tena na tena."

"Sikusema hivi hata kidogo."

"Lakini ulisema ya kwamba walisema wana imani."

"Ndiyo, barua hii inasema ya kwamba walisema wana imani. Lakini maneno tunayosema na midomo yetu hayapatani kila mara na mawazo ya mioyo yetu."

Unasema: "Lakini shairi hili linasema juu ya damu aliyotakaswa nayo..."

"Neno hili, ya kwamba alitakaswa, linahakikisha ya kwamba alikuwa mwamini wa kweli?"

Unajibu: "Ndiyo."

Ninajibu: "Sivyo. Ndani ya 1 Wakorinto 7:14 tunasoma ya kwamba mume asiyeamini anatakaswa na muke wake Mukristo, lakini hata hivi yeye ni kwanza musiyeamini."

Mutu hawezi kuhesabiwa haki bila imani, lakini anaweza kutakaswa bila kuwa mwamini wa kweli. Waebrania hawa walikuwa wametakaswa, lakini walikuwa waamini wa kweli? Mwandishi alionyesha mawazo yake ndani ya mashairi 9-12 ya sura 6. Alionyesha mwisho wa kuogopesha wa wale wanaorudi kwa dini ya Wayuda (sh.8). Alisema kama kwa watu wasiookolewa bado. Lakini kabisa kabisa ndani ya roho yake alisadiki maneno mazuri zaidi juu ya wasomaji wa barua yake. Aliona maneno ndani ya maisha yao yaliyokuwa matunda ya wokovu. Maneno haya yalionyesha ya kwamba waliokolewa kweli. Hata hivi alitoa maonyo haya ya kuogopesha ili hata mutu mumoja asianguke kwa sababu ya kukosa imani. Kwa sababu mutu akikosa imani yeye ni musiyeamini.

Hivi wakati tunaposoma barua hii tunaona tena na tena na tena ya kwamba kuwa na imani ni neno kubwa sana. *"Mwenye haki ataishi kwa imani"* (10:38).

Unaamini kweli kweli ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu? *"Kila mutu anayeamini ya kuwa Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu"* (1 Yoane 5:1). Halafu barua hii ikupatishe nguvu rohoni hata kama ukianguka mara nyingine, ao hata kukana Bwana wako unayemupenda, kama Petro alivyofanya. Ukiwa mwamini wa kweli una Kuhani mukubwa aliye hai na anayeokoa kabisa wote wanaokuja kwake Mungu kwa njia yake (7:25). Hataacha hata mwamini mumoja wa kweli kupotea. Hata kama ukianguka mara ngapi, *amekamilisha hata milele wenye kutakaswa* (10:14), kama wao ni waamini wa kweli.

Hivi haifai tuwe na shaka rohoni. Kuna mashairi mengi ndani ya barua hii yanayoonyesha ya kwamba kila mwamini wa kweli atafika mbinguni. Lakini vizuri ujiulize leo, "Nimeamini kweli kweli? Ao nilikiri tu na midomo ya kwamba niliamini?" Kama wewe ni mwamini wa kweli, Kristo atakuokoa kabisa, na hata watu wengine wataweza kuona ndani ya maisha yako matunda ya wokovu yatakayohakikisha ya kwamba uliamini kweli.

# *Kristo ni Mungu*
# *Sura 1*

Ndani ya sura iliyopita tulijaribu kuonyesha kama mwandishi aliandika barua hii kwa watu wa namna gani. Kufahamu hali yao kutatusaidia kupata faida kwa roho na maisha yetu wakati tunaposoma barua hii.

Tumeona ya kwamba ilipasa Wakristo wale kuchagua. Kuchagua nini? Iliwapasa kuchagua ao kusimama imara ndani ya imani yao ya kwamba Yesu ni Masiya na Mungu, ao kurudi nyuma, kukana ya kuwa Yesu ni Mungu, kukataa damu ya agano lake na kuzarau neema ya Mungu.

Maneno haya yalikuwa maneno makubwa. Kama wakiendelea mbele kwa imani, watapata mateso, kupotewa vitu vyao na labda hata uzima wao. Lakini zaidi ya maneno yale, kama wakienda mbele, itawapasa kuachana kabisa na dini ile iliyowafunga na kuwatawala sana kufika wakati ule. Itawapasa kuachana na hekalu na kutoka inje ya kambi ya Wayuda, itawapasa kuachana na maneno yote ya dunia na dini zote nyingine, na kufungana na Bwana Yesu tu.

Wengi wa watu wale hawakujifunza maneno mengi ya dini na walipata matata kwa njia nyingine vilevile. Walimu wao wa mbele kwa maneno ya dini walifika karibu nao na kuwahamakia juu ya kuachana na dini ya baba zao, dini Mungu mwenyewe aliyoisimamisha ndani ya Agano la Kale. Na bila shaka walibishana na waamini hawa wa sasa juu ya uungu wa Kristo.

Wakristo walikuwa wamefahamu ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, ya kwamba yeye ni Mungu. Bila shaka walimu wao waliwafikia tena na tena na kutaja mashairi toka Agano la Kale kama wana-

vyofanya hata leo. Walisema nao: "Mwone ya kwamba Agano la Kale linasema, *'Sikia, Ee Israeli: Bwana Mungu wetu ni Bwana mumoja'* (Torati 6:4). Sisi taifa la Wayuda tumesimamia kweli hii kubwa kwa mia za miaka."

Mbele ya kuhamishwa toka inchi yao miaka mingi mbele Waisraeli waliabudu sanamu mara nyingi na ilipasa Mungu kuwaazibu. Ndani ya mia za miaka iliyopita tangu waliporudia inchi yao toka Babeli taifa la Israeli limesimama na nguvu kwa kweli hii ya kwamba Mungu ni mumoja. *"Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho, na zaidi yangu hakuna Mungu"* (Isaya 44:6).

Lakini ilipasa Waebrania hawa waliopokea Yesu kuamini ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, na ya kwamba Yesu huyu aliyeonekana hapa duniani kama mutu alikuwa Mungu. Wayuda wengine walifikili ni matukano kusema Yesu ni Mungu. Ndiyo, walikuwa wamesulibisha Yesu kwa sababu alijionyesha kuwa Mungu. Hawakumusulibisha kwa sababu ya maajabu aliyoyafanya, ao kwa sababu ya maneno aliyoyafundisha, lakini kwa sababu alijifanya sawa na Mungu (Yoane 5:18).

Basi waamini hawa wafanye nini? Walikuwa wameitika ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na waliamini ahadi yake ya kuwa atakuja tena. Walifikili watu wote wa taifa lao wataamini kwa wakati ule. Lakini miaka ilipita naye hakufika. Hatushangai kuona ya kwamba walianza kufazaika na kuona shaka rohoni mwao.

*Yesu, Mwana wa Mungu*

Mwandishi wa barua hii (hatujui kama alikuwa nani) alisumbuka juu ya hali ya roho ya waamini hawa. Wengine hawakufikia makusanyiko ya kanisa tena. Walikuwa katika hatari kabisa lakini hakuanza mara moja kuwahamakia kwa sababu aliwahurumia. Neno lililowasumbusha lilikuwa neno kubwa sana, ndilo hili: Yesu ni Mwana wa Mungu kweli ao sivyo? Mutume Yoane aliwaambia waamini wa Mataifa, *"Hii ni kushinda kunakoshinda dunia, imani yetu ... ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu"* (1 Yoane 5:4-5).

Tukumbuke neno hili. Tukitaka kuwa watu wenye kushinda dunia sharti tuamini ya kwamba Yesu ni kweli Mwana wa Mungu. Ni vizuri kuamini ya kuwa zambi zetu zimesamehewa na tuna uzima wa milele, lakini neno kubwa zaidi ni kuamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

Neno hili lilikuwa neno kubwa kwa Wayuda. Ao Yesu ni Mwana wa Mungu na tunainama kwa miguu yake na kumwabudu kama Mungu, ao yeye si Mwana wa Mungu lakini mutukanaji na mudanganyi. Kulikuwa na neno moja tu lililoweza kusaidia waamini hawa kusimama imara, ndilo imani ya nguvu ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

Hivi mwandishi alianza mara moja kufundisha juu ya uungu wa Bwana Yesu. Alitaka kufariji wasomaji wake waliolazimishwa kuachana na dini ya baba zao na hekalu na maneno yote yaliyokuwa ya damani sana kwao. Ndani ya barua yake alionyesha tena na tena ya kuwa Bwana Yesu, kiongozi mukubwa wa wokovu wao (2:10), anapita mbali kabisa kwa uzuri maneno yote iliyowapasa kuachana nayo. Yeye ni muzuri kupita malaika, na Musa, na Yosua, na Haruni; yeye ni muzuri kupita hema takatifu na zabihu, na agano lake ni zuri kupita agano la kwanza. Ni kama mwandishi alisema na waamini hawa tena na tena, "Si hasara kwenu kufuata Bwana Yesu. Maneno munayopata ni mazuri kupita maneno munayoyaacha kwa sababu Yesu anapita yote."

*Muzuri kuliko malaika*

Yesu ni muzuri kuliko malaika kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu. Wayuda waliheshimu malaika sana kwa sababu Mungu alikuwa amewapa sheria kwa njia ya malaika (Wagalatia 3:19). Mungu alikuwa amesema nao kwa njia ya malaika na maneno aliyowaambia kwa njia yao yalikuwa ya damani sana kwao. Sasa Wayuda walisema maneno kama haya: "Munataka sisi kuacha maneno Mungu aliyosema nasi kwa njia ya malaika na kupokea mawazo yenu, ninyi wafuata wa mutu yule wa Nazareti?" Wafarisayo walikuwa wamesema maneno namna hii juu ya Bwana Yesu vilevile. Ona Yoane 9:29.

## *SOMA 1:1-3*

Mwandishi alianza barua hii na kusema ya kwamba kweli Mungu alisema zamani kwa njia ya Musa na manabii (sh.1). (Leo watu wengi wanaona Agano la Kale bule, lakini shairi 1 linaonyesha wazi ya kwamba Agano la Kale vilevile ni sauti ya Mungu kwetu.)

Lakini Mungu aliyesema na watu zamani amesema tena katika siku hizi za mwisho, na maneno aliyosema zamani yanapatana na maneno aliyoyasema sasa. Mungu huyu amesema tena na tena, *kwa nyakati mbalimbali,* kwa Adamu katika shamba la Edeni, kwa Abrahamu, Musa, Daudi, na watu wengi wengine. Alisema na watu *kwa njia mbalimbali.* Mara nyingine alisema kwa njia ya ndoto. Mara nyingine alionekana kwa watu kwa sura ya mutu kama alivyofanya kwa Abrahamu (Mwanzo 18:1). Mara nyingine alisema kwa njia ya manabii na mara nyingine kwa njia ya vitu vya hema takatifu na utumishi wake.

Alisema nusu nusu kwa njia mbalimbali na kwa nyakati mbalimbali. Neno hili lingalipasa kufahamisha Wayuda ya kwamba maneno haya yalikuwa matayarisho tu kwa maneno mazuri zaidi yasiyotokea bado. *"Mungu, aliyesema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, katika siku hizi za mwisho amesema*

*nasi katika Mwana.*" Tangu mwanzo alisema nusu nusu, lakini sasa, katika Mwana wake, amesema yote pia.

### *Mungu mumoja*

Mbele Mungu alisema kwa njia ya watu mbalimbali, watu zaifu na wenye zambi, lakini kwa siku hizi za mwisho alisema katika mumoja aliye Mungu, ndiye Mwana wa Mungu. Unafahamu maana ya neno hili? Sisi Wakristo hatuamini miungu mitatu. Agano Jipya linatangaza ya kwamba kuna Mungu mumoja tu. Lakini kuna watatu ndani ya Mungu huyu mumoja, Baba, Mwana, na Roho Mutakatifu. Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu, na Roho Mutakatifu ni Mungu, lakini si miungu mbalimbali. Kuna Mungu mumoja tu.

Unauliza: "Neno hili linawezekana namna gani?"

Hili ndilo neno Mungu alilotuambia. Hatuwezi kufahamu Mungu na nia zetu za kimutu lakini tuamini maneno iliyomupendeza kutujulisha. Bwana wetu Yesu Kristo ni Mungu. Wakati unaposikia Yesu unasikia Mungu!

Ni kama mwandishi alisema na wasomaji wa barua hii: "Siwaombi ninyi kuacha maneno Mungu aliyoyasema kwa kufuata maneno yaliyosemwa na nabii. Ninawaomba ninyi, muliosikia mbele maneno ya Mungu kwa njia ya manabii, kuweka roho sasa juu ya maneno ya Mungu yaliyosemwa na Mungu mwenyewe."

### *Muriti*

Halafu mwandishi aliendelea kutuonyeshea utukufu wa Mwana wa Mungu. Tuwaze juu ya maneno haya na kumwabudu yule katika yeye Mungu alisema kwa siku za mwisho. *"Amesema nasi katika Mwana, aliyemuweka kuwa muriti wa vitu vyote, kwa yeye aliyefanya ulimwengu"* (sh.2). Elfu za miaka mbele Mungu aliweka misingi ya dunia hii na nyota za asubui waliimba kwa furaha na wana wa Mungu walipiga mikono (Yobu 38:4-7). Basi ulimwengu uliumbwa kwa kusudi gani? Uliumbwa kwa Mwana wa Mungu. Kwa nini dunia yetu hii iliumbwa? Iliumbwa kwa yeye atakayekuwa Muriti wa vitu vyote. Katika shairi hili na katika Wakolosayi 1:16 tunaona ya kwamba ndiye aliyeumba vitu vyote na watu vilevile kusudi waweze kutafuta na kujua Mungu.

### *Utukufu wa Mungu*

Tumewaza juu ya maneno Mwana wa Mungu aliyoyafanya na atakayoyafanya. Sasa tuwaze kama yeye ni nani. *"Akiwa kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe, akichukua vitu vyote kwa Neno la uwezo wake..."* (sh.3). Haya ndiyo maneno ya

kweli juu ya Kristo aliye tangu zamani, na hata sasa, na maneno aliyofanya tangu zamani na kuendelea kuyafanya leo. Yeye ni kungaa kwa utukufu wa Mungu. Hata mutu mumoja hakuona Mungu Baba wakati wo wote. Hata Musa hakumwona. Wakati Musa aliposimama pale katika pango la mwamba na utukufu wa Mungu ulipopita, Musa Hakuna mutu aliyeona Mungu wakati wo wote (Yoane 1:18). Musa aliona nani basi? Alimwona yeye aliyejulikana hapa duniani kama Yesu wa Nazareti, lakini aliyekuwa tangu zamani kungaa kwa utukufu wa Mungu. Amengaa mbele ya watu na kuwaonyesha kama Mungu ni ngu. Amengaa mbele ya watu na kuwaonyesha kama Mungu ni namnamna gani. Alionyesha utukufu wake kwa njia ya vitu alivyoviumba.

Isaya aliona Bwana wa majeshi juu, mwenye kunyanyuliwa, na pindo za nguo zake zilijaza hekalu (Isaya 6:1-12). Lakini mutume Yoane, akiongozwa na Roho Mutakatifu, alitujulisha ya kwamba siku ile Isaya aliona Bwana Yesu. Ni yeye anayengaa kwa utukufu wa Mungu. Yeye si kama kioo kinachorudisha nuru, lakini yeye mwenyewe *ni* kungaa kwa utukufu wa Mungu. Alikuwa hivi zamani, yeye ni hivi sasa na atakuwa hivi kwa milele. Hata wakati alipokuwa hapa duniani aliweza kusema: *''Aliyeniona mimi, ameona Baba; namna gani unasema: Utuonyeshe Baba?''* (Yoane 14:9). Hatuna miungu mitatu ao miwili; Mungu Mwana alisema: *''Yeye aliyeniona mimi, ameona Baba.''*

*Mwenye kuchukua vitu vyote*

Kuna neno lingine Kristo analolifanya tangu zamani na atakalolifanya hata milele — anachukua vitu vyote kwa neno la uwezo wake (sh.3). Anategemeza ulimwengu huu aliouumba.

Unaogopa watu wataharibu dunia hii na vitu vyao vya vita? Usiogope — Bwana wetu anategemeza vitu vyote kwa neno la uwezo wake. Tazama mbingu — jua na mwezi na milioni za nyota — Bwana wetu anazichukua zote!

Zaidi ya ile tunasoma, *''akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu.''* Bwana wetu atakuwa Muriti wa vitu vyote, aliviumba vyote na anavichukua vyote, na wakati zambi ilipoviharibu alifika yeye mwenyewe kuvitengeneza! Alikuja na kufanya kazi iliyohitajiwa kusudi mwishoni ulimwengu huu usafishwe kabisa toka maneno yote yanayouchafua sasa. Nyuma yake aliketi kwa mukono wa kuume wa Mungu, ndipo pahali pa heshima na utukufu zaidi. Neno hili linaonyesha wazi ya kwamba yeye na Baba ni sawasawa. *''Mimi na Baba yangu ni mumoja''* (Yoane 10:30). Baba hakumuketisha na Mwana hakuomba ruhusa toka Baba mbele ya kuketi; aliketi pale na ruhusa yake mwenyewe kwani yeye ni Mungu, sawasawa na Baba.

*SOMA 1:4-9*

Labda Waebrania waliopokea barua hii walisema: "Ndiyo, ni kweli. Tuliamini maneno haya vilevile. Lakini hata ninyi viongozi mukisema maneno haya mazuri sana juu ya Yesu wa Nazareti, munaweza kuhakikisha ya kwamba ni masemo ya kweli?"

Sisi tunaopenda Bwana tunaamini maneno haya kwa sababu tunakubali ya kwamba ni Neno la Mungu. Lakini tuwaze kwanza juu ya Waebrania hawa. Wayuda wasiookolewa bado walifikili ni matukano mabaya sana. Na hata Waebrania waliokiri ya kwamba wao ni Wakristo walihitaji ushuhuda ya kwamba ni maneno ya kweli. Wala haikutosha kwa mwalimu kutaja mashairi toka sehemu ile ya Agano Jipya iliyokwisha kuandikwa. Agano Jipya iliandikwa na Wakristo walioamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na maandiko yao hayakuweza kuaminisha Wayuda.

*Agano la Kale*

Kwa sababu hii mwandishi wa barua hii hakutaja masemo ao maandiko ya mitume. Alijua ya kwamba ilikuwa lazima kwake kutumika na Agano la Kale kwa kuaminisha Wayuda ya kuwa Yesu ni Mungu. Kwanza ilimupasa kuhakikisha ya kwamba ilipasa Masiya kuwa Mungu. Kufanya hivi alitaja mashairi mawili toka Agano la Kale (sh.5). La kwanza ni Zaburi 2:7, pahali Mungu aliposema: *"Wewe ni mwana wangu; leo nimekuzaa."* La pili ni 2 Samweli 7:14: *"Nitakuwa baba wake, naye atakuwa mwana wangu."* Mashairi haya mawili ni unabii juu ya Mufalme wa Israeli, ndiye Masiya, aliye Mungu.

Lakini Wayuda waliweza kujibu: "Katika Agano la Kale malaika waliitwa wana wa Mungu, hivi maneno haya 'Atakuwa mwana wangu' si sharti kusema mwana huyu ni Mungu." Ni kweli ya kwamba malaika wanaitwa wana wa Mungu ndani ya Agano la Kale, lakini Mungu alisema na malaika gani wakati wo wote, *"Uketi kwa mukono wangu wa kuume"* (sh.13)? Vilevile Mungu hakuita hata mumoja wao "Mwana *wangu.*" Sivyo, Mwana wa Mungu ni juu kupita malaika kwa sababu *"ameriti jina lenye utukufu kuliko lao"* (sh.4). Malaika ni viumbe tu; Mwana ni Muriti kwa sababu ana uzima wa Mungu naye NI Mungu na hakuumbwa. Ndiyo, hakuna kiumbe aliye Mwana wa Mungu kama yeye.

*Kuja kwa pili kwa Kristo*

Wakati Bwana Yesu alipokuja mara ya kwanza watu walimuzarau na hawakutambua ya kwamba yeye ni Mungu. Haitakuwa hivi wakati atakapokuja tena. Kwa Kiyunani shairi 6 linasema hivi: *"Na wakati anapoleta TENA muzaliwa wa kwanza katika dunia, anasema: Na malaika zote za Mungu wamwabudu."* Wamwabudu? Wayuda wali-

kataa na nguvu kuabudu mutu ye yote, hata malaika. Ona Ufunuo 19:10. Basi Agano la Kale linasema juu ya nani wakati lilipoagiza, *"Malaika zote za Mungu wamwabudu"* (Zaburi 97:7)? Ni Mungu Mwana anayestahili kupokea kuabudu kama Mungu Baba.

Halafu Mungu alisema na Mwana: *"Kiti chako cha ufalme, Mungu, ni cha milele na milele, na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki"* (sh.8). Wafalme wengi walikuwa wametawala Waisraeli lakini wao wote walianguka kwa njia nyingine na hawakutawala kwa haki kabisa. Lakini Agano la Kale (Zaburi 45:6-7) lilisema ya kwamba Masiya atakuwa mukamilifu. Ndiyo, hakuwa mutu tu, alikuwa Mungu mwenyewe. Ametiwa mafuta *kupita wenzake* (sh.9).

### *SOMA 1:10-12*

Halafu mwandishi anawaza juu ya dunia hii Mungu aliyoiumba. Wakati tunapotazama elfu za nyota mbinguni, milima mirefu na bahari, tunafahamu ya kwamba tuko viumbe zaifu tu. Milima ile imesimama elfu za miaka, lakini maisha yetu ni mafupi tu, kama majani. Tuko wadogo sana.

Ndani ya mashairi 10-12 Mungu anasema na Masiya akitumia mashairi 25-28 ya Zaburi 102. Soma mashairi haya tena polepole na utashangaa juu ya ukubwa na utukufu wa Masiya - na kumbuka ya kwamba Masiya huyu ni Yesu!

### *MALAIKA, 1:13-14*

Haiwezekani kusawanisha malaika na Kristo. Ndiyo, tumeona ya kwamba malaika wameitwa wana wa Mungu vilevile mara nyingine, lakini *"kwa malaika gani amekwisha kusema hata mara moja: Uketi kwa mukono wangu wa kuume hata nitakapoweka adui zako chini ya miguu yako?"* (sh.13).

Malaika wanapigania Mungu. Kwa wakati wa kuja Mikaeli na malaika zake watapigana na joka, ndiye Shetani, na Mikaeli atashinda (Ufunuo 12:7-9). Lakini wakati Mikaeli atakapotokea tena mbele ya Mungu atakuja na upole na unyenyekevu. Na Mungu hatasema naye: "Kuja uketi kwa mukono wangu wa kuume hata nitakapoweka adui zako chini ya miguu yako." Sivyo, Mungu hajasema hivi kwa malaika ye yote. Amefanya hivi kwa Mumoja tu, ndiye Mwana wake aliye sawasawa naye kwani yeye ni Mungu vilevile.

Hivi hakuna njia kusawanisha Kristo na malaika. Malaika ni watumishi tu wanaotumikia wale watakaoriti wokovu.

Basi tumefikia mwisho wa sura ya kwanza ya barua hii. Imejaza roho zetu na kuabudu kwa Bwana wetu, na tunapata hamu vilevile kujitoa muzima kwake.

Tuwaze juu ya maneno mawili mengine mbele ya kuendelea kwa Sura 2.

Kwanza, mafundisho haya ya kwamba Masiya ni Mungu, Mungu kabisa asiyeumbwa, hayakutoka katika nia na mawazo ya wavuvi katika Galilaya. Ni habari Mungu alizofunua hata ndani ya Agano la Kale. Hakutuma Mwokozi toka mbinguni gafula bila kujulisha watu mbele. Wakati Mungu alipokuwa akitayarisha mataifa kwa kuja kwa Mukombozi wao alisema tena na tena ya kwamba Mukombozi huyu atakayekuja atakuwa Mungu. *"Hatukufuata hadizi zilizotengenezwa kwa hila"* (2 Petro 1:16).

Neno la pili ndilo hili: Nyuma ya kuwaza sana juu ya utukufu wa Bwana wetu, tuwaze juu yetu wenyewe tunaoabudu kwa kiti cha miguu yake. Tunakumbuka ya kwamba anapita malaika mbali kwa ukubwa; wao ni watumishi wake tu. Halafu tunamusikia akituambia: "Ninyi munaonipenda, mulio tayari kunifuata na kupata mateso kwa ajili yangu wakati ninapokataliwa kwanza hapa duniani ... nitasema na malaika hawa kuwatumikia ninyi mutakaoriti wokovu. Mukisumbuka sasa na kupata haya kwa ajili yangu, musilegee rohoni. Watumishi wangu hawa, ndio malaika, watawalinda ninyi kwa safari yenu nzima kufika siku nitakapowaleta ninyi kuketi pamoja nami katika utukufu wangu."

# *Utu wa Kristo*
# *Sura 2*

Sura 1 ya Waebrania ilionyesha wazi sana ya kwamba Yesu ni Mungu. Neno hili ni neno kubwa sana na liligawa wale walioamini na wale wasioamini. Wayuda walikuwa wamesulibisha Yesu mbele ya watu wote kwa sababu alisema yeye ni Mungu nao walifikili yeye ni mutu tu.

Halafu ndani ya sura 2 mwandishi alifundisha juu ya utu wa Bwana Yesu na mateso aliyojipatia wakati alipofika hapa duniani kwa mwili wa mutu.

Wafuata wa Bwana Yesu walishituka kabisa wakati alipowaambia ya kwamba taifa lao watamukataa na ya kwamba itamupasa kuteswa sana. Walifikili Bwana Yesu atakomboa Israeli lakini wakubwa wao walimuhukumu kufa (Luka 24:41)!

Halafu Bwana Yesu alifufuka toka wafu na kurudia mbingu na Roho Mutakatifu alikuja. Ilionekana wazi ya kwamba taifa la Israeli walikuwa wameanguka wakati waliposulibisha Bwana Yesu na watu wengi walimwamini na kuokolewa. Wahubiri kwa wakati ule walifundisha ya kwamba Yesu ni Masiya. Hata kama wakubwa walimuhukumu kusulibishwa, Mungu alimufufua toka wafu. Waliweza kuona wao wenyewe unabii ndani ya Agano la Kale ya kuwa Masiya atakataliwa na atateswa. Hivi Petro aliwaambia watawala ya kwamba bila kujua walikuwa wametimiza unabii wa Agano la Kale wakati walipohukumu Bwana Yesu kuteswa na kufa (Matendo 3:18).

Wayuda walioamini Yesu hata kama alisulibishwa walikuwa tayari kusimamia Mwokozi aliyeteswa kwa sababu waliamini alikuwa amefufuka toka wafu na atarudi nyuma kidogo na uwezo na utukufu mukubwa.

Lakini miaka ilikuwa ikipita. Wengi wa Wakristo wale wa kwanza walikuwa wamekufa. Wakristo wengine walianza kusitasita kwa sababu mateso yao kwa Kristo hayakupunguka lakini yalizidi kuongezeka. Kwa sababu hii mwandishi alifikili pamoja na kuwafundisha juu ya uungu wa Bwana Yesu ilimupasa vilevile kuwafundisha juu ya utu wake na mateso yake. Atawaonyeshea ya kwamba Yesu ni Masiya na

atatukuzwa kwa sababu ya mateso yale yale. Kristo hakuteswa kwa bahati mbaya tu, lakini mateso yale yalikuwa njia Mungu aliyomutayarishia na kusudi, wala hakuna njia nyingine kwa yeye kufikia utukufu na kupeleka pamoja naye wana wengi Mungu aliowachagua kushiriki ndani ya utukufu ule. Iliweza kusaidia Wakristo wale sana kufahamu ya kuwa mateso yao na mateso ya Kapiteni wa wokovu wao hayakuwa kizuizo ilichowapasa kujaribu kushinda. Hayakuwa haya iliyowapasa sana kujaribu kusahau lakini yalikuwa njia Mungu aliyowatayarishia na kuwachagulia kuwapeleka hata utukufu.

*MAONYO, 2.1-4*

Basi tuangalie sura hii pamoja polepole. Kwanza tunaona ya kwamba mwandishi anatoa maonyo nyuma ya mafundisho juu ya uungu wa Bwana Yesu ndani ya sura 1 na mbele ya kuendelea na mafundisho juu ya utu wake:

> *''Kwa sababu ile imetupasa kuangalia zaidi maneno tuliyoyasikia tusije tukayaacha kuponyoka.''*

Alikuwa ameonyesha ya kwamba kwa siku hizi za mwisho Mungu hakusema kwa njia ya mutu fulani tu lakini kwa njia ya Mungu. Ndani ya Agano la Kale Mungu alisema kwa njia ya manabii, na kwa njia ya malaika vilevile wakati alipotolea Musa na Waisraeli sheria, na watu wale walioasi waliazibiwa mara moja na ukali. Basi kama Mungu aliazibu watu walioasi maagizo aliyoyatoa kwa njia ya malaika, ataazibu zaidi wale wanaoasi habari hizi zilizowafikia kwa njia ya Mwana wa Mungu aliye Mungu kabisa!

Ilikuwa hatari kabisa kwa wakati wa Agano la Kale kuasi sheria ya Mungu. Unakumbuka habari za mutu yule aliyeokota kuni siku ya sabato? Mutu huyu alijua sheria ya Mungu lakini aliiasi. Lilikuwa tendo dogo tu, kuokota nusu ya kuni, lakini Mungu aliagiza wapeleke mutu huyu inje ya kambi na kumwua kwa njia ya kumutupia mawe. Ona Hesabu 15:32-36. Ilikuwa vibaya kwa watu kuona bule maneno Mungu aliyosema kwa njia ya malaika. Ni vibaya zaidi kwa sisi kuona bule maneno Mungu aliyosema nasi kwa njia ya Mwana wake!

Basi wokovu wetu ni wokovu mukubwa sana. Bwana yeye mwenyewe alitoa habari zake kwanza, na wale waliomusikia walihakikisha habari hizi kwetu. Mungu vilevile alihakikisha habari hizi kwa njia ya zawadi za Roho Mutakatifu na kwa njia ya maajabu. Basi sisi tutapona namna gani kama tusipochunga wokovu mukubwa namna hii?

Ona ya kwamba tunasoma: *Tu*tapona namna gani kama *tu*sipochunga...'' Neno hili linatuleta kufikili ya kwamba mashairi haya yaliandikwa kwa Wakristo. Basi Wakristo wamepona, wameokolewa. Watapona tena mara ya pili? Sivyo. Tutaje tena shairi moja tulilolitaja

mbele, ndilo 6:9, *"Hata tukisema hivi tumesadiki maneno mazuri zaidi juu yenu, yaliyo ya wokovu."* Mwandishi alikuwa akisema maneno kama haya: "Hata kama ninaandika sawasawa hamujaokolewa bado, ninafikili ninaweza kuona matunda ndani ya maisha yenu yanayoonyesha ya kwamba mumeokolewa kweli."

Kama mutu akiamini kweli kweli, Neno la Mungu linasema mutu huyu ameokolewa kwa milele na hatapotea kamwe. Lakini mutu huyu aliyekiri ya kwamba aliamini, aliamini kweli kweli? Hatuwezi kujua kabisa. Tunaweza kujua tu kwa kipimo, kwa njia ya matendo yake. Labda matendo yake hayaonyeshi wazi ya kwamba aliamini kweli. Basi mengine ya matendo ya Waebrania yaliamsha shaka ndani ya roho ya mwandishi kama waliokolewa kweli, hivi alifikili sharti awaonye juu ya maneno haya, hata kama ndani ya roho yake alifikili ya kwamba walikuwa wameokolewa.

Maneno haya ni maneno makubwa. Tuwaze sana juu yao! Inawezekana kujua habari za wokovu na akili yetu tu na kupotea kwa milele kwa sababu hatukushikamana nao na imani ya kweli. Tutapona namna gani kama tusipochunga, kama tukiona bule wokovu mukubwa namna hii?

Halafu mwandishi aliwakumbusha ya kuwa wakati Habari Njema ilipowafikia, ilifika pamoja na alama na maajabu kuhakikisha ya kwamba ilitoka kwa Mungu. Tunaweza kusoma juu ya maalama haya ndani ya kitabu cha Matendo. Watu walishangaa kabisa na waliamini wakati walipoona wagonjwa wakiponyeshwa, viwete wakiweza kutembea na vipofu wakiweza kuona tena. Ilikuwa kama muda ule wa baraka waliosoma juu yake ndani ya Agano la Kale ulikuwa umewafikia.

### *2:5-8*

### *Mutu Kristo Yesu*

Lakini muda ule ulikuwa haujafika bado. Na ulimwengu ule unaokuja haukuwekwa chini ya malaika lakini chini ya mutu. Ni kama mwandishi alisema na Waebrania: "Munaona utu wa Yesu wa Nazareti bule? Viongozi wenu wanasema na kuzarau juu ya nabii yule wa Galilaya asiyejifunza maneno? Wanamuzarau kwa sababu alikuwa mutu munyenyekevu na alizaliwa nyumbani mwa seremala? Wanajisifu kwa sababu sheria yao ilitolewa kwa njia ya malaika, si kwa njia ya seremala aliyekaa pamoja na wavuvi?"

Basi watu wale wafahamu ya kwamba muda ule muzuri walioutazamia na tumaini kubwa haukuwekwa chini ya malaika, lakini mutu mumoja katika pahali fulani alishuhudia akisema, *"Mutu ni nani hata umukumbuke?"* Zamani sana, ndani ya Agano la Kale (Zaburi 8:4-6) Mungu alionyesha ya kwamba hakukusudi kwa malaika kuongoza

muda ule unaokuja. Lilikuwa shauri la Mungu tangu zamani kuweka maneno yote chini ya mutu.

Tunakumbuka namna Mungu alivyoumba mume na muke na kuwaweka shambani. Aliwabariki na kusema nao: *"Muzidi na kuongezeka, na mujaze tena inchi na kuitiisha"* (Mwanzo 1:28). Mungu alikusudi tangu zamani kwa dunia hii kutawaliwa na watu, si malaika. Ndiyo, alifanya mutu chini kupita malaika. Malaika ni roho. Mutu ni roho na mwili, lakini Mungu amemuvalisha taji ya utukufu na heshima na kuweka vitu vyote chini ya miguu yake, si nyama tu lakini ndege na samaki vilevile.

*Yote chini ya Kristo*

Mwandishi wa Zaburi 8 alisema Mungu ameweka *"vitu vyote chini ya miguu yake"* (sh.6). Mwandishi wa Waebrania alitaja shairi hili ndani ya shairi 8, akiongeza ya kama Mungu alifanya hivi kweli kweli wala hakuacha hata kitu kimoja kisichowekwa chini yake. Hili lilikuwa shauri la Mungu tangu zamani. Lakini si nguvu kuona ya kwamba shauri hili halijatimizwa bado. Nyama wakali kama simba wanatii watu kweli kwa wakati wa sasa? Watu wanalima shamba lakini saa zote inawapasa kushindana na majani mabaya yanayozidi kuota, na kushindana vilevile na vidudu vinavyotaka kula vyakula walivyovipanda. Hata kama watu wamejifunza maneno mengi juu ya kazi ya dawa, wanateswa na gonjwa mbalimbali hata sasa. Dunia hii ni pahali pa taabu tu, maisha ya watu ni mafupi, gonjwa zinazidi, na mwisho wao ni kufa. *"Hatujaona bado vitu vyote kuwekwa chini yake."* Ni kweli kabisa!

*2:9-10*

Basi Mungu ameacha shauri lake la mbele kwa sababu zambi imeingia duniani na mutu aliasi maagizo yake? Sivyo, Mungu hakuacha shauri lake hata kidogo. Wenye imani wanaweza kuona ya kwamba yeye ni karibu kutimiza shauri lake. Anataka dunia kwa wakati wa kuja kuwa chini ya mutu, si chini ya malaika. Na kuna mumoja aliyefanywa kwa saa kidogo chini ya malaika kwa sababu alikamata mwili na damu na kugeuka mutu, ndilo neno malaika wasiloweza kulifanya kamwe. Jina lake ni Yesu, jina lake la kibinadamu. Hatuagizwi hapa kuwaza juu yake kama Mwana wa Mungu lakini kama yule aliyegeuka Mutu na kupokea jina kwa lugha ya watu. Ni jina la Kiebrania. Maria na Yosefu walimupa jina hili wakiongozwa na malaika. Ndiyo, tunaona *Yesu.*

*Mateso, kisha utukufu*

Ni kweli ya kwamba watu walikataa Bwana Yesu na kumuhaya-

risha, naye aliteswa juu ya musalaba, lakini sasa amevalishwa taji ya utukufu na heshima.

Ndiyo, Bwana Yesu alitiwa taji ya utukufu na heshima *kwa sababu* aliteswa na kufa. Mutu alitenda zambi na alipoteza utukufu wake. Kuna njia moja tu kwa mutu kufikia utukufu ule tena, ndiyo mateso. Bwana Yesu hakuteswa na kufa musalabani kwa sababu ya bahati mbaya lakini kwa sababu *kwa njia hii* Mungu alikusudi kumuvalisha taji ya utukufu na heshima. Mateso yale hayakuwa haya lakini neno la kujisifu ndani yake.

Na kwa sababu ya mateso na kufa kwa Kristo ukombozi unapatikana kwa vitu vyote kwa sababu ya neema ya ajabu ya Mungu. Kwa sababu Bwana Yesu alionja kufa, vitu vyote vitapatanishwa na Mungu kwa wakati wa kuja, vitu mbinguni na duniani (Wakolosayi 1:20).

*Kristo aliteswa kwa sababu gani?*

Ni kama njia nyingine haikuwa kuleta wana wengi kwa utukufu (sh.10). Unauliza kwa nini Mungu hakutumia uwezo wake na kutuma majeshi kumi na mawili ya malaika kuponyesha Mwana wake na Petro na waamini wengine na kuwapeleka mbinguni mara moja?

Ndiyo, Mungu alikuwa na uwezo kufanya hivi, lakini isingalikuwa vizuri. Haiwezekani kupeleka watu wenye zambi kama sisi mara moja mbinguni. Sharti tutayarishwe polepole kwa pahali pale pa utukufu. Tunaweza kutayarishwa kwa njia gani? Kwa njia ya mateso tu. Si kazi yetu kuulizana na Mungu juu ya namna anavyofanya kazi yake. Kazi yetu ni kuangalia tu. Lakini ukikumbuka ya kwamba Mungu anatumia maumivu kutayarisha watoto wake kwa mbingu, utafahamu kwa nini Wakristo wengi wanapata mateso na maumivu. Halafu kwa kuwaleta hata pahali pale pa utukufu Mungu aliwapa Kiongozi wa wokovu, ndiye Yesu, aliyewapatia wokovu na anayewaongoza kufika mbinguni. Lakini kiongozi asiyejuana na mateso yeye mwenyewe hakuweza kuwasaidia vizuri. Musa alikuwa kiongozi muzuri kwa Waisraeli kwa safari yao ndefu jangwani kwa sababu Mungu alimutayarisha jangwani mbele naye alijuana na taabu ya jangwa. Vivyo hivyo ilipasa Kristo kujuana na mateso yeye mwenyewe ili aweze kuwa Kiongozi muzuri kutuongoza katika taabu na mateso ya dunia hii na kutufikisha mbinguni.

*2:11-13*

Kiongozi wetu aliteswa na anastahili kutuongoza. Zaidi ya ile amegeuka mutu kama sisi. Yeye ni Mungu na mutu vilevile. Yeye anayetakasa nao wenye kutakaswa wote pia wanatoka kwa mumoja na kwa sababu hii haoni haya kutuita ndugu.

*"Haoni haya."* Mwandishi wa barua hii aliandika juu ya haya

tena na tena. Kwa nini? Kwa sababu Waebrania wale walianza kuwa na haya juu ya Bwana Yesu. Labda ilikuwa haya iliyowazuiza wasikutane tena pamoja. Tunaweza kuwafahamu vizuri kwani sisi vilevile tumeona haya juu ya Bwana wetu mara nyingine. Lakini tufikili kwanza kama Yesu ni nani. Yeye ni *Mungu!* Nasi tunaona haya juu yake? Kabisa kabisa ni yeye anayeweza kuona haya juu yetu! Lakini *"haoni haya* kuwaita ndugu zake"! Neema kubwa!

Haifai kwetu kuwa na haya juu ya unyenyekevu wa Bwana yetu. Ingetupasa kujisifu ndani yake. Hakuna dini yo yote iliyo na Mwokozi mwenye utukufu na ajabu aliyekubali kuwa sawa na watu wake na kuwaita ndugu. Ni neno Mukristo analoweza kujisifu juu yake. Kuna unabii juu ya maneno haya hata ndani ya Agano la Kale.

### *Mateso ya Daudi na ya Kristo*

Ndani ya Zaburi 22:22 tunasoma: *"Nitahubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kusanyiko nitakusifu."* Daudi aliandika maneno haya lakini hayakutimizwa kabisa ndani ya maisha yake hata kama aliteswa sana yeye mwenyewe. Agano la Kale lilitazamia Mumoja atakayekuja na atakayeteswa zaidi.

Mwenendo wa Waisraeli ulikuwa mwovu lakini wakati walipolilia Mungu, Mungu aliwasikia. Mwenendo wa Yesu ulikuwa mukamilifu kabisa lakini *hakusikiwa* wakati alipolia — ao hata akisikiwa hakupata jibu (Zaburi 22:1-6). Zaburi 22 ni unabii juu ya Yule atakayekuja na atakayelia juu ya musalaba: *"Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"* (Matayo 27:46). Alijua kwa nini ilipasa Mungu kumwacha, hata kama aliuliza hivi. Aliachwa kwa sababu ya kufungana na ndugu zake, kwa sababu alikataa kujitenga nao hata kama walikuwa zaifu na waovu, hata kama walipoteza utukufu wao kwa njia ya kufanya zambi. Alichagua kuwaita ndugu zake na kubeba azabu wao waliyostahili kuipata kwa zambi zao. Na nyuma ya kuvumilia taabu hii yote kwa kuwapatia ukombozi alisema juu yao na mapendo: *"Nitahubiri jina lako kwa ndugu zangu."*

Baba anapenda mutoto wake, lakini mapendo ya mama aliyepata taabu kwa njia ya kuzaa mutoto huyu ni makubwa zaidi. Bwana Yesu alipenda wafuata wake hata mbele ya kufa musalabani, lakini sasa nyuma ya kubeba mateso makali kwa ajili yao yeye ni karibu zaidi nao.

### *Isaya*

Isaya vilevile aliishi kwa wakati wa matata katika taifa la Yuda. Zambi zilizidi, watu walishindwa vitani, Mufalme Uzia aligeuka mukoma, akakufa, na kwa miaka mingi wafalme waliotangulia Uzia, hata mumoja wao hakufa na salama; wote waliuawa. Lakini hata ndani ya giza na taabu ile yote nabii alikuwa na tumaini. Alisema: *"Tazama,*

*mimi pamoja na watoto niliopewa na Mungu*'' (Isaya 8:18).

Kwa njia ya masemo haya nabii alionyesha ya kwamba aliamini Mungu kabisa. Ni kama alisema: ''Hata matata ni mengi, ninaamini ya kwamba Mungu atanishindisha pamoja na watoto wangu.'' Lakini hakujua maana nzima ya masemo yake, ya kwamba yatatimizwa kabisa ndani ya Bwana Yesu. Bwana Yesu kama mutu angeweza kusema maneno kama haya: ''Nitaweka imani yangu ndani ya Mungu lakini si kwa mimi mwenyewe tu lakini kwa watoto hawa Mungu alionipa. Ninajua taifa la Israeli wamenikataa, na nimewaambia watoto wangu ya kwamba watapata mateso hapa duniani. Hata hivi ninatumainia Mungu na ninajua ya kwamba atatushindisha na kutuleta hata utukufu.''

Hivi tunaona ya kwamba Bwana Yesu anatuita watoto wake. Na tunajisifu juu ya Mwokozi anayefanyiza taabu na mateso kuwa njia itakayotufikisha hata utukufu, na zaidi ya ile yeye ni karibu sana nasi hata kushiriki ndani ya taabu yetu yeye mwenyewe.

## *ASILI YA WATU, 2:14-15*

Halafu tunaona ya kwamba kwa sababu watoto wameshiriki damu na mwili, *''yeye mwenyewe vivyo hivyo alishiriki kama wao, hata kwa njia ya kufa apate kuharibu yeye aliyekuwa na nguvu za kufa, ndiye Shetani, na kuwafungua wale wote waliokuwa maisha yao yote katika hali ya utumwa, kwa woga wa mauti*'' (2:14-15). Tumewaza juu ya mateso ya Kristo; sasa tunaona kwa sababu gani aliteswa. Ametupenda, lakini sisi watu tuko mwili na damu, na tangu zambi ilipoingia dunia, mwili na damu zimelaaniwa na mauti yanamaliza maisha yetu. Sisi sote hatutaki kufa. Mauti yanasumbusha roho zetu na kuamusha maulizo mengi ndani ya nia zetu. Ni faida gani kuishi hapa duniani kama mwisho wake ni mauti ya huzuni na kuumia? Bwana Yesu alijua mafazaiko ya roho zetu.

Na aliona mwingine vilevile, adui wetu, ndiye Shetani anayefunga wanaume na wanawake maisha yao mazima katika woga wa mauti. Furaha ya watu inapunguka wakati wanapokumbuka ya kwamba watakufa nyuma kidogo na wanaogopa nini itawapata nyuma ya kufa.

Unauliza: ''Nini ingalitokea kama Adamu asingalifanya zambi? Angaliishi kwa milele hapa duniani?'' Sijui. Mungu hakutujulisha neno hili. Ninajua tu ya kwamba hata Adamu alifanya zambi na hata kama mauti yakimaliza maisha ya kila mutu duniani, mauti haiogopeshi tena watu wale wanaoamini Yesu. Na hata kama mauti inaleta huzuni, hatushindwi na huzuni kama wale wasio na tumaini.

Kwa nini Mukristo haogopi mauti tena? Kwa sababu Kristo alikufa vilevile na kushinda adui wetu aliyetaka kutuharibu, ndiye Shetani.

Sasa mauti kwa mwamini ni kama mulango tu kwa njia yake anaingia mbinguni.

### *KRISTO ALIGEUKA MUTU, 2:16-18*

Maneno tunayokwisha kusoma juu ya Mwokozi wetu yangepasa kujaza mioyo yetu na mapendo kwake. Lakini zaidi ya maneno yale yote alitwaa asili ya watu, maana yake aligeuka mutu ili aweze kuwasaidia. Ilimupasa kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote. Waza juu ya maneno haya:

1. Aliteswa — kusudi aweze kutukuzwa.
2. Aliteswa — kumustahilisha kuleta wana wengi hata utukufu.
3. Aliteswa — kusudi ashinde adui wetu Shetani. Sisi hatukuweza kumushinda, hivi Mwana wa Mungu aligeuka mutu na kumushinda kwa sisi.

Shairi 17 linasema "*ilimupasa* kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote." Maana yake nini? Haikuwa lazima kwa Mwana wa Mungu kutwaa asili ya mazao ya Abrahamu. Yeye mwenyewe alichagua kufanya hivi. Haikuwa sharti kwake kuokoa mutu ye yote. Alifanya hivi na kutaka kwake mwenyewe. Lakini wakati alipokwisha kutwaa asili ya watu ilikuwa sharti kwake kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote. Kwa nini? Kwa sababu sisi watu ni zaifu. Tunaanguka tena na tena na tunahitaji Kuhani aliye mwaminifu na mwenye rehema. Kwa sababu hii ilipasa Bwana Yesu kufananishwa na ndugu zake katika maneno yote kusudi aweze kuwa Kuhani mukubwa mwenye rehema na mwaminifu katika mambo ya Mungu (2:17).

Kristo alikaa duniani namna watu wa wakati ule walivyokaa. Alikuwa masikini hapa duniani. Wafuata wake walikaa vizuri kupita yeye. Walikuwa na nyumba zao, lakini Bwana Yesu alikosa pahali alipoweza kulalisha kichwa chake. Hivi anaweza kufahamu taabu ya watu wa dunia, hata ya wale walio masikini kabisa.

Kweli Mwokozi namna hii anastahili kupokea kuabudu kwetu! Una haya juu ya mateso yake? Mateso yale yale ni utukufu wake. Ni utukufu kwetu vilevile kuwa na Mwokozi namna hii na kujua ya kwamba hata saa hii ya sasa anatuombea. Yeye mwenyewe alijaribiwa, na majaribu yenyewe yalikuwa hata makubwa na machungu kupita majaribu yetu kwani yeye peke yake hakushindwa na majaribu. Kwa sababu hii anaweza kutusaidia wakati tunapojaribiwa na anafanya hivi na rehema, akitusimamia mbele ya Mungu kwa njia ya sadaka yake musalabani na kwa njia ya kutuombea.

# *Raha Yetu*
# *Sura 3 na 4*

Barua kwa Waebrania inajulikana kwa sababu ya maonyo yake na ndani ya sura 3 na 4 tunapata onyo lingine. Tuweke roho sana tuweze kufahamu vizuri maneno Roho Mutakatifu anayotaka kusema nasi.

Ona ya kwamba mara moja mbele ya kutoa onyo hili Roho Mutakatifu alisema nasi juu ya ukuhani wa Bwana Yesu Kristo. Halafu kwa mwisho wa onyo anatukumbusha tena Kuhani wetu Mukubwa anayetuhurumia ndani ya uzaifu wetu (4:14-16). Hivi wakati tunapowaza juu ya onyo hili tukumbuke ya kwamba Kuhani wetu Mukubwa, Kuhani mwaminifu na mwenye rehema, anasema maneno haya nasi. Hata yakituonyeshea uzaifu wetu, uzaifu huu utusukume tena karibu naye anayetaka kutupa sisi neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

*3:1-5*

Ndani ya sura 2 tuliona ya kwamba Bwana Yesu aligeuka Mutu ili aweze kuwa Kuhani Mukubwa mwenye rehema, na mwaminifu katika mambo ya Mungu. Sasa kwa mwanzo wa sura 3 mwandishi anatuomba kufikili. Kwa kujua Kitabu cha Mungu inatupasa kufanya maneno mawili:

1) Inatupasa kusoma na kujifunza kabisa kama Biblia inasema nini;
2) Inatupasa kuweka saa kufikili juu ya maneno tunayokwisha kuyasoma.

Tumewaza juu ya Bwana Yesu kama Mungu, mwenye kututolea habari za Mungu. Tumewaza juu yake kama Mutu anayestahili kuwa Kuhani wetu Mukubwa. Halafu mwandishi anasema: *''Kwa sababu ile, ndugu watakatifu, wenye kushiriki mwito wa mbingu, mufikili sana Yesu, mutume na Kuhani Mukubwa la imani tunayoikiri''* (3:1).

Tufikili nini juu yake? Shairi 2 linasema tumufikili yeye *''aliyekuwa mwaminifu kwake yeye aliyemuweka, kama Musa alivyokuwa*

*katika nyumba yake yote.*" Kwa Kiyunani maana yake ni "*aliye* mwaminifu," si *aliyekuwa* mwaminifu kwa wakati uliopita tu. Hata *sasa* yeye ni mwaminifu kama Kuhani wetu Mukubwa, mwaminifu kwa Mungu, ndani ya nyumba nzima ya Mungu. Bila shaka unauliza kwa nini Roho Mutakatifu anataja Musa hapa. Fungua Hesabu 12 basi na soma mashairi 1-8.

*Musa*

Maneno haya: "*kama Musa alivyokuwa mwaminifu katika nyumba nzima ya Mungu*" yanatoka kwa Hesabu 12:7. Ndani ya sura ile Miriamu na Haruni walikuwa wakinungunikia Musa juu ya mwanamuke Musa aliyemwoa, na Mungu aliwahukumu juu ya neno hili. Lakini Musa alikuwa mutu wa neema, na neema yake ilionekana wazi hapa. Waisraeli walinungunikia Musa tena na tena na tunashangaa kwa sababu hakuwakasirikia. Angaliweza kubaki nyumbani mwa kifalme katika Misri lakini aliacha maneno haya yote kusudi aweze kufungua watu wa taifa lake toka utumwa. Alijitoa kabisa kuwasaidia lakini kwa pahali pa kumupa asante walizidi kumunungunikia.

Hata hivi Musa alibaki mwaminifu kwa Mungu katika kazi ile Mungu aliyomugawia, ndiyo kuwa kiongozi mukubwa wa wokovu wa watu wa Mungu. Basi mwandishi wa Waebrania anasema: "*Ndugu watakatifu, wenye kushiriki mwito wa mbingu* (ndio mwito unaotuongoza kupita katika dunia hii hata kutufikisha mbinguni), *mufikili Kiongozi mukubwa wa wokovu wenu,*" ndiye Yesu. Tumemunungunikia tena na tena juu ya maneno mbalimbali, lakini tumufikili yeye aliye mwaminifu hata hivi na atakayekuwa mwaminifu kufika wakati atakapotufikisha kwake mbinguni.

Ndiyo, Musa alikuwa mwaminifu lakini hata hivi alianguka siku nyingine na kukasirikia watu wake sana, na kwa sababu hii hakuweza kuingia inchi ya ahadi (Hesabu 20:7-13). Labda unafikili hukumu ya Mungu ilikuwa kali zaidi. Lakini Mungu alikuwa amemupa Musa kazi ya kuchunga watu wake na kwa sababu ilishinda Musa kufanya kazi yenyewe bila kuwakasirikia ilipasa Mungu kumwondolea kazi ile. Mungu ametupa sisi vilevile Kiongozi mukubwa cha wokovu wetu, ndiye Yesu, na kumupa kazi ya kutulinda na kutuongoza kufika siku tutakapofika mbinguni. Tusifu Mungu kwa sababu tunajua Kapiteni wetu hawezi kuanguka wala kutukasirikia kamwe lakini atatimiza kabisa kazi hii Mungu aliyomugawia. Anaweza kuokoa kabisa watu wale wanaokuja kwake Mungu kwa njia yake.

Halafu mwandishi aliendelea kusawanisha utukufu wa Kristo na utukufu wa Musa. Alionyesha ya kwamba Musa alikuwa mutumishi tu ndani ya hema ya Mungu lakini Kristo ni Mwana wa mwenye kuijenga.

*3:6-14*

Tuwaze sana juu ya maonyo mwandishi anayotutolea sasa. Musa aliwekwa juu ya nyumba iliyojengwa na miti, zahabu na kitani, lakini mbao ndani ya nyumba ya Kristo ni watu wenye uzima, "ndiyo nyumba yake sisi, *kama* ..." Kama nini? Neno hili *kama* linaamsha shaka ndani ya roho zetu. Tunaliona tena ndani ya shairi 14, "Tumekuwa washiriki wa Kristo *kama* tukishika na nguvu mwanzo wa kukiri kwetu mupaka mwisho."

*Kama ...*

Tuwaze juu ya *kama* hizi. Ndani ya shairi 14 tunasoma ya kwamba tu*me*kuwa washiriki wa Kristo. Neno lenyewe linakwisha kufanyikana. Basi namna gani linaweza kusimama juu ya kushikamana na "kukiri kwetu mupaka mwisho"? Maana yake nini? Ni hii: Kila mwamini amegeuka mushiriki wa Kristo, lakini tunaweza kujua namna gani kama mutu fulani ni mwamini wa kweli? Mutu anaonyesha ya kwamba yeye ni mwamini wa kweli kwa njia ya kushika sana ujasiri wake mupaka mwisho.

Basi nini inatokea kama mutu *asi*poshika ujasiri huu? Ni kusema yeye si Mukristo tena? Ao labda hajaamini bado? Kwa kujibu ulizo hili Roho Mutakatifu ametupa sisi mufano muzuri ndani ya Agano la Kale. Soma mashairi 7-11 tena polepole pamoja na Zaburi 95:7-11.

Mwandishi wa barua hii kwa Waebrania aliandika kwa watu waliokwisha kukiri ya kwamba wameamini Bwana Yesu Kristo ni Masiya wao. Lakini matendo ya watu hawa yalikumbusha mwandishi juu ya maneno yaliyopata baba zao kwa wakati wa Agano la Kale. Baba zao walikombolewa toka Misri, walifunikwa na damu na kuanza safari kwendea inchi ya raha Mungu aliyoahidi kuwapa, lakini watu wachache tu katikati yao walifikia inchi ile. Walikasirisha Bwana sana hata aliapa katika hasira yake ya kwamba hawataingia kamwe katika raha yake. Basi tukae na ange ili maneno namna hii yasitokee tena.

"*Angalieni, ndugu zangu, asiwe katikati yenu mumoja mwenye moyo mubaya wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai*" (3:12). "*Mwonyane ... ili hata mumoja wenu asifanyike mugumu kwa udanganyifu wa zambi*" (3:13). "*Kwa kuwa ahadi hii ya kuingia katika raha yake ingali pamoja nasi, tuogope basi, mumoja wenu asije ameonekana kukosa kuipata*" (4:1). "*Basi tudumu sana kuingia katika raha ile isije mutu, hata mumoja, aanguke kwa namna ile ile ya kuasi*" (4:11).

Sharti tuweke roho sana kusudi tufahamu maneno haya vizuri. Onyo la kwanza ni juu ya kuwa na moyo mubaya wa kutokuamini. La pili ni juu ya udanganyifu wa zambi. Na kwa sura 4 tulisoma juu ya

kuasi. Kweli sisi waamini hatuamini ahadi za Mungu kabisa kila mara. Na mara nyingine tunafanya zambi na kama tukiendelea ndani ya zambi, zamiri zetu zinageuka ngumu na tunadanganywa na zambi. Basi kufanya zambi ni kuasi maagizo ya Mungu, hivi tuko wenye kuasi vilevile.

Hivi ni kusema ya kama sisi waamini hatutaingia raha ile Mungu aliyoahidi kutupa kama tusipoamini ahadi zote za Mungu, na kama tukifanya zambi na kuasi Mungu?

*Moyo wa kutokuamini*

Sivyo, hii si maana ya mashairi haya. Soma 3:12 tena. Mutu aliye na moyo mubaya wa kutokuamini ni mutu mubaya, mwovu, musiyeamini.

Halafu soma 3:13 tena. Zambi ni nini? Bwana Yesu alisema katika Yoane 16:8-9 ya kwamba wakati Roho Mutakatifu atakapokuja *"atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu; kwa maneno ya zambi, kwa sababu hawaniamini mimi."* Kuja kwa Roho Mutakatifu kulimaliza mabishano ya watu juu ya Yesu, kama yeye ni Mwana wa Mungu ao sivyo. Wayuda walisema yeye si Mwana wa Mungu na walimusulibisha hata kama alikuwa amefanya maajabu mengi kupita mutu ye yote. Basi Bwana Yesu alikufa, na alifufuka na kwenda mbinguni. Nyuma yake alituma Musaidizi kwa jina lake, ndiye Roho Mutakatifu, naye alihakikisha ya kwamba ilikuwa zambi kwa watu wale kukataa kumwamini. Ilipasa maajabu yaliyofanyikana kwa uwezo wa Roho Mutakatifu siku ya Pentekote kuaminisha watu ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na kweli wale waliokataa kuamini walikuwa na moyo mubaya wa kutokuamini, ndio shina la zambi zote.

*Kuasi*

Labda unataka kuuliza: "Katika 4:11 tunaona ya kwamba inawezekana kwa sisi kuanguka kwa namna ile ile ya kuasi. Ni kusema haiwezekani kwa mwamini kuasi?"

Sivyo. Waamini wanaasi mara nyingine. Lakini shairi hili halisemi juu ya waamini. Tusome Matendo 14:2: *"Lakini Wayuda wasioamini waliamsha mataifa na kuwatia nia mbaya juu ya ndugu."* Neno kwa Kiyunani linalotafsiriwa "amini" linaweza kutafsiriwa "tii" vilevile.

Tunaona watu namna tatu ndani ya shairi hili: Wayuda, Mataifa, na ndugu waliokuwa waamini wa kweli. Mataifa walikuwa watu wa Mataifa wasioamini bado. Halafu Wayuda wale wasioamini walikuwa Wayuda waliokwisha kugeuka Wakristo lakini wasiofanya mapenzi ya Mungu kwa wakati ule? Sivyo. Walikuwa Wayuda waliokwisha kusikia Habari Njema na waliokataa kuipokea.

Sasa soma Matendo 19:9. Neno linalotafsiriwa hapa "kuamini" ni lile lililotumiwa ndani ya 14:2 na linaweza kutafsiriwa "kutii". Hapa vilevile linasema juu ya wasioamini.

Neno hili lilitumiwa ndani ya Yoane 3:36 vilevile, na hapa lilitafsiriwa "tii", "asiyetii Mwana..." Shairi hili linaonyesha wazi ya kwamba ukitaka kuokolewa sharti uamini Yesu, lakini wale wanaoasi Mwana wa Mungu wanapotea.

Katika lugha ya Kiyunani kuna maneno mawili yanayotafsiriwa "kuasi" katika Swahili: Maana ya neno tulilolisoma ndani ya Matendo 14:2; 19:9 na Yoane 3:36 ni "kukataa kukubali." Linatumiwa kwa watu wanaosikia Habari Njema juu ya Yesu na kuona uwezo wa Roho Mutakatifu, lakini wanaokataa kukubali maneno wanayoyasikia na hivi wanayaasi. Walisikia lakini hawataona uzima kwa sababu hawakukubali maneno waliyoyasikia. Makuhani na Wayuda wale walisikia Habari Njema lakini hawakuikubali na tunafikili walipotea. Halafu mwandishi kwa Waebrania alisema: "*Basi, tudumu sana kuingia katika raha ile, isije mutu, hata mumoja aanguke kwa namna ile ile ya kuasi*" (4:11). Hasemi juu ya kuasi kwa waamini, lakini juu ya kukubali ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

### *ISRAELI KATIKA JANGWA, 3:15-19*

Unakumbuka ya kwamba Waisraeli waliondokea Misri wakiongozwa na Musa na walianza safari yao kwendea inchi ya Kanana, ndiyo inchi ya raha. Lakini hawakufika pale. Walikasirisha Mungu naye hakuwaacha kuingia raha yake kamwe. Maiti zao zilianguka jangwani.

Maneno haya yanatufundisha nini? Tusome shairi 16 tena polepole: "*Maana ni nani waliokasirisha wakati waliposikia?*" Wote walikasirisha Mungu ila watu wawili, ndio Yosua na Kalebu nao wote walikufa jangwani kwa sababu walikosa (sh.17). Walikasirisha Mungu wakati gani? Wakati walipofikia mupaka wa inchi ya Kanana na walipotuma wapelelezi na wapelelezi hawa waliporudi na habari mbaya hata Waisraeli walikataa kuingia inchi. Hata kama Musa na Yosua na Kalebu walisemezana nao na kuwakumbusha ahadi ya Mungu kuwapa inchi ya Kanana, walikataa kuamini na kukubali.

Unafikili watu wale walikuwa waamini wa kweli waliorudi nyuma kwa wakati kidogo? Sivyo. Roho Mutakatifu anaonyesha wazi ya kwamba hawakuingia kwa sababu waliasi, kwa sababu hawakukubali. Hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao. Hawakuwa waamini.

### *KUTOKUAMINI HABARI NJEMA, 4:1-3*

Basi ni nini watu wale wasioiamini? Waliamini Musa wakati alipowaambia ya kwamba atawaondoa katika Misri! Soma 4:2 tena:

*"Maana ni kweli, sisi vilevile tumehubiriwa Habari Njema kama wale. Lakini neno lile walilosikia halikuwapa faida, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia."*

Shairi hili linasema hawakuamini *Habari Njema*. Sisi tunahubiriwa Habari Njema nao walihubiriwa Habari Njema na hawakuingia inchi ya Kanana kwa sababu hawakuamini Habari Njema ile.

Vizuri tufahamu kama Habari Njema ni nini. Musa alifika karibu na Waisraeli na kuhubiri Habari Njema kwao na maneno kama haya: "Mungu amenituma kuwaokoa ninyi toka mizigo yenu na kuwaleta ninyi kwa inchi inayojaa maziwa na asali." Lakini Musa *hakusema* nao: "Neno kubwa tunalotaka kufanya ni kuwahubiri ninyi Habari Njema tu na kwa sisi kutoka katika Misri; maneno yote mengine si maneno makubwa; tutoke tu na nyuma yake munaweza kufanya kama munavyotaka." Sivyo, hii si Habari Njema.

Habari Njema ndiyo hii: "Munataka kufikia inchi ya Kanana? Mungu anaweza, naye ni tayari kuwaokoa ninyi toka Misri, kuwalinda jangwani na kuwafikisha ninyi kwa inchi ya ahadi, ndiyo inchi ya Kanana. Munaamini neno hili?" Walisema waliamini lakini wakati walipofika kwa mupaka wa inchi ya ahadi walikataa kuingia.

Basi kusudi la Habari Njema Musa aliyowahubiri lilikuwa kuwaleta ndani ya inchi ya Kanana. Haikuwa faida kwao kuondokea Misri kama wasipoingia Kanana. Lakini matendo yao jangwani yalionyesha ya kwamba hawakuamini Mungu aliweza kuwaingiza ndani ya inchi ya ahadi.

Sharti tuangalie sana wakati tunapohubiri Habari Njema kwa watu. Haifai tuseme nao: "Neno kubwa ni kwa ninyi kupata usamehe kwa zambi zenu. Maneno yote mengine si neno." Sivyo, haifai tuhubiri Habari Njema hivi. Habari Njema ndiyo hii: Bwana Yesu alijitoa kufa kwa zambi zetu, na nyuma ya kutuokoa katika dunia hii mbovu ni kusudi lake kwa sisi kushiriki ndani ya raha yake kwa milele. Halafu mwenendo wetu katika jangwa la dunia hii unaonyesha kama tumeamini Habari Njema kweli.

### *RAHA YA MUNGU, 4:4-8*

Basi ni nini, raha ile Waisraeli wale wasiyoingia ndani yake na Mungu anayotaka sisi watu wake wa sasa kuipata? Ni kwa wakati wa sasa ao wakati wa kuja? Ni kwa sasa na kwa wakati wa kuja vilevile. Raha Waisraeli wasiyoingia ndani yake ilikuwa raha ya Kanana, inchi Mungu aliyoahidi kuwapa, inchi yenye vyakula vya kutosha. Sisi tuna uriti vilevile. Tukiuliza Petro atatuambia uriti huu umewekwa akiba kwasi mbinguni (1 Petro 1:4). Tukiuliza Paulo atasema tumekami-

lishwa hata sasa pamoja naye katika pahali pa mbingu, katika Kristo Yesu (Waefeso 2:6). Wao wawili wanasema kweli. Hata kama tutaingia ndani ya raha kabisa kabisa kwa wakati wa kuja, sisi tunaoamini tunaingia ndani yake sasa vilevile. Maandiko Matakatifu yanasema: ''sisi tulioamini tu*na*ingia katika raha ile'' (4:3). Hatuhitaji kungojea siku tutakapofika mbinguni.

Raha yenyewe ni raha ya Mungu iliyoanza wakati Mungu alipomaliza kuumba dunia. Mungu alitumika siku sita kuumba dunia. Alifanya vyote vizuri na vikamilifu na nyuma yake alipumzika. Katika jangwa Mungu alisema Waisraeli wale hawataingia ndani ya raha yake (sh.5). Lakini hata hivi kulikuwa na wachache walioingia, na Mungu alisema juu yao hivi: ''*Yeye aliyeingia katika raha yake amepumzika kwa kazi zake, kama vile Mungu alivyopumzika nyuma ya kazi zake*'' (sh.10).

Sasa unaanza kufahamu kama kuingia ndani ya raha ya Mungu ni nini? Ni kuacha kutegemea kazi yako, matendo yako mema, na kuingia raha ya Mungu, ndiyo kupokea wokovu wa Mungu kwa imani. Kwa nini tunaweza kuingia raha ya Mungu hivi? Kwa sababu Mungu amemaliza kabisa kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wetu. Hizi ndizo habari Wayuda wale walizozihitaji, nasi tunazihitaji vilevile.

*Matendo ya sheria*

Kama tulivyosema mbele Waebrania wale walikuwa wamekiri ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu aliyekufa kwa zambi zao. Walikuwa wamekubali ya kwamba wanaweza kuokolewa kwa neema, bila kufanya matendo mema. Halafu walianza kuacha kukutana na Wakristo wengine. Kwa nini? Walikusudi kufungana na dini ya Wayuda tena? Itawezekana namna gani? Wenye kushikamana na dini ile wanajaribu kujipatia wokovu kwa njia ya kufanya kazi njema. Haiwezekani kuchanganya maneno haya mawili. Ao unapokea wokovu kwa imani ao unatumika kazi kujipatia wokovu. Mungu alitaka kuwapa wokovu na raha kwa njia ya imani, lakini Wayuda walikataa kuzipokea. Walishikamana na kazi zao na hawakuingia raha. Basi mwandishi wa barua hii aliogopa ya kwamba labda wengine wa wasomaji wa barua yake walikuwa watu wa namna hii. Kwa sababu hii aliandika: ''*Kwa kuwa ahadi hii ya kuingia katika raha yake ingali pamoja nasi, tuogope basi, mumoja wenu asije ameonekana kukosa kuipata*'' (sh.1). Hasemi hapa juu ya mbingu na hasemi ya kwamba walikosa kweli kuingia raha ile lakini ya kwamba *ilionekana* sawasawa walikosa kuingia. Ilionekana sawasawa wengine katikati yao walikuwa wakitegemea hata sasa matendo yao kushika sheria. Kama ilikuwa kweli, hawakuingia raha ya Mungu lakini walikuwa kwanza wasioamini.

*4:9-13*

*"Basi inabaki raha ya sabato kwa watu wa Mungu."* Maana yake nini? Ndani ya shairi 8 tulisoma kama Yosua angaliwapa Waisraeli raha katika inchi ya Kanana kama Mungu asingalisema juu ya siku nyingine. Raha katika Kanana haikuwa raha ya kweli ya Mungu. Raha ya Mungu ni raha ya roho na tunaweza kuingia ndani yake *sasa* kwa sababu Bwana Yesu alikuja na kumaliza kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wetu. Raha ile "inabaki" kwa sababu kuingia kwa Waisraeli katika inchi ya Kanana hakukutimiza kabisa ahadi ya Mungu kuwapa watu wake raha; kunabaki raha kupita ile. Basi tukae na ange *"isije mutu, hata mumoja aanguke kwa namna ile ile ya kuasi"* (sh.11).

Wakati tunaposoma mashairi haya sharti tujiulize: Nimeingia raha ile? Labda umebatizwa, na unashiriki pamoja na Wakristo wengine kwa Meza ya Bwana, labda unafikia makusanyiko ya kanisa lako kila siku, lakini neno kubwa ndilo hili: Umeingia raha ya Mungu? Uliamini? Ulisema na Mungu siku moja ya kwamba unaacha kutegemea kazi zako njema kujipatia wokovu na unaingia raha yake? Mungu anajua kama ulifanya hivi kwani *"Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni vitupu na kufunuliwa mbele ya macho yake"* (sh.13). Anaona matendo yetu na anajua mawazo ya roho zetu. Anajua kama tukiwa waamini wa kweli.

*4:14-16*

Maneno haya yanaamsha shaka ao woga ndani ya roho yako? Huhitaji kuogopa kwa sababu tuna Kuhani Mukubwa aliyekaa hapa duniani hata kama sasa ameingia mbinguni. Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, anajua uzaifu wetu na anatuita kufika kwake. Tufike basi pasipo woga, hata kama tulianguka, hata kama tulifanya zambi. Ndiyo, tunastahili kuhukumiwa, lakini hata hivi anatuita kufikia kiti cha neema bila woga na kupata rehema kwa zambi tulizokwisha kuzifanya na neema kutusaidia katika mambo magumu yote kufika siku tutakapofikia nyumba ya Baba wake mbinguni. Umutegemee yeye, si nguvu yako mwenyewe, na utaingia raha ya Mungu sasa na hata kwa milele.

# *Kuhani Mukubwa Wetu*
# *Sura 5 na 6*

Kuanza na sura 5 kufika hata sura 8 tunapata mafundisho juu ya Kuhani Mu ubwa wetu, ndiye Bwana Yesu Kristo. Asante kwa sababu tuna Kuhani Mukubwa!

Katika dunia hii kuna hatari nyingi na tuna Mwokozi aliyejitoa kama zabihu kwa zambi zetu na tuna Kuhani Mukubwa anayeweza kutuokoa kabisa (7:25). Tunakumbuka na furaha siku tulipoanza kufahamu ya kwamba zabihu yake musalabani inatosha kutuondolea hukumu ya Mungu. Tunajua vilevile ya kwamba neno litakalotupatisha nguvu kushinda katika dunia hii mbovu ni kujua ya kwamba Kuhani Mukubwa wetu anatuombea na kutusaidia katika mambo yote. Hivi ndani ya sura 5 mwandishi alianza kufundisha juu ya Kuhani Mukubwa wetu, lakini nyuma kidogo aliona ya kwamba wasomaji wake hawakufahamu maneno aliyowaambia kwa sababu walikuwa hawajaendelea zaidi ndani ya maneno ya Mungu. Hivi ilimupasa kuwaelezea maneno mengine ndani ya sura 6. Halafu ndani ya sura 7 aliendelea na mafundisho juu ya Kuhani Mukubwa.

### *KUHANI MUKUBWA, 5:1-6*

Kwanza tuwaze kama kazi ya kuhani mukubwa ni nini. Kazi yake ni kutoa matoleo na zabihu kwa ajili ya zambi. Watu ni wenye zambi na wanahitaji zabihu kuwaondolea zambi zao. Na hata kama wasingalikuwa wenye zambi ingewapasa kuletea Mungu zawadi. Mara nyingine tunafikili inatosha kama zambi zetu zikisamehewa. Kweli tuko wenye roho ngumu, wenye kujifikili wenyewe tu, bila hamu kupendeza Mungu yule aliyetuumba na kutubariki sana!

Kuhani mukubwa ndiye mutu anayeweza kuvumilia na kuhurumia wajinga (sh.2). Ni kazi yake, kama kuhani mukubwa, kufundisha watu Neno la Mungu lakini watu ni polepole kujifunza. Inamupasa kuwaambia neno fulani tena na tena kwa sababu wanasahau mbiombio. Wanafanya maneno yale anayowakataza kuyafanya na wanajiingiza ndani ya matata namna namna. Ni nguvu kwa kuhani kuwavumilia

bila kuwakasirikia, hivi ni lazima kwake kujifunza kuwa na saburi akikumbuka uzaifu wao na akikumbuka ya kwamba yeye mwenyewe ni zaifu vilevile.

Ni vivyo hivyo na Kuhani Mukubwa wetu. Inamupasa kusema neno fulani nasi mara ngapi kwa sababu tunajifunza polepole sana na tunasahau mbiombio! Mara ngapi tunajiingiza ndani ya matata bule tu. Lakini Kuhani Mukubwa wetu ana saburi nyingi na anafahamu uzaifu wetu.

Ona ya kwamba ni lazima kwa makuhani wakubwa kutoa zabihu kwa zambi zao wenyewe vilevile (sh.3), lakini haikuwa hivi kwa Kuhani Mukubwa wetu, ndiye Yesu. Hakuhitaji kamwe kutoa zabihu kwa zambi zake kwa sababu hakuwa na zambi. Hata hivi anafahamu uzaifu wetu, si uzaifu kwa sababu ya zambi tu lakini kwa sababu tuko watu wa dunia. Yeye mwenyewe alijuana na njaa na kiu, alichoka na kupata usingizi. Maneno haya si zambi. Tunashangaa tu kwa sababu alikubali kuwa mutu mwenye mwili zaifu kama miili yetu.

Mashairi 4-6 yanaonyesha namna Bwana Yesu alivyowekwa kuwa Kuhani Mukubwa. Hakuna mutu anayeweza kujikamatia kazi hii ya heshima. Ni Mungu aliyemupa Haruni kazi ya ukuhani. Ilikuwa vivyo hivyo na Kristo. Ni Mungu aliyeweka Yesu kuwa Kuhani Mukubwa wetu. Neno hili ni neno kubwa. Kwa wakati Haruni alipokuwa kuhani mukubwa, Kora, Datani na Abiramu walijaribu kujikamatia kazi ya ukuhani. Datani na Abiramu hawakuwa hata watu wa kabila la Lawi, ndilo kabila la makuhani. Basi Mungu hakukubali neno hili hata kidogo na aliwahukumu mara moja namna asivyohukumu watu mbele: dunia ilifungika na kuwameza nao wangali hai. Soma habari hizi katika Hesabu 16:1-35.

Basi Wakristo waliabudu Yesu na kumuhesabu kama Kuhani Mukubwa wao, lakini Yesu hakuwa mutu wa kabila la Lawi vilevile, lakini wa kabila la Yuda. Hivi ilikuwa sharti kwa mwandishi kuhakikisha ya kwamba neno hili lilikuwa taratibu. Alifanya hivi kwa njia ya kutaja maneno Mungu aliyosema juu ya Mwana wake. Kwanza Mungu alionyesha uungu wake kwa njia ya kusema: *"Wewe ndiwe Mwana wangu. Leo nimekwisha kukuzaa"* (sh.5). Kisha alionyesha ya kwamba yeye ni Kuhani na masemo haya: *"Wewe ni kuhani la milele, kwa mufano kama Melkisedeki alivyokuwa"* (sh.6).

Lakini sharti kuhani afahamu mahitaji ya watu wake ili aweze kuwasaidia. Kwa sababu hii ilipasa Mwana wa Mungu kujuana na taabu na kuumia na mateso yote ya dunia hii. Hata kama alikuwa bila zambi, mwenye nguvu na uhodari, aliumia sana rohoni kwa sababu ya maneno haya yote, na wakati alipoona uchungu na uharibifu zambi zilizoleta duniani alitoa machozi.

*MATESO YAKE, 5:7-8*

Tuwaze kwanza juu ya shamba la Getesemane pahali Bwana Yesu alipoomba Baba wake na uchungu kikombe kiweze kumupitia (Matayo 26:39). Aliomba na roho ya kweli wakati alipoongeza: *"si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka."* Ilimupasa kujifunza kutii kwa njia ya kunywa kikombe hiki, kwa njia ya taabu aliyoipata. Atakuwa Kuhani wa watu walioitwa kwa maisha ya kutii, hivi ilimupasa kujua yeye mwenyewe ya kwamba mara nyingine kutii ni nguvu.

Tuwaze tena juu ya Waebrania wale waliosoma barua hii. Wengine walipotewa nyumba zao na vitu vyao, ndugu zao walifungwa gerezani, walizarauliwa na kuzihakiwa kwa sababu ya imani yao. Wengine wao hawakuweza kupata kazi kwa sababu walikuwa Wakristo. Ndiyo, mara nyingine walitoa machozi kwa sababu ya kuumia na uchungu rohoni. Mara nyingine wewe ulitii Mungu na kutoa machozi kwa sababu ya taabu uliyopata kwa sababu ulitii? Kumbuka ya kwamba Bwana wako alitoa machozi vilevile kwa sababu ya kutii. Hivi usiwe na haya juu ya machozi yako.

Bwana Yesu alisikilizwa kwa sababu aliogopa Mungu (sh.7). Hata alikufa alifufuliwa, ndilo neno watu walilofikili lisilowezekana. Mungu anaheshimu wenye imani na wenye kutii na mwishoni wanashinda. Maneno haya yote yalikamilisha Bwana Yesu, maana yake kumuwezesha kuwa Mutengenezaji wa wokovu wa milele kwa watu wote wenye kumutii.

*YEYE NI BWANA, 5:9-10*

Wokovu ule ndani ya shairi 9 ni wokovu wa namna gani? Ni wokovu wa *milele*. Ni kwa watu gani? Si kwa wale wanaoamini tu lakini kwa wale wanaotii. Maana yake nini? Ni kusema ya kwamba ni sharti kwetu kufanya maneno fulani tuweze kuokolewa? Sivyo, lakini tukitaka kuokolewa, sharti tupokee Kristo kama *Bwana* wetu. Anataka tujitoe muzima kwake aliye Bwana na Mwokozi wetu na kumutii katika maneno yote.

*WATOTO KWA IMANI, 5:11-14*

Waebrania hawa hawakuwa waamini wa sasa, lakini ni kama hawakupata nguvu katika imani. Walibaki watoto tu waliohitaji maziwa, ndiyo mafundisho teketeke toka Kitabu cha Mungu wakati ilipowapasa kuweza kupokea nyama, ndiyo maneno ya ndani ya Neno la Mungu yaliyoweza kuwasaidia vizuri zaidi kwa wakati ule wa mateso na majaribu. Hivi iliwashinda kufahamu maana ya ukuhani wa Melkisedeki kama mufano wa ukuhani wa Kristo. Ilikuwa huzuni kwani maneno haya yangaliweza kutia roho zao nguvu.

Ni vivyo hivyo kila mara. Wakristo wengine hawaweki roho juu ya

kupata nguvu kwa imani na kujuana na Neno la Mungu na halafu hawajui maneno yanayoweza kuwasaidia kwa wakati wa matata. Imani ya Waebrania hawa ilikuwa ikipimwa sana kwa wakati ule na ingaliwasaidia sana kama wangalifahamu kazi ya Kuhani Mukubwa wao.

Unakumbuka saa Petro alipokana Bwana Yesu? Alitoka inje na kutoa machozi na uchungu kwa sababu ya kuanguka kwake. Nini ilimusaidia kwa wakati ule? Kukumbuka ahadi ya Bwana wake, ndiye Kuhani Mukubwa wake: *"Simoni ... nimekuombea, imani yako isipunguke"* (Luka 22:32). Basi Petro alirudi karibu na Mungu, akasimama tena mbele ya mitume wenzake, na mbele ya Bwana, na mbele ya watu, hata nyuma ya kufanya kosa lile kubwa. Ndiyo, Petro alikuwa na faida kwa Mungu tena. Kwa nini? Kwa sababu alijua ya kwamba alikuwa na Kuhani Mukubwa na kama kazi ya Kuhani Mukubwa yule ilikuwa nini.

Lakini Waebrania wale hawakujua maneno haya yaliyoweza kuwasaidia sana kwa wakati ule kwa sababu hawakuweka roho juu ya kuendelea katika imani. Wakati maneno yetu yanapotembea vizuri, tujaribu sana kujaza nia na roho zetu na Neno la Mungu ili kwa wakati wa majaribu na mateso tuweze kusimama imara.

## *KUENDELEA MBELE ... AO KURUDI NYUMA*

*Waebrania 6*

*6:1-6*

Basi Waebrania hawa waliokuwa wakiteswa kwa imani yao wafanye nini? Kulikuwa na maneno mawili tu waliyoweza kuyafanya, ao kwenda mbele hata utimilifu, ao kurudi nyuma. Hakuna njia ya katikati. Hapa tunaona Habari Njema waziwazi. Ndani ya sura 5 tuliona ya kwamba inatupasa kuacha kutegemea kazi zetu njema kama tukitaka kuingia raha ya Mungu. Ndani ya mashairi ya kwanza ya sura 6 tunaona ya kuwa kazi zile ni kazi za kufa na ya kwamba ni lazima kwetu kutubu na kuziacha na kujifunza kuamini kama tukitaka kuokolewa.

Ndani ya shairi 2 tunasoma juu ya mabatizo na kuwekea mikono, na ufufuko toka wafu na hukumu ya milele. Ukisoma kitabu cha Matendo, utaona ya kwamba hizi ndizo kweli kubwa mitume walizohubiri kwa wakati wa mwanzo wa kanisa.

Waebrania waliopokea barua hii walisema waliamini maneno haya yote, lakini matendo yao hayakuonyesha ya kwamba walikuwa wameamini kweli kweli. Basi mwandishi alisema nao maneno kama haya: "Sitajaribu kuwaaminisha ninyi tena. Kuna neno moja tu inalowapasa ninyi kufanya, ndilo kwenda mbele." Wale walioamini kweli wata-

kwenda mbele. Na wale wengine? *''Haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu...''*

Watu wale wasiokwenda mbele ni watu gani? Ni waamini wa kweli waliopoa rohoni na kuacha njia ya mapenzi ya Mungu? Ni kusema watu wa namna hii hawawezi kutubu na kurudi karibu na Mungu? Kama ingalikuwa hivi, kama kazi ya Kuhani Mukubwa wetu ni bule. Sivyo, watu wale si waamini wa kweli.

Sisi sote tumepoa rohoni na kwenda mbali na Mungu tena na tena, lakini kwa sababu ya Kuhani Mukubwa wetu na kazi yake mbele ya Mungu tumetubu na kurudi karibu na Bwana. Basi watu wale ndani ya shairi 6 ni watu gani?

Ndani ya shairi 4 tulisoma ya kwamba ''walikwisha kupewa nuru'' (sh.4). Labda unafikili ya kwamba kupewa nuru na kuokolewa ni neno moja. Sivyo. Tukitaka kuokolewa tunahitaji kupewa nuru, lakini kupewa nuru tu peke yake hakutoshi.

Wayuda waliona maajabu Bwana Yesu aliyoyafanya. Tungefikili walijua kama Yesu ni nani wakati walipomusulibisha. Lakini wakati Petro alipohubiri nyuma ya ufufuko wa Kristo, alisema nao: ''Ninajua ya kuwa *kwa ujinga mulitenda maneno haya*'' (Matendo 3:17). Kwa ujinga? Ndiyo, Roho Mutakatifu alikuwa hajawapa nuru rohoni. Halafu wakati Roho Mutakatifu alipokuja siku ya Pentekote alifungua macho yao nao walifahamu ya kwamba walikuwa wameanguka. Sasa waliona ya kuwa Yesu ni Kristo. Walipewa nuru sasa, lakini wao wote waliamini? Sivyo, wengi wao nyuma ya kupewa nuru ile walifunga macho yao na hawakuamini.

Fikili vilevile juu ya Saulo wa Tarso. Saulo alitesa watu wa Mungu kwa siku nyingi, hata nyuma ya siku ya Pentekote. Unafikili hakujua kama alifanya nini? Alifanya hivi na akili na kusudi. Lakini wakati aliposema juu ya maneno haya nyuma ya kuokolewa, alisema: ''Nilipata rehema kwa sababu *niliyafanya kwa ujinga*'' (1 Timoteo 1:13). Hakufahamu kabisa kabisa maneno aliyokuwa akiyafanya kwa sababu alikuwa hajapewa nuru na Roho Mutakatifu.

*Kupewa nuru bila kuamini*

Wasomaji wa barua hii walikuwa wamepewa nuru. Hatusomi kama waliamini ao sivyo, lakini tunaona ya kwamba *''walionja zawadi ya mbingu na kufanywa washirika wa Roho Mutakatifu''* (sh.4) na tunafikili ''zawadi ya mbingu'' na Roho Mutakatifu ni neno moja. Unakumbuka ya kwamba siku ya Pentekote Petro alitaka kuwapa Waisraeli zawadi hii kama wakitubu na kubatizwa kwa jina la Yesu. Alisema nao waziwazi juu ya zawadi ya Roho Mutakatifu (Matendo 2:38).

Watu wale katika Waebrania 6:4 walifanywa washiriki wa Roho

Mutakatifu. Labda unafikili walikuwa waamini wa kweli. Basi tufikili kwanza juu ya neno hili. Katika sura 2 tulikumbushwa ya kwamba kwa mwanzo Habari Njema ilihubiriwa pamoja na alama na maajabu. Roho Mutakatifu alitumika na uwezo mukubwa katikati yao hata kiwete kwa mulango wa hekalu aliponyeshwa (Matendo 3). Hata kivuli cha Petro kiliponyesha watu wengine (Matendo 5:15). Vivyo hivyo na vitambaa na nguo zilizogusa mwili wa Paulo (Matendo 19:12). Watu wale wote walioponyeshwa kwa njia hizi waliokolewa rohoni vilevile? Maandiko Matakatifu hayasemi hivi. Ndiyo, waliponyeshwa kwa mwili. Uwezo gani uliwaponyesha? Petro alisema wazi ya kwamba ulikuwa uwezo wa Roho Mutakatifu kwa jina la Yesu (Matendo 4:9-10).

*Washiriki wa Roho Mutakatifu*

Watu wale walifanywa washiriki wa Roho Mutakatifu na kwa njia hii walipata faida nyingi kwa miili yao. Lakini kupata faida kwa mwili si sawasawa na kuokolewa rohoni. Inawezekana kwa mutu asiyezaliwa tena kufanya hata maajabu, kutabiri na kutoa pepo wachafu ndani ya watu (Matayo 7:22).

Angalia mashairi 4-6 tena. Tunasoma ya kwamba walionja neno zuri la Mungu, na nguvu za dunia inayokuja. Maana ya kuonja nguvu ya dunia inayokuja ni nini? Haikuwa nguvu kwa Wayuda kufahamu maneno haya. Manabii ya Agano la Kale walitabiri tena na tena juu ya siku ile ya utukufu wakati Masiya atakapokuja. Walisema ya kwamba siku ile watu hawatatoa machozi tena, viwete wataruka, kuumia na magonjwa hayatakuwa tena, na mauti itamezwa na kushindwa. Kwa mia za miaka walitazamia wakati ule. Lilikuwa tumaini lao.

Basi kwa wakati Kristo alipokwisha kurudi mbinguni na Roho Mutakatifu alipokwisha kufika duniani, uwezo wa Roho Mutakatifu ulionekana sana duniani kwa njia ya maajabu yaliyofanyikana. Yalikuwa mufano wa maneno yatakayotokea kwa wakati wa kuja, wakati wa utawala wa Kristo duniani kwa miaka elfu moja. Yalihakikisha kabisa ya kwamba Yesu ni kweli Kristo Masiya! Wayuda walikuwa wamesulibisha Mwana wa Mungu kwa ujinga lakini Mungu hakuwaacha katika ujinga na kwa sababu hii alihakikisha ya kwamba Yesu ni Kristo Mwana wake kwa njia ya maalama haya yaliyofanywa kwa uwezo wa Roho Mutakatifu.

Basi wengine walisema waliamini lakini nyuma yake walirudi tena kwa dini ya Wayuda. Kwa kufanya hivi walisulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili na kumupa haya mbele ya watu. Taifa la Wayuda walisulibisha Yesu mbele na kusema yeye si Mwana wa Mungu, lakini watu hawa walikiri kwa wakati ya kwamba waliamini yeye ni Mwana wa Mungu. Lakini nyuma, kwa njia ya kushikamana na dini ya Wayuda tena ni kama walikubali uuaji wa Yesu. Ni kama walisema ili-

kuwa vizuri kwa Wayuda kumusulibisha. Hawakudanganywa na makuhani mara ile, hawakufanya hivi na ujinga. Walikuwa wamekwisha kupewa nuru na kuona uwezo wa Roho Mutakatifu. Wakijua maneno haya yote walikubali ya kwamba ilikuwa vizuri kwa Wayuda kusulibisha Mwana wa Mungu. Hii ndiyo maana ya kurudi kwa dini ya Wayuda.

Huwezi kushikamana na dini ya Wayuda pamoja na kuamini ya kwamba Yesu ni Mungu. Ukiamini ya kwamba yeye ni Mwana wa Mungu huwezi kushikamana na dini ya Wayuda. Ao unafungana na dini ya Wayuda ao unaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Basi Mungu alisema juu ya watu wale waliorudi tena kwa dini ya Wayuda ya kwamba haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu.

*Kukataa Roho Mutakatifu*

Angalia vizuri kama Mungu anasema nini hapa. Hasemi ya kwamba anakataa kusamehe zambi zao. Sivyo. Lakini anasema ya kwamba nyuma ya kurudi kwa dini ya Wayuda haiwezekani kuwafanyiza kugeuza mafikili yao tena, ndiyo kutubu.

Kwa nini? Kwa sababu kuna neno moja tu linaloweza kuwafanyiza kutubu, ndio uwezo wa Roho Mutakatifu. Nyuma ya kuonja uwezo ule na kuukataa na kusudi, hakuna uwezo mwingine duniani unaotosha kuwafanyiza kutubu.

*6:7-8*

Waza juu ya mufano mwandishi anaoleta hapa. Kuna mashamba mawili. Mvua inanyesha na kutia mashamba mawili maji sawasawa. Shamba moja linaotesha vyakula vizuri, lakini la pili linaotesha miiba na magugu tu. Kwa nini? Nini itafanyiza shamba la pili kuotesha vyakula vizuri? Hakuna kitu.

Ni vivyo hivyo na mioyo ya watu. Roho Mutakatifu anajaribu kufanyiza watu kutubu. Wengine wanatubu kweli na wanazaa matunda mazuri kwa Mungu, lakini wengine wanakataa. Wanazaa miiba na magugu tu. Nini itawaaminisha? Hakuna neno. Wakati Roho Mutakatifu ya Mungu anapokwisha kufungua macho ya mutu naye amefahamu kweli ya Mungu na kusema ya kwamba anaamini, na nyuma yake anarudi nyuma na kukana maneno haya yote, hakuna tumaini tena kwa mutu wa namna hii. Ndiyo, bila shaka Mungu anataka kumwokoa, lakini hata Mungu hana uwezo mukubwa kupita uwezo wa Roho Mutakatifu kumufanya upya tena kwa toba.

Basi wewe musomaji, umefahamu kweli hii ya Mungu na unajua nini inakupasa kufanya? Ninakusihi utii na kuamini, ili usikatae Roho Mutakatifu, na ili hamu ya kuokolewa isikuache kabisa nawe unapotea kwa milele.

*Mambo mazuri zaidi*

*"Lakini, wapenzi ... tumesadiki maneno mazuri zaidi juu yenu, yaliyo na wokovu."* Tunafurahi wakati tunaposoma shairi hili. Hata kama mwandishi aliwasumbukia na kuwaandikia maonyo haya, alifikili rohoni ya kwamba wasomaji wa barua yake walikuwa wameokolewa kweli. Aliweza kuona matunda ndani ya maisha yao yaliyoonyesha ya kwamba walikuwa waamini wa haki.

*"Kwa sababu Mungu si muzalimu hata kusahau kazi yenu, na mapendo muliyoonyesha kwa jina lake, kwa kuwa mumetumikia watakatifu, na hata sasa mungali kuwatumikia."* Unashangaa juu ya shairi hili? Ni kusema tunaokolewa kwa njia ya kazi njema? Mwandishi anasema hapa ya kwamba Mungu si muzalimu kusahau *kazi* zao. Maana yake nini? Mwandishi hakuweza kuona roho ya wasomaji wake lakini aliweza kuona kazi zao, na maneno aliyoyaona yalihakikisha kwake ya kwamba walikuwa waamini wa kweli. Mungu anataka sisi vilevile kuhakikisha kwa njia ya kazi zetu ya kwamba tulimwamini kweli kweli; kama Abrahamu alivyofanya.

## *ABRAHAMU ALIHESABIWA HAKI MBELE YA MUNGU KWA NJIA YA KAZI ZAKE, 6:13-20*

Wakati Abrahamu alipokwisha kutoa mwana wake Isaka juu ya mazabahu, Mungu alimutolea baraka hii, *"Kweli kubariki nitakubariki, na kweli kuongeza nitakuongeza."* Mungu hakusema naye hivi siku ya kwanza Abrahamu alipoamini, ndipo siku imani yake ilipohesabiwa kwake kuwa haki. Sivyo. Alisema na Abrahamu hivi wakati Abrahamu alipokwisha kutoa mwana wake kama sadaka. Tunasoma habari za Abrahamu ndani ya barua ine za Agano Jipya. Ndani ya Waroma na Wagalatia tunasoma juu ya wakati alipoamini Mungu kwanza na ilihesabiwa kwake kuwa haki. Alihesabiwa haki kwa sababu aliamini, si kwa sababu ya kutenda kazi njema. Lakini ndani ya barua ya Yakobo na barua hii kwa Waebrania tunasoma juu ya Abrahamu akitoa Isaka kama sadaka. Waandishi hawa waliandika maneno haya kuonyesha ya kwamba hata tukihesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya imani, inatupasa kwa njia ya kazi zetu kuhakikisha ya kwamba tumeamini kweli, si mbele ya watu tu lakini mbele ya Mungu vilevile.

Wakati Abrahamu alipokwisha kutoa Isaka, Mungu alisema: *"Sasa ninajua..."* Hakusema: "Sasa Sara anajua," ao "Sasa watumishi wako wanajua," lakini "Sasa *ni*najua ya kwamba unaniogopa." Labda unataka kuuliza: "Mungu hakujua mbele ya kwamba Abrahamu alimwamini?" Mungu alijua, kama anavyojua maneno yote, lakini alitaka Abrahamu kuhakikisha neno lenyewe kwa njia ya matendo yake. Anataka sisi kufanya vile.

Ni kama Mungu alisema na Abrahamu: ''Unaniamini kabisa, Abrahamu? Unasema unaniamini. Kama ni hivi, unipe Isaka. Unaniamini *mimi* kutimiza ahadi nilizokutolea ao unategemea Isaka? Unaniamini *mimi tu*? Ninaweza kukuondolea maneno yote mengine?''

Na Abrahamu alijibu maneno kama haya: ''Sijui namna gani utatimiza ahadi zako, Mungu, kama ukikamata Isaka, lakini umukamate tu. Ninakuamini hata hivi.'' Halafu Mungu alisema: ''Sasa ninajua ya kwamba unaniogopa.'' Siku ile Abrahamu alihakikisha kwa njia ya kazi zake maneno aliyokiri na midomo yake.

Ilipasa Waebrania wale kufanya neno namna hii vilevile. Walikuwa wakiamini Mwokozi kweli kweli? Kama ikiwa hivi, labda watapotewa vitu vyao vyote. Mungu alitafuta alama ndani ya maisha yao kuonyesha ya kwamba walikuwa waamini wa kweli. Sharti wewe na mimi tufahamu ya kama tukikiri kuwa waamini wa kweli, Mungu ataacha maneno fulani kutupata nyuma kidogo kupima imani ile kabisa. Wewe ni tayari kwa mapimo namna hii?

Tushukuru Mungu basi kwa Kuhani Mukubwa anayetuombea ili imani yetu isipunguke kwa wakati wa majaribu makali. Kwa sababu ya Kuhani huyu hatuhitaji kuogopa mambo gani yatakayotupata. Hata imani yetu ni ndogo, haitapotea kama ni imani ya kweli. Na Mungu anasema nasi vilevile: ''Kubariki nitakubariki.'' Na kuonyesha ya kwamba mashauri yake hayawezi kubadilika alitoa kiapo vilevile (sh.17). Atatuokoa hata kama matata gani yakitokea. Ametupa sisi nanga kwa roho na Kuhani mukubwa anayetuombea. Nanga ile inakamatana na nguvu na haitachukuliwa kamwe kufika siku tutakapofika mbinguni. Mungu anataka tujue ya kwamba hata imani yetu ikipimwa sana sana, haitaharibika. Tuna nanga kwa roho yenye salama na nguvu na Mungu anataka sisi kuwa na faraja yenye nguvu, sisi tuliokimbilia kushika matumaini yale yanayowekwa mbele yetu.

# *Melkisedeki na Agano Zuri Kupita*
## *Sura 7 na 8*

Ndani ya sura 6 tuliona nini Mungu anayoomba karibu na kila mutu anayesema yeye ni mwamini. Anataka mutu yule kuhakikisha kwa njia ya matendo na mwenendo wake ya kwamba aliamini kweli kweli. Anataka tuhakikishe imani yetu hivi mbele yake mwenyewe na mbele ya watu vilevile.

Lakini tunahuzunishwa kwa sababu tunaanguka tena na tena na mara nyingi mwenendo na matendo yetu hayapatani na maneno tunayosema na midomo yetu. Basi tufarijiwe wakati tunaposoma tena shairi 10 la sura 6. Hata tulianguka jana ao leo, Mungu hasahau matendo yetu mazuri tuliyotenda mbele ya kuanguka kwetu na yaliyohakikisha saa yenyewe ya kwamba tuko waamini wa kweli. Na zaidi ya ile tuna Kuhani Mukubwa kwa milele anayetuombea mbele ya Mungu na atakayetufikisha mbinguni kwa sababu ya kazi kubwa aliyoifanya musalabani kwa kutuokoa.

Halafu ndani ya sura 7 tunasoma juu ya ukubwa na kazi ya Kuhani Mukubwa huyu. Tukumbuke ya kwamba tunahitaji Kuhani Mukubwa anayeweza kutusaidia saa zote na kutuwezesha *kupiga mbio kwa uvumilivu katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu* (12:1).

### *MELKISEDEKI ALIKUWA NANI? 7:1-3*

Kwa mwisho wa sura 6 tuliona ya kwamba Mwokozi wetu amekuwa Kuhani Mukubwa kwa milele *kwa mufano wa Melkisedeki* (sh.20). Basi Melkisedeki huyu ni nani? Maana ya jina lake ni *Mufalme wa haki* na halafu *Mufalme wa salama* (sh.2). (Ona ya kwamba haki ni kwanza; hatuwezi kuwa na salama na Mungu bila haki!) Kuhani wetu Yesu ni mwenye haki yeye mwenyewe na kwa sababu alikufa kwa zambi zetu sisi tunahesabiwa haki vilevile na tuna salama na Mungu.

Hatujui habari nyingine juu ya Melkisedeki. Bila shaka alikuwa na baba na mama lakini Roho Mutakatifu hakutupasha juu yao, hata kama majina ya wazazi wa watu wengine yaliandikwa ndani ya Biblia.

Roho Mutakatifu aliongoza ndani ya maneno yote ya Biblia, maneno yaliyoandikwa na maneno *yasi*yoandikwa. Hakuna habari juu ya *kufa* kwa Melkisedeki vilevile. Hivi ndani ya Kitabu cha Mwanzo Melkisedeki hakuwa na mwanzo wala mwisho na kwa njia hizi yeye ni mufano muzuri sana wa Bwana Yesu Kristo kwani Mwana wa Mungu ni tangu milele na hata milele. Hana mwanzo wala mwisho.

### *MELKISEDEKI ALIKUWA MUKUBWA KUPITA ABRAHAMU, 7:4-10*

Soma habari za Melkisedeki na Abrahamu ndani ya Mwanzo 14. Melkisedeki alikutana na Abrahamu wakati Abrahamu aliporudi nyuma ya vita na alimubariki. Basi kila mara mukubwa anabariki mudogo, hivi tunaona ya kwamba Melkisedeki alikuwa mukubwa kupita Abrahamu. Lakini Abrahamu alikuwa muzazi wa Lawi na Haruni, hivi alikuwa baba wa ukuhani wa Lawi.

Abrahamu alimupa Melkisedeki sehemu moja ya kumi ya vitu vyote alivyovipata vitani. Alifanya hivi kwa sababu alifahamu Melkisedeki alimupita mbali kwa ukubwa. Basi Wayuda wote walitoa kwa wana wa Haruni sehemu moja ya kumi ya mali na vitu walivyovipata na kwa njia hii walikubali kabila la Lawi lilikuwa lenye heshima kupita makabila mengine. Lakini wakati Abrahamu alipotolea Melkisedeki zaka (sehemu moja ya kumi) ilikuwa sawasawa *Lawi* alimutolea Melkisedeki zaka kwa sababu Lawi alikuwa muzao wa Abrahamu. Kwa njia hii tunafahamu ya kwamba ukuhani wa Melkisedeki ulikuwa muzuri kupita ule wa Haruni aliyekuwa mwana wa Lawi. Neno hili ni neno kubwa kwa sababu ukuhani wa Bwana wetu Yesu ni kama ukuhani wa Melkisedeki.

Labda Wayuda wengine walisema: Hata ukuhani wa Kristo ni muzuri kupita ule wa Haruni, ni sharti kwetu kuachana na ukuhani wa Haruni? Hata mutu akinunua vazi jipya, si lazima kwake kutupa vazi lake la zamani. Anapenda vazi lake la zamani vilevile nasi Wayuda tunapenda ukuhani wa Haruni, hata kama ukuhani wa Kristo ni muzuri kupita. Kwa nini hatuwezi kuwa na ukuhani wa Kristo mbingun na ule wa Haruni ndani ya hekalu letu duniani?

Lakini mwandishi wa barua hii alisema neno hili haliwezekani.

### *7:11-19*

#### *Kuhani mukubwa kupita Haruni*

Kama ukuhani wa Lawi ungalikuwa mukamilifu kama ukuhani mwingine usingalihitajiwa (sh.11). Lakini hata ndani ya kitabu cha Zaburi Mungu alisema juu ya kuhani mwingine aliye kwa mufano wa Melkisedeki. Neno hili linaonyesha ya kwamba kwa macho ya Mungu ukuhani wa Lawi haukutosha na haukutimia. Kwa sababu hii ilimu-

pasa kuleta kuhani mwingine. Lakini ukuhani ukibadilika ilipasa sheria kubadilika vilevile (sh.12). Kwa nini?

Ndani ya vitabu vya Kutoka, Walawi na Hesabu tunaona ya kwamba Mungu alitoa sheria juu ya ukuhani wa Haruni na hakuruhusu mutu ye yote kugeuza utaratibu huu. Yeye mwenyewe aliweka Haruni kuwa kuhani mukubwa. Haruni na wana wake tu walikuwa na ruhusa kufanya kazi ya ukuhani.

Lakini sasa Mungu alianza kusema juu ya ukuhani mwingine, kwa mufano wa Melkisedeki. Hivi ni lazima kwa sheria kubadilika kwani sheria ya zamani haikuweza kukubali kuhani aliye kwa mufano wa Melkisedeki, kuhani wa kabila lingine, si wa kabila la Lawi. Kabisa kabisa kuhani huyu mupya hakuwa kuhani kwa sheria ya amri iliyo ya mwili, lakini kwa nguvu za uzima usio na mwisho (sh.16).

Mwandishi wa barua hii alijua maneno haya namna gani? Alijua kwa njia ya Zaburi 110:4: *"Wewe ni kuhani milele, kwa namna ya Melkisedeki."* Ona ya kwamba ni *kwa milele*. Hatakombolewa kamwe na kuhani mwingine kwani uzima wake hautakwisha kamwe.

*Mwisho wa ukuhani wa Lawi*

Kwa sababu hii sheria ya zamani imeondoshwa na maneno yote sheria iliyoagiza ndani ya Agano la Kale juu ya ukuhani wa Lawi si kwa wakati wa sasa. Alikuwa Mungu aliyesimamisha utaratibu wa ukuhani wa Haruni na sasa Mungu mwenyewe alisema ukuhani huu ulikuwa zaifu na haukutosha na hauna faida tena. Ilikuwa nguvu sana kwa Wayuda kukubali neno hili kwa sababu ukuhani wa Haruni ulikuwa wa damani sana kwao. Waliheshimu makuhani yao sana na hawakukumbuka ya kwamba ilishinda Haruni na wana wake kuwaleta karibu na Mungu. Wakati Mungu alipotoa sheria zamani juu ya Mulima Sinai Waisraeli waliagizwa na nguvu kusimama mbali. Siku kubwa ya upatanisho watu walizunguka hema takatifu na woga na *walibaki inje*. Hata kama walikuwa na kuhani mukubwa, kuhani huyu hakuwa na ruhusa kuwaleta karibu na Mungu. Basi tushukuru Mungu kwa sababu sasa tuna ruhusa *kumukaribia* kwa sababu ya Kuhani Mukubwa wetu, ndiye Yesu Kristo.

*7:20-22*

Mashairi haya yanaonyesha ya kwamba ukuhani wa Bwana Yesu unapita ule wa Haruni kwa ukubwa na heshima. Wana wa Haruni walifanyizwa makuhani pasipo kilapo, lakini juu ya Bwana Yesu Mungu mwenyewe alitoa kiapo: *"Bwana ameapa, naye hatageuka, Wewe kuhani hata milele kwa mufano wa Melkisedeki"* (sh.20; Zaburi 110:4).

### *UKUHANI WA KRISTO NI UKUHANI WA MILELE, 7:23-25*

Ukuhani wa Kristo unapita ule wa Haruni kwa njia nyingine vilevile, ndiyo hii: *Kristo ni hai kwa milele.* Kwa ukuhani wa Haruni makuhani walikombolana saa zote. Wakati kuhani mumoja alipokufa kuhani mwingine alimukomboa. Mutu aliweza kufikia hekalu mwaka mumoja na kusaidiwa rohoni na kuhani aliyekuwa pale lakini wakati alipofika tena mwaka wa nyuma labda kuhani wa mbele alikuwa amekufa na kuhani mwingine alikuwa pale asiyejuana na mahitaji yake hata kidogo. Hivi ukuhani ule ulikuwa zaifu na haukuweza kusaidia watu vizuri.

Ukuhani wa Kristo ni namna nyingine kabisa. Kuhani huyu hatakombolewa kamwe na kuhani mwingine. Yeye ni hai milele, naye ni palepale tayari kutusaidia wakati wo wote. Na kwa sababu anakaa milele *''anaweza kuokoa kabisa wao wanaokuja kwake Mungu kwa njia yake; maana yeye ni hai siku zote kuwaombea''* (sh.25).

Tuwaze kwanza juu ya shairi 25. Mbele tuliona ya kwamba Mungu anataka sisi kuhakikisha kwa njia ya mwenendo na matendo yetu ya kwamba tuko waamini wa kweli. Na tena sasa tulisoma ya kwamba hatuhitaji kusumbuka kwani tutaokolewa kabisa. Maneno haya yanapatana namna gani? Tutaokolewa tu hata tukitembea vibaya?

Sivyo. Tutaokolewa kabisa kwa sababu Kristo ni hai siku zote apate kutuombea. Kama ingaliwezekana kwa Kristo kufa ao kuacha kutuombea tungalikwenda mbali na Mungu kwa sababu ya zambi zetu na tungalianguka kama Waisraeli walivyoanguka jangwani. Lakini neno hili haliwezekani. Kwa sababu hii tushukuru Mungu sana kwa Kuhani Mukubwa aliye hai milele kutuombea, na kwa sababu anatuombea tunajua bila shaka ya kwamba atatuokoa kabisa.

### *KRISTO NI KUHANI MUKAMILIFU, 7:26-28*

Kweli sisi watu wa zambi tunahitaji Kuhani namna ya Bwana Yesu aliye mutakatifu kabisa, pasipo zambi hata moja na aliye juu kuliko mbingu. Naye hakuhitaji kutoa zabihu kwa zambi zake mwenyewe kama ilivyopasa makuhani wa Agano la Kale kufanya. Ndiyo, alitoa zabihu, lakini ilikuwa kwa zambi *zetu*, si zambi zake. Aliitoa mara moja tu, si tena na tena kama wana wa Haruni, nasi tunakubaliwa na Mungu kwa sababu ya zabihu ile moja.

Makuhani wengine walikuwa watu wenye uzaifu. Bwana Yesu alijuana na uzaifu wa mwili vilevile wakati alipokuwa hapa lakini sasa kama Kuhani Mukubwa wetu hana uzaifu. Halali usingizi kamwe, hachoki kamwe ndani ya kazi ya kutuombea. Neno la kiapo lilimufanyiza Kuhani, yeye aliye Mwana wa Mungu na aliyekamilika hata milele.

### *NENO KUBWA KATIKA MANENO HAYA, 8:1-3*

Neno kubwa ndani ya maneno yote tunayokwisha kuyasoma, neno kubwa barua hii inalotufundisha ndilo hili: *"Tuna kuhani mukubwa la namna hii, aliyeketi kwa mukono wa kuume wa kiti cha Mwenyezi katika mbingu."*

Ndani ya sura 7 tuliwaza juu ya ukubwa na uzuri wa ukuhani wa Bwana Yesu, na ndani ya sura 8 tunasoma juu ya kazi yake kama Kuhani Mukubwa wetu.

Kazi ya Kuhani Mukubwa wetu inapita ile ya wana wa Haruni kwa njia tatu:

1. Kazi yake inapita kwa sababu ya *pahali anapoifanya.* Makuhani wa Agano la Kale, ndio wana wa Haruni, walifanya kazi yao ndani ya hema takatifu iliyokuwa mufano wa Hema ya kweli Bwana aliyoisimamisha mbinguni.
2. Kazi yake inapita kwa sababu ya *zabihu yake.* Wana wa Haruni walitoa zabihu za nyama. Bwana Yesu alitoa mwili wake mwenyewe kama zabihu. Wao walitoa zabihu nyingi; yeye alihitaji kutoa zabihu moja tu. Iliwapasa kutoa zabihu tena na tena, lakini zabihu yake moja ilimaliza kabisa kazi iliyohitajiwa kwa wokovu wa watu.
3. Kazi ya Kristo ni nzuri kupita kwa sababu *yeye ni Mupatanishi wa agano lililo zuri kupita* agano wana wa Haruni walilolitii.

### *AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA, 8:4-5*

Tuone sasa kama Agano la Kale na Agano Jipya ni mbalimbali kwa njia gani.

Kwanza mwandishi anatukumbusha ya kwamba kwa utaratibu wa agano la kale Bwana Yesu asingaliweza kufanya kazi ya ukuhani kwa sababu alizaliwa katika kabila la Yuda, si katika kabila la Lawi. Mwandishi anatukumbusha neno hili kwa sababu alikuwa akiandika kwa Wayuda waliogeuka Wakristo lakini waliopendana sana na utaratibu wa ukuhani wa Haruni, hekalu lao zuri, mavazi ya mapambo ya makuhani, vivi hivi. Ilikuwa nguvu kwao kuachana na maneno haya yote na kufuata Yesu tu.

Waamini hawa walipenda Bwana Yesu. Waliokolewa kwa sababu ya kazi yake musalabani na kazi yake kama Kuhani Mukubwa wao kwa wakati wa sasa. Basi kama agano la kale lisipomuruhusu kufanya kazi yake kwa sababu hakuwa mwana wa Haruni, ilipasa Wakristo wale kujitenga na agano na dini ile vilevile.

Kwa wakati wa sasa kuna makanisa mengine wasiokubali ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Hawaamini ya kuwa kazi yake musalabani tu inatosha kuokoa watu toka zambi. Ingepasa Wakristo wa kweli kujitenga na makanisa namna hii kama ilivyopasa Wayuda waliogeuka Wakristo kujitenga na dini ya Wayuda.

### *AGANO LA KALE LIMEPITA, 8:6-8*

Unakumbuka agano Mungu alilofanya na Israeli wakati alipowaondosha katika Misri? Aliahidi kuwaleta kwa inchi yenye maziwa na asali kama wakishika agano lake na kufanya maneno yote aliyowaagiza.

Waisraeli waliahidi kutii maagizo yote ya Bwana, lakini iliwashinda kutimiza ahadi yao. Basi Mungu alisema hatatimiza agano lake vilevile kwa sababu Waisraeli hawakutimiza sehemu yao ya agano hili lakini waliasi sheria. Agano lenyewe lilikuwa agano la haki kabisa: Waisraeli wakitii maagizo ya Mungu, Mungu atawaingiza inchini mwa Kanana, lakini wakati walipoasi Mungu alikataa kuwaleta inchini.

### *AGANO JIPYA LILILO NAMNA NYINGINE, 8:9-11*

Soma shairi 9 tena. Kama Waisraeli wasipotimiza sehemu yao ya agano la Mungu, Mungu hakutimiza sehemu yake vilevile. Ni kwa sababu hii Mungu alikomboa agano la kale na agano jipya. Basi agano jipya ni namna nyingine kwa njia gani?

Kwanza Mungu anatia amri zake ndani ya nia zetu na kuziandika ndani ya mioyo yetu na halafu tunazipenda na kuzitii na furaha. Vilevile anaahidi kuwa Mungu wetu na kuwa karibu sana nasi hata hatuhitaji mutu kutufundisha kumujua kwa sababu tunaweza kumukaribia na kujuana naye kabisa kama mutoto anavyojua baba wake.

Labda unawaza ndani ya roho yako, "Ndiyo, tangu nilipookolewa ninapenda mapenzi ya Mungu na ninawaza sana juu ya maneno yake. Kweli mawazo yangu sasa ni namna nyingine na mawazo niliyokuwa nayo mbele ya kuokolewa. Mbele sikutaka kufanya mengine ya maneno Mungu aliyoagiza lakini sasa ninafurahi kuyafanya. Lakini hata hivi sifanyi mapenzi ya Mungu kila mara." Ni vivyo ndani ya maisha yetu sisi sote. Kama Paulo tunapenda maagizo ya Mungu lakini hata tukitaka kutenda yaliyo mema tunaanguka tena na tena (Waroma 7:18)!

### *8:12-13*

Halafu nini inatokea wakati tunapoanguka hata kama tulitaka kufanya mema? Maneno yetu yanaharibika pia saa yenyewe?

Sivyo, hata kidogo, kwani katika agano jipya Bwana alisema: "*Ni-*

*tasamehe maovu yao na zambi zao sitazikumbuka tena.*" Asante kwa Mungu kwa *namna* agano hili lilivyoandikwa. Mungu hakusema *kwanza* ya kwamba atasahau zambi zetu, na *nyuma yake* ya kwamba ataandika amri zake katika nia zetu. Sivyo; *kwanza* aliandika amri zake ndani ya mioyo yetu na nia zetu. Halafu tukianguka hata hivi atatukataa kama alivyofanya na Waisraeli? Sivyo; agano hili jipya ni namna nyingine: "*Nitawasamehe maovu yao, na zambi zao sitazikumbuka tena.*" Hatazikumbuka tena kamwe!

Basi, ndugu yangu Mukristo, unafikili nini wakati unaposoma maneno haya? Wakati unapowaza juu ya neema kubwa ya Mungu kwako na juu ya Kuhani huyu aliyekufa na atakayekuokoa kabisa, unapata hamu kutenda maovu na kutembea katika zambi namna zote? Ukiwa Mukristo wa kweli hutapenda kufanya hivi. Utataka kupendeza Bwana tu siku zote ukisukumwa na mapendo na roho ya asante. Na utaomba Kuhani Mukubwa wako kukusaidia siku zote usifanye zambi zitakazomuhuzunisha.

# *Kuhani Mbinguni*
# *Sura 9*

Tumeona ya kwamba ukuhani wa Kristo ulikuwa kwa mufano wa Melkisedeki na kwa sababu hii ulipita ukuhani wa Haruni kwa njia tatu:

1. Kuna agano jipya sasa lililo zuri kupita agano la zamani Haruni alilolitii.
2. Pahali Kristo anapofanya kazi yake ya kuhani ni pahali pazuri kupita. Haruni alifanya kazi yenyewe ndani ya hema iliyofanywa na watu, lakini Mwokozi wetu anafanya kazi yake ndani ya hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, iliyosimamishwa na Bwana, si na watu (8:2).
3. Kwa maneno ya zabihu ilipasa makuhani ya Agano la Kale kutoa zabihu nyingi, lakini zabihu moja Bwana Yesu aliyoitoa itatosha kwa milele.

Ndani ya sura 8 tuliwaza juu ya agano jipya. Sasa tusawanishe pahali Bwana Yesu anapofanya kazi ya ukuhani na pahali Haruni alipoifanya.

Kila agano, agano la zamani na agano jipya, lina utaratibu fulani kwa maneno ya kuabudu. Sehemu ya kwanza ya sura 9 inaeleza utaratibu wa kuabudu kwa wakati wa hema Waisraeli waliyoisimamisha na hata kufika wakati mwandishi alipokuwa akiandika barua hii kwa Waebrania.

### *HEMA YA AGANO LA KALE, 9:1-5*

Soma mashairi haya polepole. Maana ya "hema ya kwanza" (sh.2) ni nini? Kulikuwa na hema mbili? Sivyo, kulikuwa na hema moja tu iliyokuwa na vyumba viwili ndani yake. Wakati kuhani alipoingia hema kwa pazia la kwanza toka kiwanja kilichozunguka hema, aliingia ndani ya chumba kinachoitwa hapa "hema ya kwanza." Chumba hiki kilikuwa na taa, meza, na mikate ya onyesho na kiliitwa Pahali Patakatifu. Halafu akipita toka chumba cha kwanza kwa pazia la pili aliingia ndani ya chumba cha pili kilichoitwa Pahali Patakatifu pa patakatifu, na alikuta pale sanduku ya agano. Pazia tu liligawa hema

ya kwanza na hema ya pili. Wakati tunaposoma juu ya "pazia" ndani ya Agano Jipya, ni zaidi pazia hili la pili, si pazia kwa lango la hema.

*VYUMBA VIWILI, 9:6-7*

Makuhani wote waliingia siku zote ndani ya chumba cha kwanza, ndicho hema ya kwanza kufanya kazi yao kwa Mungu. Lakini kuhani mukubwa tu aliingia ndani ya hema ya pili, ndiyo Pahali Patakatifu pa patakatifu. Alikwenda mara moja tu kila mwaka pamoja na damu ya zabihu aliyoitoa kwa ajili yake mwenyewe na kwa zambi za ujinga za watu.

*HEMA YA KWANZA, 9:8-10*

Basi kwa nini hema ilikuwa na vyumba viwili? Maana yake nini? Roho Mutakatifu anatupasha sasa ya kuwa *"Njia ya kuingia Pahali Patakatifu haijafungika wazi bado, hema ya kwanza ilipokuwa ingali kusimama."* Maana yake nini? Tukumbuke ya kuwa wakati mwandishi wa barua hii alipoandika juu ya "hema ya kwanza" alifikili juu ya chumba cha kwanza ndani ya hema. Halafu Roho Mutakatifu anaonyesha ya kwamba wakati chumba hiki cha kwanza kilipokuwa kingali, njia ya kuingia chumba cha pili, ndicho Pahali Patakatifu pa patakatifu ilikuwa haijafunguka wazi bado.

Usiache maneno haya kukufazaisha. Kumbuka ya kwamba kulikuwa na pazia ndani ya hema. Pazia hili liligawa hema kwa vyumba viwili na kuzuiza watu wasiingie Pahali Patakatifu pa patakatifu. Bila pazia hili hema ingalikuwa chumba kimoja tu na njia kufikia Pahali Patakatifu pa patakatifu ingalikuwa wazi. Lakini pazia lilipokuwa lingali pale na kugawa hema kwa nyumba viwili, njia ya kuingia Pahali Patakatifu pa patakatifu ilikuwa haijafunguka wazi bado.

Nyuma kidogo tutasawanisha hema ile na hema ya kweli pahali tunapoweza kuabudu kwa wakati wa sasa. Hakuna vyumba viwili sasa. Njia ni wazi kwa sisi kuingia Pahali Patakatifu pa patakatifu. Hakuna pazia sasa linalotenga Mungu na watu wake kwa maneno ya roho (lakini kwa njia nyingine pazia ni vile - ona 6:19-20 tena).

*Kazi ya pazia ilikuwa nini?*

Tuwaze tena juu ya hema kwa wakati wa Agano la Kale na tuulize: Pazia lilihitajiwa kwa sababu gani? Kwa nini ilikuwa lazima kuzuiza watu wasiingie Pahali Patakatifu pa patakatifu? Utaona jibu kwa ulizo hili ndani ya mashairi 9 na 10. Zabihu watu walizotoa kwa wakati ule hazikuweza kukamilisha wenye kuabudu kwa maneno ya zamiri zao. Wakati mutu alipofanya zambi alileta zabihu yake kwa hema, damu ya zabihu ilimwangika, na halafu kuhani alikuwa na amri kusema ya kwamba zambi hii ilikuwa imesamehewa (ona Walawi 4:31). Lakini

hata mutu yule alisamehewa zambi hii, si kusema maneno yake yalitengenea kwa milele mbele ya Mungu. Akifanya zambi nyingine kesho yake ilimupasa kutoa zabihu nyingine.

Kwa maneno ya zamiri zao kwa wakati wa Agano la Kale, hata waamini hawakukamilishwa kamwe. Kwa sababu hawakuwa wakamilifu hawakuwa na ruhusa kufika mbele ya Mungu. Lakini Mungu alitaka watu wake kufika karibu naye, hata kwa wakati ule, hata kama zabihu zao hazikutosha kabisa, hivi kwa rehema yake alisema maneno kama haya: ''Muweke pazia ndani ya makao yangu kwa kuficha pahali ninapokaa. Halafu watu wangu wataweza kufika karibu nami hata kama ikiwapasa kubaki kwa ngambo nyingine ya pazia.''

Hivi kwa wakati ule makuhani waliweza kuingia chumba cha kwanza na kutumikia Mungu kwa meza na kinara na kutoa uvumba juu ya mazabahu hata kama zamiri zao hazikukamilishwa wakati wo wote na hata kama zabihu zao hazikutosha kabisa. Maneno yale yalikuwa mazuri tu, lakini tusifu Mungu kwa sababu kwa wakati wa sasa ni mazuri zaidi!

*9:11-15*

*Mbingu*

Ndani ya mashairi 11-15 kuna masawanisho ya kushangaza. Kristo, Kuhani Mukubwa wetu, anafanya kazi yake ndani ya hema isiyo ya dunia hii na isiyofanywa na vitu vya dunia. Hema hii ni kubwa kupita na kamilifu kupita hema ya dunia. Ni ya mbingu, karibu na Mungu. Wakati tunapoisawanisha na hema ya wakati wa Agano la Kale, mapambo ya hema ya Haruni yanaonekana kama kitu bule.

Kristo hakuingia ndani ya hema ile na damu ya nyama lakini na damu yake mwenyewe. Hakuhitaji kuingia kila mwaka kama kuhani mukubwa wa Waisraeli, lakini aliingia mara moja tu kwa sababu damu aliyoimwanga ilitupatia ukombozi ulio wa milele. Kwa sababu ya zabihu ile njia kuingia Pahali Patakatifu pa patakatifu imefunguliwa kwa milele. Hatuhitaji kuleta zabihu nyingine kila mara tunapokaribia Pahali Patakatifu pa patakatifu na tunaweza kufika tena na tena, kwa wakati wo wote, kwa sababu zabihu ile moja inatosha kila mara kutuleta karibu na Mungu.

Kwa wakati wa Agano la Kale watu walifikia jengo lililofanywa na mbao na mawe na zahabu na feza, na zabihu zao ziliweza kusafisha miili yao (9:13). Sasa tunakaribia hema iliyo ya mbingu na tunakaribia Mungu aliye Roho. Hatuhitaji zabihu kusafisha miili yetu lakini zamiri zetu ili tuweze kukaribia Mungu bila woga. Basi kama zabihu zilizotolewa kwa wakati wa Agano la Kale ziliweza kusafisha miili ya watu, kuzidi sana damu ya Kristo, aliyejitoa mwenyewe kwa Mungu kwa njia ya Roho ya milele, itasafisha zamiri zetu.

*Kristo Zabihu yetu*

Mungu ni Roho nasi tunaweza kumukaribia kwa njia ya roho tu. Lakini tulikuwa wafu katika roho kwa sababu ya makosa na zambi zetu (Waefeso 2:1). Hatukuwa na upatano na Mungu kwa sababu tulikuwa wafu katika roho. Basi Kristo alijitoa kama zabihu musalabani kwa Roho ya milele kwa kufungua njia tena kwa sisi. Faida ya zabihu hii kwa sisi ni hata milele!

Zabihu zilizotolewa wakati wa Agano la Kale, zaidi ile ya kinda la ngombe, ziliweza kusafisha mwili. Kwa wakati ule mutu akigusa kitumba ao maiti, alihesabiwa kuwa muchafu. Hakuweza kuingia kambi ya Waisraeli na hakuweza kukaribia hema pahali Mungu alipokaa. Kwa njia hii Mungu alikuwa akifundisha watu uchafu wa mauti.

Shairi 14 linatupasha ya kwamba Mungu ni hai. Ndani yake hakuna uharibifu wala kuoza. Basi zambi iliingiza mauti ndani ya dunia hii Mungu aliyoiumba, na pamoja na mauti uharibifu na kuoza. Mungu alichukia maneno haya na kwa sababu hii hakukubali mutu aliyegusa kitu kilichokufa kumukaribia. Lakini mutu namna hii aliweza kusafishwa na majivu ya kinda la ngombe. Soma juu ya maneno haya katika Hesabu 19:2-19.

*Kazi zilizokufa*

Sisi watu tumechafuwa kwa njia ya mauti. Miili yetu inakufa na wakati tusipookolewa bado matendo yetu yalikuwa matendo ya kufa kwa sababu tulikuwa wafu kwa macho ya Mungu kwa wakati ule. Wakati mwandishi alipoandika juu ya matendo ya kufa hakufikili juu ya zambi kubwa kama uzini ao ulevi tu lakini vilevile juu ya maneno mengi watu wanayofanya kwa njia ya dini, maneno yanayoonekana mazuri kwa macho ya watu. Ni matendo ya kufa kwa macho ya Mungu aliye hai kwa sababu wale wanaoyatenda ni wenye zamiri zisizosafishwa kwa damu ya Yesu.

Hata nyuma ya kuokolewa inawezekana kwa utumishi wetu kuwa kitu cha kufa kama tukifanya kazi ya Mungu kwa nguvu yetu bila kuongozwa na Roho Mutakatifu. Sisi vilevile tunahitaji kusafishwa. Asante kwa sababu damu ya Kristo itasafisha zamiri zetu tupate kutumikia Mungu aliye hai (9:14).

Tuone sasa kama tunasafishwa kwa sababu gani. Ni kusudi tuweze kutumikia Mungu aliye hai. Kuhani Mukubwa wetu ameingia ndani ya hema ya mbingu nasi tunaitwa vilevile kukaribia Mungu na kumutumikia kama makuhani kwa maneno ya roho. Tunafanya hivi wakati na wakati saa tunapokutana pamoja na Wakristo wengine kuabudu Mungu. Hata miili yetu ikikutana hapa duniani, kwa njia ya roho zetu tunaweza kuingia Pahali Patakatifu mbinguni. Lakini tunafahamu tu ya kwamba tumefanya zambi, na kuchafuwa na maneno ya dunia yanayotuzunguka, na tunajua ya kwamba hatuwezi kutumikia Mungu

aliye hai vizuri kama zamiri zetu zikichafuwa. Basi tufanye nini?

*Zamiri iliyotakaswa*

Mara nyingine tunafikia kusanyiko la kanisa na tumefanya zambi inayochokoza zamiri yetu. Kama tulikosea Mukristo mwingine, sharti tutengeneze neno hili mbele ya kufikia meza ya Bwana. Lakini tufanye nini kama zambi yetu isipogusa mutu mwingine ila Mungu tu? Inatupasa kungoja kwanza siku fulani mbele ya kukubaliwa na Mungu tena?

Sivyo, damu ya Kristo inatosha kabisa kusafisha zamiri zetu mara moja. Tukikiri zambi zetu mbele ya Mungu na roho ya kweli tunaweza kumukaribia tena mara moja sawasawa hatukufanya zambi.

Labda Wakristo waliosoma barua hii walishangaa wakati waliposoma ya kwamba zabihu za nyama wazazi wao walizotolea Mungu hazikutosha. Bila shaka waliuliza kama wazazi wao walioishi mbele ya wakati wa Agano Jipya walipotea. Wazazi wao walitoa zabihu za nyama kama Mungu alivyowaagiza kufanya. Basi kama zabihu hizi zilisafisha miili yao tu, walikuwa wamepotea wote? Sivyo, hata kidogo. Soma shairi 15 polepole. Zabihu ya Kristo inatosha kwa zambi watu walizofanya zamani na kuzifunika na damu ya zabihu zao za nyama; inatosha kwa wakati wa sasa na hata kwa milele. Inatosha kwa zambi za Musa na Yosua, kwa zile za Paulo na Petro, kwa zambi zako na zangu, na kwa zambi za watu wote watakaookolewa kwa wakati wa kuja!

## *AGANO, NA AGANO LA URITI, 9:16-23*

Halafu mwandishi alianza kufundisha juu ya maagano na maagano ya uriti. Alionyesha ya kwamba agano la uriti halina faida wakati yule aliyelifanya ni kwanza hai. Kwa maneno ya sheria agano ni mbalimbali na agano la uriti. Watu wawili ao makundi mawili ya watu wanahitajiwa kufanya agano, lakini mutu mumoja tu anafanya agano la uriti na agano lile halina faida kufika siku ya kufa kwa mutu huyu.

Zamani Mungu alifanya agano na watu kwa Mulima Sinai, ndilo agano la kale. Damu ya zabihu ilihitajiwa kwa agano hili. Kristo alifanya agano vilevile kwa njia ya kufa kwake. Agano Kristo alilolifanya ni agano la uriti naye alilifanya peke yake. Hatuhitaji kufanya kitu kupata faida ya agano hili ila kutubu zambi zetu na kuamini.

Waisraeli waliahidi kutii maneno yote Mungu aliyoyaagiza ndani ya agano la kale (Kutoka 19:8), lakini iliwashinda kabisa kutimiza ahadi hii. Kwa rehema tu Mungu hakuondoka katikati yao, kwa sababu ya zabihu za damu walizozitoa. Hema na vitu vyote vya kazi ya makuhani ndani ya hema vilinyunyiziwa damu kuvisafisha. Ndiyo, ''*katika torati karibu vitu vyote vinasafishwa kwa damu.*'' Lakini shairi

23 linaonyesha ya kwamba hata kama ilipasa vitu hivi vilivyokuwa mifano ya mambo ya mbingu kusafishwa hivyo, mambo ya mbingu yenyewe yalipaswa kusafishwa na zabihu nzuri zaidi.

*9:24-28*

*Hema ya kweli*

Kwa mwisho wa sura hii tunawaza tena juu ya hema ya Agano la Kale na vyumba vyake viwili, na hema nzuri zaidi pahali sisi tunapoweza kutumikia Mungu pamoja na Kuhani Mukubwa wetu. Kwa wakati wa zamani watu walihitaji kusafishwa na damu, na hema ilihitaji kusafishwa vilevile. Maneno haya yalifanywa mara moja kila mwaka kwa siku ya Upatanisho, ona Walawi 16. Tunaona kusudi la maneno haya ndani ya shairi 16 la sura ile. Ndiyo, watu walihitaji kusafishwa toka zambi zao, na kwa sababu walikaa karibu na hema ya Mungu, walichafua hema vilevile, ndipo pahali Mungu alipokaa. Kulikuwa na njia moja tu kwaye kukaa katikati yao, ndiyo kusafisha watu kila mwaka na hema na vitu makuhani walivyotumika navyo.

Watu hawakufanya zambi na kusudi kila mara. Kusudi kubwa moja la siku kubwa ya upatanisho lilikuwa kusafisha watu toka zambi zao *za ujinga*. Kuhani mukubwa aliingia Pahali Patakatifu pa patakatifu mara moja kila mwaka, pamoja na damu (9:7). Alitoa damu hii kwa yeye mwenyewe na kwa zambi za ujinga za watu. Kila mara mutu fulani alipofahamu ya kwamba alikuwa amefanya zambi, ilimupasa yeye mwenyewe kutoa zabihu. Lakini Waisraeli walifanya zambi nyingi nyingine vilevile, bila kujua. Ni vivyo hivyo ndani ya maisha yetu. Basi zambi namna hii zinahitaji zabihu vilevile.

Halafu wakati kuhani mukubwa alipokwisha kufanya upatanisho kwa watu, na hema ilipokwisha kusafishwa vilevile, Mungu alikubali kukaa pamoja na watu wake wenye zambi kwa mwaka mumoja mungine.

*Mbingu zenyewe*

Soma Waebrania 9:24-27 tena polepole. Mashairi haya yanatukumbusha tena siku kubwa ya upatanisho. Zabihu ilichinjwa katika kiwanja cha hema mbele ya kuhani mukubwa. Halafu kuhani mukubwa aliingia chumba cha kwanza cha hema na kupita kwa pazia kwa chumba cha pili na kutokea mbele ya Mungu kwa ajili ya watu. Watu wote walikuwa wakingoja inje kufika saa alipotoka tena katikati yao. Maneno haya yalikuwa mufano wa Kristo aliyetokea *mara moja tu* (si kila mwaka) na kuondoa zambi kwa njia ya kujitoa mwenyewe.

Kisha alifufuka toka wafu na kwa sababu ya faida ya damu yake mwenyewe alirudi mbinguni na anatokea sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu. Sasahivi yeye ni pale katika Pahali Patakatifu. Miaka 1900

na zaidi imepita tangu aliporudi mbinguni na kwa miaka ile yote amekubaliwa na Mungu katika Pahali Patakatifu. Angaliweza kuingia pale bila zabihu kama angaliingia kwa yeye mwenyewe tu. Lakini hakuingia kwa ajili yake mwenyewe lakini kwa ajili yetu. Hakutaka kutengwa nasi, hivi anatokea sasa mbele ya Mungu kwa ajili yetu. Hata kama sisi hatuwezi kutokea pale kwanza katika mwili, tunaweza kufika hata sasa kwa njia ya roho.

Halafu nyuma kidogo Bwana atakuja tena. Ataonekana mara ya pili, si tena kwa zambi, lakini kuokoa wale wanaomungojea kwa wokovu (sh.28).

Unaona maneno haya mawili ''kwa wokovu''? Maana yao nini? Bwana ametuokoa mbele toka zambi zetu na anakaa kutuokoa toka kuanguka kwetu siku zote. Halafu wakati atakapokuja tena ataokoa miili yetu ya uzaifu na kufa na uharibifu, isiyostahili kufika karibu na Mungu kwa hali yao ya sasa.

Mambo haya yote ni ajabu kubwa kabisa. Kwa roho tunaweza kukaribia Mungu hata sasa, lakini tunangojea Kuhani Mukubwa wetu kuja kuokoa miili yetu vilevile. Atabadilisha miili yetu ya haya ipate kufanana na mwili wake wa utukufu (Wafilipi 3:21). Siku ile Kristo atatuleta mbele ya Mungu na tutakuwa tumeokolewa pia, roho, nafsi na mwili. Itakuwa siku ya furaha kubwa!

*Kwami, Mwokozi wangu anaishi mbingu,*
*Neema, rehema vile analeta kwangu.*
*Hanizarau mimi na uzaifu wangu,*
*Mapendo yake kwangu ni matamu sana.*

*Sasa anatukuzwa kwa kiti cha Baba,*
*Na toka kule mbingu anatutazama.*
*Anatupenda sana na sisi tutakwenda*
*Kwake kumutukuza hata kwa milele.*

(Nyimbo za Kuabudu No. 104)

# *Zabihu Inayotosha*

## *Sura 10*

Ndani ya sura hii tutasawanisha ukuhani wa Bwana Yesu na ule wa Haruni na tutaona tena ya kwamba ule wa Yesu ni muzuri zaidi.

Tukumbuke ya kuwa barua hii iliandikwa kwa Wayuda waliokuwa wameamini Bwana Yesu Kristo. Kwa miaka mingi walikuwa wametolea Mungu zabihu za nyama kama wazazi wao walivyofanya mbele yao. Hawakuweza kukubali mbio mbio kuacha kuzitoa kwa sababu Mungu mwenyewe ndani ya Kitabu chake alikuwa amewaagiza kuzitoa.

Kwa wakati ule sehemu kubwa ya Agano Jipya ilikuwa imeandikwa lakini bila shaka walikuwa na vitabu vichache tu. Vilevile hawakuheshimu Agano Jipya mara moja kwa kipimo walichoheshimu Agano la Kale. Basi ilipasa mwandishi kuwafahamisha ya kwamba zabihu zao za nyama hazikutosha hata kidogo na ya kwamba kazi ya zabihu hizi ilikwisha. Atawafahamisha namna gani?

*HAKUNA UKAMILIFU NDANI YA AGANO LA KALE, 10:1-6*

Kwanza mwandishi aliwakumbusha ya kwamba iliwapasa kutoa zabihu zao tena na tena, mwaka kwa mwaka. Kwa nini? Kwa sababu zabihu hizi hazikuweza kukamilisha wenye kukaribia Mungu. Ilikuwa hivi kwa sababu torati ni kivuli tu cha yale mema yatakayokuja (sh.1).

Halafu ndani ya kitabu cha Zaburi tunasikia Mungu yeye mwenyewe, na Bwana Yesu akitabiri. Soma mashairi 5-7 pamoja na Zaburi 40:6-8. Mashairi haya yanaonyesha ya kwamba Mungu hakufurahi tena juu ya zabihu zile za nyama. Basi Wayuda waliamini ya kwamba kitabu cha Walawi ni Neno la Mungu na kitabu cha Zaburi vilevile. Halafu kila mara maneno yaliyoandikwa nyuma yanakomboa maneno yaliyoandikwa mbele, hivi pale pale ndani ya Zaburi, zilizoandikwa nyuma ya Walawi, tunaona mawazo ya mwisho ya Mungu juu ya maneno ya zabihu za nyama. *"Zabihu na sadaka hukutaka."* Hata kama Mungu aliagiza watu wake mbele kutoa zabihu hizi, kwa miaka ile yote hazikuweza kutuliza roho yake. Hakuweka roho juu yao tena. Zabihu namna nyingine ilihitajiwa na ndani ya shairi 5 tunaona masemo ya Bwana Yesu: *"Mwili uliniwekea tayari."* Si neno kama

mwandishi wa zaburi hii alikuwa nani, Wayuda walifahamu ya kwamba haya yalikuwa masemo ya Masiya.

*10:7-10*

*Mapenzi ya Mungu*

Ndani ya mashairi 8 na 9 tunaona ya kwamba kwanza Mungu hakufurahi juu ya zabihu na sadaka za Agano la Kale, kisha Bwana Yesu alisema: *"Tazama, nimekuja nifanye mapenzi yako."* Ndiyo, watu wale wa zamani wali*jaribu* kupendeza Mungu, lakini hawakuweza. Zabihu zao hazikuhitajiwa tena wakati Kristo alipokuja kutimiza mapenzi ya Mungu kabisa. Ona ya kwamba zabihu yake ilikuwa namna nyingine kabisa.

*Mwili wa Kristo*

Zabihu Waisraeli walizozitoa katika Agano la Kale zilikuwa miili na damu za nyama, nazo hazikutosha kabisa. Wakati Kristo alipokuja kutoa zabihu yake, zabihu hii ilikuwa mwili wa mutu uliowekwa tayari (sh.5). Ndani ya sura 9 Roho Mutakatifu alisema juu ya kazi ya Kristo ya kwamba "kwa Roho ya milele" alijitoa mwenyewe kwa Mungu (9:14). Roho zetu zilizokufa zilihitaji kupatanishwa na Mungu aliye Roho na kwa kusudi hili Kristo alijitoa kwa Roho ya milele.

Lakini ndani ya sura 10 tunawaza juu ya Kristo akitoa *mwili* wake, mwili aliokuwa nao hapa duniani. Kuna vitu viwili juu ya meza wakati tunapoizunguka siku ya kwanza ya juma kukumbuka Bwana: kuna mukate na mvinyo. Juu ya mukate Bwana Yesu alisema: *"Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu"* (Luka 22:19). Ndiyo, mukate ule ni mufano wa mwili wake ulioumia juu ya musalaba. Tunawaza mara nyingi juu ya damu ya Kristo iliyotusafisha toka zambi zetu lakini tusisahau ya kwamba alitoa mwili wake vilevile. Tumepata utakaso kwa sababu ya kutolewa kwa *mwili* wa Yesu Kristo (10:10). Ona ya kwamba mwandishi hakusema tumetakaswa kwa sababu ya kutolewa kwa Yesu Kristo. Neno hili ni kweli vilevile, lakini alisema wazi: "tumepata utakaso kwa kutolewa *mwili* wa Yesu Kristo mara moja."

Bwana Yesu alisema: Tazama, nimekuja nifanye mapenzi yako, Mungu." Basi mapenzi ya Mungu yalikuwa kwa Mwana wake kutoa mwili wake naye Mwana alifanya hivi. Neno alilofanya lilikuwa kamilifu na kwa njia yake amekamilisha hata milele wenye kutakaswa (sh.14). Ajabu kubwa!

*10:11-14*

*Mara moja tu*

Ona ya kwamba zabihu hii ilitolewa *mara moja* tu. Mara ile moja inatosha kwa milele (sh.12).

Makuhani ndani ya hema ya zamani walisumbuka kila siku na kazi ya kutoa zabihu, lakini zabihu hizi hazikuweza kabisa kuondoa zambi. Yalikuwa maneno ya kuchokesha kabisa. Lakini Bwana Yesu "wakati alipokwisha kutoa zabihu moja kwa zambi hata milele," aliketi kwani kazi yenyewe ilikwisha, ilitimia! Tusifu Mwokozi wetu kwa sababu zambi zetu *zote* zimesamehewa, zile tulizozifanya zamani, zile tulizozifanya leo, na zile tutakazozifanya kwa wakati wa kuja.

Unasema watu wakiamini neno hili watazidi kutembea katika zambi? Tukumbuke basi ya kwamba Mungu ni Baba wetu naye anaazibu watoto wake wakati wanapoasi maagizo yake. Kila siku inatupasa kukiri zambi zetu mbele yake na mbele ya watu tuliowakosea. Zambi hizi zitasamehewa kama tukisamehe wenzetu waliotukosea sisi. Kama tusipowasamehe, hatutasamehewa vilevile lakini tutaazibiwa na Baba. Haya ni maneno katikati ya Baba Mungu na watoto wake, lakini kwa sababu ya kazi ya Kristo musalabani kwa ajili yetu sisi ni safi kwa macho ya Mungu kwa sababu tuko ndani ya Mwana wake. Tunaweza kumukaribia bila woga kwa sababu hatakumbuka zambi zetu tena kamwe (sh.17).

Soma shairi 14 tena polepole. Ndiyo, kwa macho ya Mungu tumekamilishwa kwa milele. Halafu maana ya "wenye kutakaswa" ni nini? Ni kusema kazi ya kututakasa haijakwisha bado. Tungali kupata nguvu na kuendelea katika imani, tungali tukitakaswa. Lakini hata kama mwenendo wetu haujatimia bado, hata kama tukianguka tena na tena, tumekamilishwa hata sasa kwa macho ya Mungu!

### *ROHO MUTAKATIFU NI MUSHUHUDA, 10:15-18*

Ona ushuhuda wa Roho Mutakatifu ndani ya mashairi 15-17. Kwanza Mungu anatia sheria zake ndani ya mioyo yetu na nia zetu hata tunafurahi kuzifanya na kuwaza juu yao, lakini hata hivi tabia yetu ya zambi inatukokota kwa njia mbaya na tunafanya zambi tena na tena. Kwa sababu hii tunasoma ndani ya shairi 17, "*Zambi zao na maovu yao sitayakumbuka tena.*" Kwa agano jipya zambi zetu zimesamehewa kabisa kabisa hata Mungu mwenyewe hatazikumbuka tena kamwe. Kwa sababu hii tunasoma ndani ya shairi 18, "*pahali maneno haya yanaposamehewa, hapana toleo tena kwa zambi.*" Ndiyo, kama Mungu asipokumbuka zambi zetu tena kamwe, hatuhitaji zabihu nyingine kwa zambi. Tusifu Mungu kwa neema yake kubwa na kwa sababu ametusamehe zambi zetu zote.

### *10:19-20*

Toka mwisho wa sura 4 na kufika hata sura 10 tumesoma juu ya ukuhani wa Bwana Yesu. Tunapata majumlisho ya mafundisho haya sasa:

Kwa sababu ya zabihu ya Mwokozi wetu sisi watu bule tuna ukaramisu kuingia Pahali Patakatifu (bila shaka mwandishi alikuwa akiwaza juu ya Pahali Patakatifu pa patakatifu ndani ya hema). Neno la ajabu kabisa. Tunaweza kufika mbele ya Mungu na kumwambia maneno yote yaliyo rohoni mwetu. Tukiitwa kwa nyumba ya mutu mukubwa hapa duniani, tunaingia na kutetemeka na tunaogopa kusema neno. Lakini tunaweza kufika mbele ya Mungu na ukaramisu na tuna ruhusa kumwambia maneno yo yote tunayotaka! Hatuhitaji kuogopa hata kama yeye ni Mungu mukubwa na mutakatifu kwa sababu tuna Kuhani Mukubwa anayesimama pamoja nasi (sh.21).

Mbele ya kuendelea, tuwaze tena juu ya maneno haya: *''tuna uhodari wa kuingia Pahali Patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyoanza kwa ajili yetu, mpya, na hai, katika pazia, ndio mwili wake''* (sh.20). Labda unafazaika juu ya pazia hili. Ndani ya barua kwa Waebrania pazia ni mufano wa maneno mawili mbalimbali. Soma 6:19-20 tena pamoja na 10:20. Ndani ya sura 6 pazia si mwili wa Kristo kama ndani ya sura 10. Ndani ya sura 6 tunasoma ya kwamba Kristo aliingia ndani ya pazia, maana yake ameondoka hapa duniani na kupita kwa pazia linalotenga dunia tunayoweza kuiona na pahali Mungu anapokaa, ndipo pahali tusipoweza kupaona sasa. Pazia hili litaondoshwa siku Kristo atakaporudi kutawala juu ya dunia.

Lakini ndani ya 10:20 pazia ndilo mwili wake na tunaona ya kwamba tuna uhodari wa kuingia Pahali Patakatifu kwa damu ya Yesu, katika pazia, ndio mwili wake. Tuliona mbele ya kwamba kulikuwa na vyumba viwili ndani ya hema ya Mungu vilivyotengwa na pazia. Kwa sababu ya pazia lile njia ya kuingia Pahali Patakatifu pa patakatifu ilifungwa na watu hawakuwa na ukaramisu kuingia pale. Kwa sababu ya pazia lile makuhani waliweza kufanya kazi yao kwa Mungu ndani ya chumba cha kwanza. Waliweza kugusa pazia hata kama walikuwa watu wa zambi na hata kama Mungu alikuwa kwa ngambo yake nyingine.

Pazia hili ni mufano kwetu wa Bwana Yesu Kristo wakati alipokuwa hapa duniani. Alitengenezewa mwili na alisema mwili huu ulikuwa hekalu la Mungu.

### *Mwili wa Kristo ulikuwa pazia*

*''Katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu''* (Wakolosayi 2:9). Hata hivi kahaba na mutoza kodi waliweza kufika karibu na Yesu na zambi zao zote na mahitaji yao yote, na waliweza kumugusa. Waliweza kugusa mwili ule mutakatifu hata kama Mungu mutakatifu alikaa ndani yake. Hawakuweza kufika karibu na Mungu mbinguni kwani yeye ni mutakatifu, lakini waliweza kugusa mwili wa Yesu. Kwa nini? Kwa sababu mwili wake ulikuwa kama pazia.

Labda unafikili, "Kama ningalikuwa pale kwa wakati Bwana Yesu alipokuwa dunianil" Kweli Mungu alikuwa karibu sana na watu wakati mwili wa Yesu ulipokuwa duniani. Lakini tulete asante kwa sababu sasa tunaweza kufika karibu zaidi na Mungu. Kwa wakati ule mwili wa Yesu ulikuwa pazia lakini tulisoma mbele kidogo ya kwamba alitoa mwili ule kwa Mungu kama zabihu. Kwa miaka 33 mwili ule ulifanya kazi ya pazia lakini wakati Bwana Yesu alipokufa juu ya musalaba, mwili ule haukufanya kazi ya pazia tena - uligeuka zabihu. Alitoa kwa Mungu mwili ule usiokuwa na zambi.

Mungu alipokea zabihu ya Yesu na sasa Yesu ameingia Pahali Patakatifu pa patakatifu kwa ajili yetu, na mwili wa utukufu wake, na ameketi kwa kuume wa Mungu. Nasi vilevile tunaweza kuingia Pahali Patakatifu kwa sababu pazia haliko tena. Tunaweza kuingia *kwa roho* sasa. Kwa wakati wa kuja *miili yetu* itaingia vilevile.

Labda unataka kuuliza juu ya maana ya kupasuliwa kwa pazia ndani ya hekalu. Wakati Bwana Yesu alipokwisha kutoa mwili wake kama zabihu alisema, *Imekwisha*. Mungu alipokea zabihu ile, zabihu mpya, na alisema kazi ya zabihu za zamani ilikwisha. Hivi kama mutu anavyopasua barua asiyoihitaji tena, Mungu alipasua pazia lile kwa sababu kazi yake ilikwisha kwa milele.

### *10:21-25*

Hivi tunaweza kufika mbele ya Mungu na uhodari. Tukaribie basi kwa moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, mioyo yetu ikikwisha kunyunyizwa na damu ya Kristo kwa kuacha zamiri mbaya, na miili yetu ikioshwa kwa maji safi. Tufanye maneno mawili mengine vilevile, kama tunavyosoma ndani ya mashairi 23-25. Tushike sana kukiri kwa tumaini letu, kusudi lisigeuke. Maana yake tusimame imara kwa imani yetu na kukiri ya kwamba tunatazamia kuja kwa Mwokozi wetu. Na tuangaliane vilevile kwa njia ya kusukumana katika mapendo na kazi nzuri tukifahamu ya kwamba siku ya kuja kwa Kristo inakaribia. Tusaidiane na kupatishana nguvu ndani ya kazi yetu kwa Bwana ili tusilegee kufika siku Mwokozi wetu atakapokuja.

### *MAONYO, 10:26-39*

Mashairi haya ni maonyo zaidi kwa Wayuda wale waliokiri ya kwamba wao ni Wakristo lakini kuna mafundisho kwa sisi vilevile. Maneno haya yote yalielezwa mbele. Kazi ya zabihu za Agano la Kale ilikwisha hata kama makuhani hekaluni waliendelea nayo. Hivi haikuwezekana tena kwa Mukristo wa kweli aliyepokea zabihu ya Kristo kwa wokovu wake kuendelea na maneno yale ya zamani. Kujaribu kufanya hivi kulikuwa kuzarau Kristo na zabihu yake. Halafu nini itatokea kama wakichagua kukataa kuachana na zabihu za zamani?

Kama wakiendelea na zabihu zile *wanakanyaga Mwana wa Mungu na kuhesabu damu ya agano waliyotakaswa nayo kitu kichafu* (sh.29). Wanakataa ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, hivi kwa macho yao damu yake ni sawasawa na damu ya watu wote na wanahesabu agano jipya kuwa kitu bule. Kwa njia ya kufanya hivi wanatukana Roho ya neema, ndiye Roho Mutakatifu aliyewafahamisha habari za usamehe na wokovu bila kutenda kazi njema. Wanamuzarau kama wakirudi tena kwa dini inayofundisha tunahitaji kufanya kazi njema kwa kujipatia wokovu.

Kwa sababu ya zabihu kamilifu ya Kristo tunakubaliwa na Mungu hata sasa. Basi kwa nini hatupelekwi mbinguni mara moja? Imependeza Mungu kutuacha hapa duniani kwa wakati kusudi tutumikie Kristo na kupata mateso kwa ajili yake kwa kupima imani yetu na kuonyesha ya kwamba ni imani ya kweli. Tunahitaji zaburi vilevile, ili tukikwisha kufanya mapenzi ya Mungu tupate ile ahadi (sh.36; 9:15).

Kwa sababu hii tukae na ange wakati tunapohubiri Habari Njema kwa wasioamini. Sharti tuwafahamishe ya kwamba pamoja na usamehe na furaha watakayopata wakati wanapoamini Yesu watapata majaribu na mateso vilevile katika dunia hii iliyo kama jangwa. Watahitaji uhodari na roho ya kudumu ili wakikwisha kufanya mapenzi ya Mungu wapate ile ahadi.

Lakini pamoja na kuwaambia ya kwamba watapata taabu na mateso tuwajulishe vilevile ya kuwa ni kwa muda mufupi tu. *"Kwa kuwa bado kidogo sana yeye anayekuja atakuja, wala hatakawia"* (sh.37).

Mungu anatazama toka mbinguni na anafurahi sana wakati anapoona watoto wake wakisimama imara. Lakini kama akiona mwingine akirudi nyuma, kushikamana na maneno ya dunia na kuepuka mateso kwa ajili ya Kristo, atasema juu ya mutu yule, *"roho yangu haina furaha naye"* (sh.38). Mutu anayefuata njia ile atapotea kwa milele (sh.39).

Tuwaze sana juu ya maneno haya na kusimama imara katika imani tukikumbuka ya kwamba bado kidogo sana Mwokozi wetu atakuja wala hatakawia.

# *Imani*
# *Sura 11*

Mafundisho makubwa ya sura hii ni imani. Imani ndiyo neno wasomaji wa barua hii walilolihitaji sana. Mwenendo wao ulikuwa umeamsha shaka ndani ya roho ya mwandishi kama walikuwa wameamini kweli kweli.

Mwandishi aliwakumbusha mbele ya kwamba baba zao hawakuingia inchi ya ahadi kwa sababu walikosa imani. Halafu kwa mwisho wa sura 10 alijumlisha mafundisho yake yote. Alisema iliwapasa kuchagua, *ao* kuendelea mbele wakingojea kuja kwa Bwana na saburi, wakiishi kwa imani (kwani Mungu alisema *"mwenye haki ataishi kwa imani"*) *ao* kurudi nyuma, maana yake kukataa maneno yale waliyosema waliyaamini mbele, na kupotea kwa milele.

### *IMANI NI NINI? 11:1-2*

Mwandishi anaendelea sasa na kueleza kama imani ni nini na kama kazi yake ni nini. Tumeona tena na tena ndani ya barua hii ya kwamba mutu hawezi kupendeza Mungu bila imani na ya kwamba hawezi kuwa mwamini bila imani. Waisraeli jangwani tuliosoma habari zao ndani ya sura 3 na 4 hawakuamini Habari Njema. Hawakuwa waamini hata kidogo.

Tufahamu vilevile ya kwamba kuna imani namna moja tu. Tunazaliwa tena kwa njia ya imani na nyuma yake tunakaa kuishi kwa imani ile ile tu, si kwa imani namna nyingine. Labda tuna imani ndogo tu wakati tunapoanza kutembea pamoja na Mungu, lakini imani hii inaweza kupata nguvu na kuwa na uhodari na kufanya kazi. Haiwezekani kuficha imani ya kweli - sharti ionekane ndani ya maisha yetu na kugeuza maisha yetu kwani imani ya kweli ina uzima ndani yake.

Ni kweli ya kwamba tunaokolewa bila kutenda kazi njema. Tunaokolewa kwa njia ya kuamini tu; tunapokea wokovu kwa imani.

Lakini imani ya kweli inafanya kazi vilevile. Mwanamuke mwenye zambi katika Luka 7:36-50 aliamini Mwokozi na kwa sababu hii alianguka mbele yake na kunawa miguu yake na machozi yake. Mwanamuke mwenye kutoka damu alimwamini na kwa sababu hii alimukaribia katikati ya makutano na kugusa vazi lake. Mutu anayeamini Bwa-

na Yesu kweli anafika karibu naye na kunyolosha mikono yake kupokea wokovu Bwana anaotaka kumupa.

Mwandishi wa barua hii alikuwa ameonyesha wazi kabisa kwa Waebrania waliopokea barua hii ya kwamba wakiamini Kristo kweli kweli kama Masiya wao, iliwapasa kujitenga kabisa na dini ya Wayuda na hekalu lake na zabihu zake. Iliwapasa kuacha maneno haya yote na kufuata Masiya aliyekataliwa, na kufungana na Wakristo wengine waliozarauliwa na Wayuda wenzao. Hawatahesabiwa kama Wayuda tena, lakini watakatiliwa mbali kama wafu. Labda watakataliwa hata na jamaa zao kama Paulo aliyepata hasara ya maneno yote kwa ajili ya Kristo (Wafilipi 3:8). Labda nyumba zao na vitu vyao vitanyanganywa nao wenyewe watafungwa gerezani. Ndiyo, iliwapasa kufahamu vizuri maana ya kuamini Kristo. Ni kutembea kwa imani, hata kama wakipotewa vitu vyote.

Hivi ndani ya mashairi 1 na 2 tunaona ya kuwa imani ni hakika ya maneno yanayotumainiwa (maneno usiyoyapata bado). Unaamini ya kwamba maneno haya ni yako - kwa mafikili yako ni kama umeyapokea hata sasa. Ahadi nyingi za Mungu zitatimizwa kwetu kwa wakati wa kuja tu, lakini kwa imani ni kama zimetimizwa kwetu hata sasa. Tunatumika na imani namna hii mara nyingi. Tunaamini ya kwamba Bwana Yesu atakuja tena, lakini hajafika bado. Tunaamini yeye ni mbinguni, lakini hatuwezi kumwona pale. Tunaamini anatuombea kila siku lakini hatuwezi kusikia maombi haya na masikio yetu. Tunaamini Bwana Yesu alifufuliwa toka wafu, lakini hatukuwa duniani kwa wakati ule. Tunaamini maneno haya yote na tumeona ya kwamba ni maneno ya kweli. Ndiyo, imani ni kuwa na hakika ya maneno tunayoyatumaini, kusadiki sana maneno yasiyoonekana.

### *HATUWEZI KUPENDEZA MUNGU BILA IMANI, 11:3-6*

Sasa tutasoma maneno matatu mengine juu ya imani:

1) Juu ya kuumbwa kwa dunia tunasoma: *''Kwa imani tunafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu.''*

2) Kwa imani Abeli alitolea Mungu zabihu nzuri kupita Kaina.

3) Juu ya kutukuzwa tunasoma: *''Kwa imani Enoka alihamishwa asije akaona mauti.''* Halafu shairi 6 linajumlisha maneno haya matatu: kuumbwa kwa watu, kukombolewa kwao, na kutukuzwa kwao.

*Kuumbwa kwa dunia.* ''Kwa imani tunafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyoonekana.'' Tunaona na macho vitu vinavyotuzunguka, tunaweza kuvigusa na kuvinusa na kuvionja, lakini vitu hivi vyote vilitoka wapi? Vilikuwa tangu milele? Sivyo; vilifanywa toka vitu tusivyoweza kuviona na macho.

*Ukombozi.* Lakini dunia hii Mungu aliyoiumba ilikologana. Abeli alikuwa mutu wa kwanza aliyeonyesha ya kwamba aliamini Neno la Mungu juu ya kukologana kwa dunia. Alionyesha imani yake namna gani? Kwa njia ya kutoa zabihu nzuri zaidi kupita Kaina. Mungu alikuwa amesema udongo ulilaaniwa kwa sababu ya zambi. Abeli aliamini neno hili na kwa sababu hii alileta zabihu ya damu. Kaina hakuweka roho juu ya kulaaniwa kwa udongo na alileta toleo lisilokuwa na damu. Na kweli Kaina na Abeli walihitaji imani kuamini ya kwamba dunia ilikuwa imelaaniwa kwa sababu ilionekana kwanza vizuri kama siku Mungu alipoiumba. Basi Abeli aliamini Neno la Mungu na alionyesha imani yake kwa njia ya kutoa zabihu yenye damu. Lakini inatushinda kufahamu namna gani watu wa sasa wanaweza kufikili maneno yote yanatembea vizuri duniani wakati tunapoweza kuona pahali pote uharibifu ulio matunda ya zambi na laana.

*Kutukuzwa.* Kwanza inatupasa kuamini ya kwamba Mungu aliumba dunia hii toka vitu visivyokuwa mbele. Nyuma yake inatupasa kuamini ya kwamba dunia hii imelaaniwa kwa sababu ya zambi kwani tunaweza kuona matunda ya laana hii. Ni kwa sababu hii tunahitaji kukombolewa. Halafu wote wanaoamini Mungu hivi wanangojea na furaha neno kubwa lingine litakalotokea nyuma kidogo. Bwana atakuja na halafu wao wote watapelekwa mbinguni kama Enoka alivyopelekwa mbinguni.

Tunafahamu maneno haya yote kwa imani kwa sababu pasipo imani haiwezekani kupendeza Mungu, kwa maana sharti mutu anayekuja kwa Mungu aamini ya kuwa Mungu yuko na ya kwamba anawapa zawabu wale wanaomufuata. Matendo yetu yataonyesha kama tukiamini kweli. Tutaona ndani ya maisha ya Noa, Abrahamu, Sara na Isaka kama imani ya kweli inazaa matunda ya namna gani.

### *11:7-19*

#### *Matunda ya imani, 11:7-12*

Kwa imani Noa akikwisha kuonywa na Mungu alitengeneza safina na kwa njia hii alihukumu dunia, akakuwa muriti wa haki inayopatikana kwa imani. Ndiyo, Noa alitaka kujiponyesha mwenyewe pamoja na watu wa jamaa yake. Labda hakukusudi kuhukumu watu aliokaa katikati yao kwa njia ya kujenga safina, hata kama alihubiri na kuonya watu juu ya maneno yatakayowapata. Lakini hata kama Noa asingalisema hata neno moja, tendo lake la kutayarisha safina hii kujiponyesha toka garika lilikumbusha watu ya kwamba garika lilikuwa likikaribia.

Ni vivyo hivyo leo. Mungu hakutuagiza kujenga safina, na hukumu inayokaribia ni namna nyingine na hukumu kwa wakati wa Noa. Lakini huwezi kuwa Mukristo wa kweli bila kuhukumu dunia. Watu wengine

wanasema: Ndiyo, ninaamini Yesu, lakini wengi wa rafiki na jirani zangu hawaamini na sitaki kusema nao wanaanguka.'' Huwezi kuamini Kristo hivi. Kama ukiamini Habari Njema kweli kweli unaamini ya kwamba watu wale wanaoikataa watapotea. Unangojea kuja kwa Kristo kutuokoa toka gazabu itakayoangukia dunia hii. Basi kwa njia ya kungojea Mwokozi wetu tunaonyesha ya kwamba dunia hii itahukumiwa wakati Mwokozi atakapokuja.

*Abrahamu* aliamini vilevile. Wakati alipoitwa aende pahali atakapopata uriti alitii, akakwenda. Hakuweka roho kama alikuwa akienda wapi. Alifurahi tu kutoka katika maneno ya dunia pale kwa Uri, muji uliotawaliwa na Shetani, akageuka musafiri na mugeni. Imani ya kweli itatulazimisha sisi vilevile kutenda vivyo. Kama sivyo, hatujafahamu vizuri bado Habari Njema ile tunayosema tunaiamini.

Lakini tukiwa na imani ya kweli, hatutawaza tu juu ya hukumu itakayopata dunia hii. Tutatazama mbele kwa maneno mazuri Mungu atakayoyafanya. Wakati Abrahamu alipoondokea Uri, hakutazamia inchi ya Palestina tu, lakini zaidi ya ile alitazamia muji wenye musingi, ndio mwenye kuujenga na kuufanya ni Mungu (sh.10).

Ni kama Abrahamu alisema: ''Dunia hii nzima, hata inchi ya Palestina, itaharibiwa siku nyingine. Mimi ninatazamia muji muzuri zaidi, wenye misingi mizuri kupita usioharibika kamwe. Ninakubali kuwa musafiri na mugeni hapa duniani kufika siku itakapopendeza Mungu kunipeleka kule.''

Watu wenye imani ya kweli wanafanya hivi kila mara. Hata tukiwa kwanza ndani ya dunia na kufurahi na vitu vizuri Mungu anavyotupa sisi hapa tunakumbuka ya kwamba dunia hii ni kwa wakati tu - na tutafikia pahali pazuri zaidi. Ni kama kwa roho tumeondokea dunia hata sasa.

Halafu tukae bule tu kufika siku ile tutakapofika mbinguni? Sivyo. *Sara* aliamini vilevile. Alitazamia muji ule mukubwa mbinguni vilevile, na kwa imani alipokea uwezo katika mwili wake kupata mimba na kugeuka mama ya milioni za watu watakaokaa ndani ya muji ule. Abrahamu na Sara waliamini kabisa ya kwamba Mungu atatengeneza pahali pazuri kupita dunia yetu ya sasa hata walianza kutayarisha watu kukaa ndani ya pahali pale.

Wala si kwa maneno ya mwili tu. Abrahamu na Sara ni wazazi kwa maneno ya roho ya watu wote wanaoamini. Tushukuru Mungu kwa imani ya Abrahamu na Sara. Na tuwaige na kutayarisha watu kukaa mbinguni kwa njia ya kuwahubiri Habari Njema.

*Kufa katika imani, 11:13-16*

Watu hawa wote walikufa katika imani. Kama Abrahamu angalitaka kurudia Uri kama angaliweza kwani watu wa Uri hawakumu-

fukuza. Lakini hakutaka kurudi. Aliweka roho juu ya pahali pazuri zaidi, pahali pa mbingu.

Abrahamu alikuwa mutajiri na mutu mwenye heshima wakati alipokuwa kwanza kwa Uri. Alikuwa na mali nyingi hata nyuma ya kuondoka kwa Uri kwa sababu ya agizo la Mungu lakini hakuwa tena na heshima aliyokuwa nayo katikati ya watu wa Uri. Halafu siku atakapofikia ule muji Mungu anaotayarisha atakuta ni muzuri kupita mafikili yake yote. Ataona ya kwamba Mungu alifanya hata kupita maneno aliyoyasema. *"Kwa sababu hii Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea muji"* (sh.16).

Mungu anajua maneno yote watu wake waliyoacha kwa ajili yake. Anajua taabu na hasara yote wanayoipata, na kuumia na machozi yao yote. Anajua vilevile ya kwamba wakati watakapofika mbinguni wataona mateso yao yote yalikuwa madogo tu wakati yanaposawanishwa na utukufu unaowangojea pale. Kwa sababu hii Mungu hatakuwa na haya kuitwa Mungu wao kwa sababu Mungu tu aliweza kutayarisha muji muzuri namna aliowatayarishia. Hivi tunaweza kutazama mbele na tumaini hata kama sasa tunapata hasara nyingi kwa sababu ya imani yetu.

*Mapimo ya imani, 11:17-19*

Imani ya Wakristo inasimama juu ya Neno la Mungu. Imani hii inapimwa kwa njia mbalimbali. Inapimwa na Mungu na inapimwa na dunia. Inapimwa wakati maneno yetu yanapotembea vizuri na wakati yasipotembea vizuri.

Ndani ya shairi 17 tunaona namna imani ya Abrahamu ilivyopimwa. Mungu alikuwa amemupa Abrahamu ahadi nyingi na nzuri sana zitakazotimizwa ndani ya Isaka, lakini nyuma yake alimwomba kurudisha Isaka kwake na kukaa kumwamini tu.

Ilikuwa vivyo hivyo na Wakristo wale waliokuwa katika dini ya Wayuda mbele na waliopokea barua hii. Walikuwa wameishi kwa miaka mingi wakiamini ya kwamba dini yao yenye ahadi nyingi ilikuwa zawadi toka Mungu. Lakini sasa iliwapasa kuacha maneno haya yote na kuamini ya kwamba Mungu atawapa maneno mazuri zaidi na ya kuwa siku nyingine atatimiza ahadi zile zote ndani ya Agano la Kale juu ya taifa la Israeli.

*11:20-22*

Hatusomi maneno mengi juu ya imani ya Isaka na Yakobo ndani ya Agano la Kale ila neno hili moja: Walitazamia wakati wa kuja. Yakobo alisumbuka maisha yake mazima kujipatia mali na heshima. Alikufa katika inchi ya kigeni. Mbele ya kufa kwake alisifu Yosefu kwa sababu ya heshima aliyokuwa nayo pale Misri? Alijisifu kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa mukubwa kupita Farao? (Kwani pasipo mabisha-

no mudogo anabarikiwa na mukubwa, 7:7, na Yakobo alibariki Farao.) Sivyo; aliacha maneno haya yote. Alitazamia wakati wa kuja saa Mungu atakapotimiza ahadi zake kabisa.

Na Yosefu vilevile, wakati alipofikia mwisho wa maisha yake, hakusema, ''Nimeendelea vizuri sana hapa Misri na ninataraji wana wangu watafanya vivyo.'' Sivyo. Alisema na Waisraeli kupeleka mifupa yake pamoja nao wakati watakapokwenda kwa inchi Mungu aliyoahidi kuwapa. Hakutaka kuwa mufalme wa Wamisri na hakutaka wana wake kuwa wafalme wao nyuma yake. Alijua ya kwamba kukaa kwa Waisraeli katika Misri kulikuwa kwa wakati tu na ya kuwa nyuma yake Mungu atatimiza ahadi alizozitoa mbele.

### *ZAWABU ZA IMANI, 11:23-30*

Ilikuwa vivyo hivyo na Musa. Musa alikataa usitawi wa Misri kwa njia ya kukataa kuitwa mwana wa binti ya Farao, na alichagua kuteswa pamoja na watu wa Mungu. Alihesabu ya kuwa kulaumiwa kwa Kristo ni utajiri wengi kuliko hazina ya Misri. Kulaumiwa kwa *Kristo*? Labda unataka kusema ya kuwa kwa wakati ule Kristo alikuwa hajazaliwa bado. Musa alijua habari za Yesu kweli? Sivyo, Musa hakujua habari za Yesu, lakini alijua habari za Kristo. Alijua ya kwamba Masiya atakuja atakayetawala dunia hii nzima. Hivi Musa hakutaka kuwa na heshima hapa duniani. Alitaka kusimama kwa upande wa Kristo wakati atakapokuja kutawala dunia.

Tusifikili tunaweza kushiriki ndani ya mambo ya utawala wa dunia hii, kazi ya serikali, na halafu wakati Kristo atakapokuja, kutia utawala wa dunia hii kwa mikono ya Bwana. Ndani ya kitabu cha Ufunuo tunaona ya kwamba watawala watashindana na Bwana sana wakati atakapokuja. Hivi sisi tunaomwamini tumusimamie sasa na uhodari. Tukiteswa pamoja naye sasa, tutatawala pamoja naye kwa wakati wa kuja.

Hivi kwa imani Musa alifanya Pasaka na kwa imani Waisraeli walipita kati ya Bahari Nyekundu (sh.29). Hatusomi juu ya imani yao wakati waliposafiri jangwani kwani mara nyingi walionyesha ukosefu wa imani kwa njia ya kunungunika kwao. Hata hivi kwa mwisho kuta za Yeriko zilianguka kwa sababu ya imani yao (sh.30). Umesikia watu wakisema kuta za Yeriko zilianguka kwa sababu ya tetemeko la inchi? Labda kulikuwa na tetemeko la inchi kweli. Lakini ilikuwa imani ya watu wa Mungu iliyosukuma Mungu kuangusha kuta zile kwa wakati ule na labda alitumia tetemeko la inchi kwa kuziangusha. Neno kubwa ndilo hili: Aliziangusha kwa sababu ya imani yao.

### *IMANI BILA WOKOVU, 11:31-40*

Watu wengi wengine walifanya matendo ya ajabu kwa sababu ya

imani (sh.32). Lakini haifai tusahau kundi kubwa la watu waliokuwa na imani vilevile lakini walioteswa na hata kufa kwa sababu ya imani ile. Mungu hakuponyesha watu wale. Ni kama hakusikia maombi yao na watu wa dunia waliwazarau wakisema: Faida ya imani yenu ni nini? Ni upumbafu kufikili Mungu ni kwa upande wenu na atawalinda ninyi.''

Sharti tufahamu ya kwamba Mungu haponyeshi kila mara watu wale wanaomwamini. Unakumbuka ya kuwa Petro aliponyeshwa toka gereza lakini Yakobo aliuawa kwa upanga? Sharti tuamini Mungu kabisa hata ikitupasa kufa, tukitazamia wakati wa kuja.

Tunasoma jina la mumoja aliyeteswa hivi *bila kuponyeshwa*, ndiye *Yesu* (12:1-2). Yeye ndiye mwenye kuanzisha na mwenye kutimiliza imani yetu. Ndiyo, alikufa musalabani lakini alifufuliwa tena na sasa anaketi kwa mukono wa kuume wa Mungu naye ni juu ya maneno yote ya dunia hii. Itakuwa vivyo hivyo kwetu. Ukiamini Kristo na kumufuata — hata ukipata mateso — wewe vilevile utaketi juu ya kiti chake cha kifalme, kama yeye alivyoshinda na kuketi juu ya kiti cha kifalme cha Baba wake.

Imani si neno tunalosikia rohoni tu kama tunavyosikia furaha ao huzuni. Wenye imani wanatumika na akili yao vilevile. Musa alitumika na akili yake wakati aliposawanisha kulaumiwa kwa Kristo na hazina za Misri, na alifahamu ya kwamba kulaumiwa kwa Kristo ni faida nyingi zaidi; basi alichagua lililokuwa na faida zaidi.

Mungu alisema na Abrahamu kumutolea Isaka. Abrahamu hakufahamu kama Mungu atatimiza ahadi yake namna gani, ndiyo ahadi kubariki Abrahamu kwa njia ya Isaka, lakini alimwamini hata hivi. Aliamini ya kwamba Mungu akitaka atoe Isaka kama zabihu Mungu atamufufua tena. Alifahamu maneno haya na akili yake na alilalisha Isaka juu ya mazabahu.

Na Bwana Yesu mwenyewe alikubali kuvumilia musalaba na kuzarau haya yake kwa sababu alikumbuka furaha iliyowekwa mbele yake. Alizarau haya ya kutundikwa juu ya musalaba mbele ya watu lakini hakuzarau musalaba. Ilimupasa kuvumilia taabu na maumivu ya musalaba. Alifanya hivi kwa sababu alifurahi kwa wewe na mimi kukombolewa na kukaa pamoja naye kwa milele. Ndiyo, kwa sababu ya furaha hii alikuwa tayari kuvumilia taabu ya musalaba! Mungu atupe sisi imani yenye akili namna hii ili tuchague yaliyo mazuri zaidi.

# *Mwenendo Katika Imani Sura 12 na 13*

Barua hii imetufundisha maneno mengi juu ya imani. Tumeona ya kuwa tunakubali habari nyingi kwa imani, habari za kuumbwa kwa dunia hii, habari za ukombozi wetu, habari za maneno yanayotungojea mbinguni. Tumeona vilevile ya kwamba wenye imani hawaweki roho sana juu ya maneno ya dunia hii. Tumeona ya kwamba wenye imani wanapata matata namna mbalimbali na mara nyingine Mungu anawashindisha lakini mara nyingine hawaondoshi katika taabu yao na inaonekana kwamba imani yao haina faida. Faida ya imani ya watu wale itaonekana wazi kwa wakati wa kuja na kwa saa ile Mungu atawapa zawabu.

Tumeona kwa nini watu wa Mungu kwa wakati wa Agano la Kale hawakuona kutimia kwa ahadi Mungu alizowatolea. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alitaka kutuingiza sisi ndani ya ahadi hizi vilevile. Hakutaka wakamilishwe bila sisi. Watu wa zamani wenye imani walingoja kutimizwa kwa ahadi za Mungu kwa mia za miaka. Asante kwa Mungu kwa sababu sisi hatutahitaji kungoja muda murefu namna hii kwani kuja kwa Bwana wetu ni karibu sasa.

### *KUMBUKENI BWANA, 12:1-3*

Halafu sasa tunaagizwa kumukumbuka yeye aliyevumilia mabishano makubwa namna hii ya wenye zambi juu yake, kusudi tusipate kuchoka wala kulegea katika nafsi zetu. Yalikuwa mabishano gani? Walibisha wakisema yeye si Kristo. Walibishana naye tena na tena juu ya neno hili.

Ilikuwa vivyo hivyo na Wakristo waliopokea barua hii. Watu walibishana nao saa zote juu ya imani yao. Wakubwa wa serikali na rafiki na ndugu zao — wote waliwachambua kwa sababu waliamini Yesu. Masemo yao makali yalikata na kuumiza roho za Wakristo. Basi nini iliweza kuwasaidia wasichoke na maneno haya na kulegea rohoni? Kukumbuka Yesu aliyevumilia mabishano makubwa vilevile.

*12:4-13*

Mashairi haya yanatufundisha juu ya mapigo ya Bwana. Labda taabu tunayoipata ni mapigo ya Bwana. Tusiyaone bule kwa sababu ni kwa faida yetu. Mungu angeweza kuondosha mara moja mateso yale tunayoyapata kama neno hili lingeweza kutusaidia vizuri kupita. Anafanya hivi mara nyingine lakini mara nyingine anaacha sisi kuteswa kwanza kwa sababu anajua mateso haya yatakuwa faida kwa roho zetu.

Kuna maneno mawili inayotupasa kuepuka:

1. Haifai tuone mapigo ya Bwana bule; tukiyaona bule, hayatakuwa na faida kwetu.
2. Haifai tulegee kama Bwana akituhamakia, kwani tukilegea, itapasa Mungu kuondosha mapigo yenyewe nasi hatutajifunza maneno aliyotaka kutufundisha.

Tusisahau kamwe ya kuwa yeye Bwana anayemupenda, anamutakasa kwa mateso. Ukiteswa sana, usilegee lakini fikili hivi: Bwana ananipenda sana! Kumbuka ya kwamba mateso haya ni kwa faida yako. Ndiyo, kama tusipopata mateso, ingetupasa kujiuliza kama sisi ni Wakristo kweli!

Maana ya neno linalotafsiriwa hapa ''mapigo'' si mapigo tu lakini ''mafundisho'' kama baba anavyolea na kufundisha mutoto wake. Baba wa dunia anafundisha mutoto wake na mutoto anamuheshimu. Baba muzuri haazibu mutoto wake kwa kumwua. Hamutumi kwa darasa kwa kumutesa lakini kusudi mutoto huyu aweze kuwa na maisha mazuri kupita kwa wakati anapopata nguvu. Vivyo hivyo Baba wetu mbinguni hakusudi kutuharibu lakini kututayarisha kwa maisha ya faida na baraka. ''Basi, si afazali sana kujitia chini ya Baba ya roho zetu na *kuishi*?'' (sh.9).

*Makusudi ya Mungu*

Kusudi la Mungu ni nini wakati anapotuacha kupata matata? Tuwaze kwanza juu ya mutoto mudogo. Anacheza jua zima na kukaa na furaha nyingi. Halafu wakati anapopata nguvu kidogo inamupasa kuanza darasa. Labda hapendi darasa. Hafurahi kukaa juu ya kiti na kujaribu kujifunza kusoma na kuandika. Angependa sana kurudi nyumbani na kuchezacheza kama mbele. Lakini miaka inapita, hata miaka kumi, naye amejifunza maneno mengi. Hatafurahi tena kuchezacheza kama mutoto mudogo. Sasa anataka kufanya maneno yenye faida kupita.

Mungu anafanya vivyo hivyo na watoto wake. Tulikaa na furaha nyingi wakati tulipokuwa waamini wa sasa, lakini nyuma ya muda fulani Mungu aliacha maneno magumu kutupata ili aweze kupatisha imani yetu nguvu tusikae watoto tu siku zote. Mungu hafikili tu miaka

michache tunapokaa hapa duniani lakini elfu elfu za miaka tutakayokaa mbinguni. Anataka kututayarisha kwa wakati ule. Basi tunyenyekee maneno anayotuma kwetu na kuamini ya kwamba yeye ni mwenye akili yote na anajua maneno yote yaliyo mbele yetu.

Ndani ya shairi 10 tunaona ya kwamba maneno Mungu anayotufundisha si kwa faida yetu hapa duniani tu lakini kusudi tuweze kushiriki utukufu wake. Wakati tunapogeuka Wakristo tunaingizwa ndani ya jamaa ya Mungu na Mungu anaweka roho sana juu ya mwenendo wa wana wake. Anataka watembee katika utakatifu. Ni kwa kusudi hili anatufundisha na kutuazibu.

Ndiyo, kwa wakati wa sasa azabu haionekani kuwa kitu cha furaha, lakini cha huzuni, lakini nyuma inazalia watu wale waliofundishwa nayo matunda ya haki yenye salama (sh.11). Tukumbuke maneno haya mawili: *lakini nyuma.* Azabu ile haitaendelea milele; itakwisha siku nyingine na halafu faida yake itaonekana wazi kabisa.

Tuwaze juu ya maneno mawili mengine ndani ya shairi 11: *waliofundishwa nayo.* Inawezekana kwa mwalimu kukaa kufundisha mutoto bila mutoto kujifunza neno! Wakristo wengine ni kama mutoto namna hii. Mungu anawafundisha na kuwaazibu lakini hata hivi hawajifunzi maneno anayotaka wajifunze. Tuweke roho sana kufahamu na kujifunza maneno Mungu anayotaka kutufundisha kwa njia ya maneno magumu anayotuma kwetu.

Baba wetu wa mbinguni anatujua sana. Anajua uzaifu wetu na mateso anayotuma kwetu yanafunua uzaifu ule kwetu. Hafanyi hivi kwa kutuzarau ao kutuhamakia lakini aweze kutupatisha nguvu. Tukifahamu neno hili hatutamwomba kuondosha mateso yenyewe lakini tutaomba yaweze kutupatisha nguvu na kutusafisha ili tuweze kupendeza Mungu vizuri kupita mbele.

### *ESAU, 12:14-17*

Ndani ya mashairi 14-17 kuna maonyo matatu. Tunaona tena ya kwamba kuna njia mbili mbele yetu na inatupasa kuchagua kama tutafuata njia gani. Ukiamini Kristo kweli na kushika njia ya imani utapata mateso. Mapimo na mateso si kwa watu wachache tu ndani ya Kanisa lakini kwa Wakristo *wote.* Lakini kuna njia nyingine vilevile. Tunaweza kuwa kama Esau. Kwa kufahamu maneno mwandishi anayotaka kutufundisha hapa tujikumbushe kwanza habari za Esau ndani ya kitabu cha Mwanzo. Unakumbuka sawasawa Esau na Yakobo walishindana hata mbele ya kuzaliwa (Mwanzo 25:22-26). Nyuma kidogo tunasoma namna Esau alivyouza uriti wake wa muzaliwa wa kwanza kwa chakula siku ile alipotoka polini bila mawindo (Mwanzo 25:29-34).

Maandiko Matakatifu hayaonyeshi wazi kama uriti wa muzaliwa

wa kwanza ulikuwa nini. Tunajua tu Esau hakuwa muzaliwa wa kwanza kwa sababu ya kazi yake mwenyewe lakini kwa sababu Mungu alikusudi hivi. Kwa wakati ule Isaka na Rebeka na wana wao walikaa kwanza ndani ya hema kama wasafiri, na ahadi Mungu alizowatolea mbele zilikuwa hazijatimia bado. Lakini siku ahadi hizi zitatimizwa Esau atapokea sehemu iliyowekwa kwa muzaliwa wa kwanza, ndiyo sehemu nzuri kupita sehemu ya wana wengine.

Lakini Esau hakuweka roho juu ya baraka zile atakazobarikiwa nazo kama muzaliwa wa kwanza *kwa wakati wa kuja* na aliona bule heshima na uwezo atakazokuwa nazo kwa wakati ule. Ahadi za Mungu zilikuwa nzuri sana lakini zilikuwa *kwa wakati wa kuja*. Lakini Esau hakutaka kujikana mwenyewe na kungojea baraka *kwa wakati wa kuja*. Sivyo, alitaka kukaa vizuri bila njaa na bila matata *sasa,* si kwa wakati wa kuja. Aliona ahadi za Mungu bule.

Esau alikuwa baba wa Waedomu. Mufalme Herode aliyetawala wakati Bwana Yesu alipokuwa duniani alikuwa Muedomu. Hakuwa Muyuda wala Muroma. Waroma walikuwa wakitawala inchi ya Yudea na Palestina kwa wakati ule. Wayuda waliwachukia na walitazamia kuja kwa Masiya. Walikuwa na tumaini kwani Mungu alikuwa amesema: *"Israeli ni muzaliwa wangu wa kwanza"* (Kutoka 4:22). Walisoma unabii ndani ya Agano la Kale ya kuwa Masiya atakuja na kuwafungua toka utawala wa wale waliowaonea na atafanyiza taifa lao kuwa na heshima kupita mataifa mengine. Walifikili maneno haya wakati wote. Kwa sababu hii, nyuma ya ufufuko wa Bwana Yesu wanafunzi wake walifika karibu naye na kuuliza: *"Bwana, utarudishia Waisraeli ufalme wao tena wakati huu?"* (Matendo 1:6).

Mungu alikuwa amesema: "Israeli ni muzaliwa wangu wa kwanza" na Waisraeli wenye imani walikuwa wakingojea kutimia kwa ahadi hii. Herode, mufalme wao, aliona maneno haya bule. Hakutaka kungojea Masiya atakayefika kwa wakati wa kuja. Alikuwa mufalme na alitaka kutawala yeye mwenyewe. Hivi alifanya mapatano na Waroma, na Waroma walimuweka juu ya Waisraeli kama mufalme. Wakati Bwana Yesu alipotokea Herode alijaribu kumwua kwa sababu hakutaka kunyanganywa ufalme wake. Alikuwa Muedomu na hakuweka roho juu ya ahadi za Mungu kwa wakati wa kuja. Alitaka faida na heshima yote saa ile ile.

Mwandishi hakutaka wasomaji wa barua yake kuwa watu wenye roho namna ya Esau na Herode. Kulikuwa na njia moja tu kuepuka mateso waliyokuwa wakiyapata, ndiyo kufikili kama Esau na kusema: "Siweki roho juu ya ahadi za Mungu kwa wakati wa kuja. Sipendi kuishi kwa imani. Sitaki kupata mateso na kukosa vitu na mali kwa ajili ya Kristo. Ninataka kukaa vizuri na kula vizuri *sasa.* Si neno kama

nikiwa na ushirika na watu wa dunia ao dini za uwongo — ninataka tu kujipatia vitu vizuri vyote ninavyovitamani. Ninaishi kwa wakati wa sasa tu na siweki roho juu ya ahadi zisizo na maana.''

### *SAYUNI, SI SINAI, 12:18-25*

Ndiyo, mwandishi hakutaka wasomaji wake kuwa kama Esau. Lakini njia mbili zilikuwa mbele yao na kuna njia mbili mbele yetu vilevile. Ao tunaweza kufuata Kristo sasa wakati anapokataliwa na kubeba musalaba wake. Ao tunaweza kufungana na watu wa dunia, kuepuka mateso, kujifurahisha na maneno ya dunia hii na kupoteza baraka zote za Mungu. Tuwaze sana juu ya maneno haya. Hatukufikia Mulima Sinai na mushindo wa ngurumo wake, wa kuogopesha sana. Sivyo, kwa maneno ya roho tumefikia mulima wenye kuogopesha zaidi, Mulima Sayuni.

Tumefikia Mungu, si sasa kama Baba wa watu wote, lakini kama Mwamuzi wa wote. Wakati Mungu aliposema toka Mulima Sinai, wengine walimukataa, wakakufa. Zaidi sana wale watakufa wanaomukataa yeye anayewaonya kutoka mbinguni!

Mungu anataka kutukokota kwake kwa njia ya mapendo, kwa njia ya baraka zote za wokovu Kristo anaotaka kutupa sisi. Kweli Mwokozi wetu ni Mwokozi wa ajabu kabisa na tunaweza kufurahia mateso yote tunayovumilia kwa ajili yake. Tufunge roho na kusimama na nguvu ndani ya mateso yenyewe. Lakini nini itatokea kama tukikataa kupata mateso, kama tusipomupenda na kumufuata? Bila Kristo uharibifu tu unatungojea — hata kama Mungu kwa njia ya Kristo alitayarisha njia kutuokoa toka uharibifu ule!

### *MUNGU ATATETEMESHA DUNIA, 12:26-29*

Mungu alitetemesha dunia mbele, lakini ameahidi ya kwamba nyuma kidogo ataitetemesha tena, wala si dunia tu, lakini mbingu vilevile. Ni kusema ataziondosha kabisa kwa sababu kutakuwa na mbingu na dunia mpya. Ni huzuni kuona watu wakifungana sana na maneno ya dunia hii, vitu wanavyoweza kuviona na macho, kwani nyuma kidogo vitu hivi vyote havitakuwa tena. Hata wakishikamana na vitu hivi, watabaki pasipo kitu kwa milele. Kristo tu anabaki kwa milele pamoja na wokovu Mungu anaotupa sisi kwa njia yake.

Tukumbuke maneno haya wakati tunapohubiri Habari Njema. Tuonyeshee watu mapendo makubwa ya Mungu na uzuri wa Kristo na ukubwa wa wokovu wake. Lakini tuwafahamishe vilevile ya kwamba kwa mateso mengi itatupasa kuingia ufalme wa Mungu (Matendo 14:22). Wakifika karibu na Mwokozi wakikokotwa na mapendo yake, itawapasa vilevile kuwa tayari kupata mateso kwa ajili yake. Tuwa-

ambie wazi ya kwamba kuna njia mbili tu: kuamini na kuokolewa: ao kurudi nyuma na kupotea kwa milele.

*MAONYO, SURA 13*

Barua hii imetupasha maneno ya ajabu kabisa juu ya uzuri na utukufu wa Mwokozi wetu. Ndani ya sura yake ya mwisho kuna maagizo na maonyo mengi kwa maisha yetu ya kila siku. Tusione sura hii bule lakini tuweke roho sana kutimiza maneno haya ndani ya maisha na mwenendo wetu.

*13:1*

Maonyo ndani ya sura hii si nguvu kufahamu, lakini ni nguvu kuyatii. Wakristo waliopokea barua hii walikuwa wakiteswa sana na mwandishi aliwaonya kukaa kupendana kwani neno hili litawasaidia kusimama imara katika mateso. Maonyo haya ni kwa sisi vilevile. Kwa wakati wa mateso Wakristo hawakumbuki tena maneno madogo madogo yanayowagawa na Wakristo wengine, lakini sharti wakae kupendana kama ndugu.

*13:2-3*

Hata kwa wakati wa sasa Wakristo katika inchi nyingine, ndugu zetu katika Kristo, wanafungwa na kuteswa gerezani kwa sababu ya imani yao. Tuwakumbuke na kuwaombea siku zote.

*13:4-6*

Tuwaze zaidi juu ya mashairi 5 na 6. Tunasubutu kusema, ndiyo tuna uhodari kusema: *"Bwana ni Mwenye kunisaidia; sitaogopa."* Kwa nini? Kwa sababu Mungu aliahidi hatatupungukia kabisa wala hatatuacha hata kidogo!

Labda una rafiki anayefungana nawe kabisa lakini mara nyingine anakupungukia kwa sababu hana nguvu ao akili ya kutosha kukusaidia katika kila neno. Mungu wetu si hivi. Ameahidi kuwa pamoja nasi hata mwisho naye hatatupungukia kamwe!

Hivi tuwe wafungulifu kwa mapendo ya mali, maana tusiweke roho sana juu ya mali. Ndiyo, tunahitaji mali kwa kuishi hapa duniani, lakini tusijivimbishie mali nyingi. Bwana ameahidi kuwa pamoja nasi na kwa sababu hii tunaweza kusema na uhodari: *"Bwana ni mwenye kunisaidia; sitaogopa; watu watanifanyia nini?"* Neno baya zaidi wanaloweza kulifanya ni kuua miili yetu, lakini hili si baya kweli kwani tutafika karibu na Bwana Yesu mara moja.

*13:7-8*

Bila shaka wengine wa viongozi wale walikuwa wamekufa. Walikuwa watu wa Mungu kabisa waliokaa pamoja na mitume. Wengine

walisikia masemo ya Bwana Yesu na masikio yao wenyewe. Ni desturi yetu sisi watu kufikili ya kuwa wale waliokufa walikuwa wazuri kupita na wenye imani kubwa kupita watu wa sasa. Lakini haifai kwetu kuwalilia. Kwa pahali pa kuwalilia ingetupasa kujaribu kuwaiga. Ndiyo, walikuwa watu wa imani, lakini bila shaka wangekubali ya kwamba imani yao na uwezo kuishi maisha matakatifu zilitoka kwa Yesu Kristo tu. Viongozi wa wasomaji wa barua hii walikuwa wamekufa, lakini Yesu Kristo anabaki. Tushukuru Mungu kwa sababu Mwenye uwezo wote, yule anayeweza kutupa sisi uwezo, ni pamoja nasi leo kama alivyokuwa pamoja na watu wa Mungu wa zamani. *"Yesu Kristo ni sawasawa, jana, leo, na hata milele."*

*13:9-14*

Basi kama wasomaji wa barua hii wakiachana na dini ya Wayuda, iliwapasa kutembea namna gani? Sharti wakae na ange kwa mafundisho namna namna, zaidi juu ya vyakula kwa sababu maneno haya hayana faida. Dini ya Wayuda ilitoka kwa Mungu na ilikuwa na maagizo mengi juu ya vyakula na vinyweo na masafisho na siku takatifu. Damu ya zabihu nyingine ililetwa ndani ya Pahali Patakatifu pa patakatifu na kitumba cha sadaka ile ilipelekwa inje ya kambi ya Israeli na kuteketezwa pale. Kuhani mukubwa aliyetoa zabihu hii hakupewa nyama yake kwa chakula chake.

Maneno haya yalikuwa mufano wa Bwana Yesu aliyeteswa inje ya lango (maana yake akatoka kati ya mambo ya dini ya Wayuda) kusudi atakase watu wake kwa damu yake mwenyewe. Aliacha maneno ya dini ya Wayuda na alikwenda inje ya lango kwa kutoa zabihu kwa zambi zetu. Lakini wale wanaoshikamana na dini ya Wayuda hawapati faida kwa njia ya zabihu hii, kama vilevile kuhani mukubwa aliyeleta zabihu ndani ya Pahali Patakatifu pa patakatifu hakuweza kula nyama yake.

Ndiyo, Mungu ameacha maneno ya dini ya Wayuda sasa na Mwana wake alikufa inje ya kambi. *"Basi twende kwake inje ya kambi tukichukua laumu lake."* Si neno kama watu wakizarau kazi kubwa Bwana Yesu aliyoifanya musalabani wakati alipokufa kwa zambi zetu. Si neno kama wakituona bule kwa sababu hatuna makuhani wenye mavazi ya mapambo mengi wala nyumba nzuri kukutana ndani. Tusiache mazarau ya watu kuchokoza roho zetu lakini tukumbuke kwamba hapa hatuna muji unaodumu, lakini tuko wasafiri tu, hivi tusifungane na dini za watu.

*13:15*

Tusijitenge tu na dini za watu, maneno yasiyo na faida, lakini tuweke roho juu ya yale yaliyo na faida kweli, ndiyo zabihu ya sifa na

mashukuru, tunda la midomo yetu inayokiri jina lake. Zabihu namna hii inatukuza na kupendeza Bwana zaidi.

*MAOMBI YA MWISHO, 13:20-21*

Mungu alijua ya kwamba tunahitaji muchungaji kutuongoza ili tuweze kutembea katika utakatifu, hivi alifufua Bwana Yesu aliye Muchungaji mukubwa wa kondoo kwa sababu alikumbuka agano lake kutufanyiza watakatifu kwa damu ya Yesu. Vizuri sisi vilevile tuweke roho sana ili maneno yanayoandikwa ndani ya shairi 21 yatimizwe ndani ya maisha yetu.

*13:22-25*

Waamini waliopokea barua hii ni pamoja na Bwana Yesu sasa katika utukufu. Hatujui kama Bwana wetu atakuja tena mwaka gani ao siku gani lakini labda nyuma ya muda mufupi tu tutakuwa pamoja naye na pamoja nao kwa milele!

IMPRIME AU CANADA